# Nipashe

Jumatano Juni 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579936

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




Siasa

UCHAMBUZI:

Kimataifa

TUNAPOELEKEA katika uchaguzi tusisahau kila uhuru una mipaka yake

Trump ataka mpango mkubwa wa kibiashara na Uingereza

EAC na changamoto za Rwanda 'kujiekeleza' DRC

UKURASA 13



**Mwalimu shule ya msingi anaswa na silaha ya kivita**

UKURASA 2



*Eid El Fitri*

# Bodi mikopo elimu yalegeza masharti

**WAKOPAJI** sasa ruksa hadi umri wa miaka 35, vigezo vipya vyawekwa hadharani... *Endelea ukurasa wa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**PSSSF SASA KUTOWALIPA MAFAO WASIOHAKIKIWA**
MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umesema hautalipa...

UKURASA WA 3

**WASHTAKIWA KUCHAPISHA MAUDHUI BILA KIBALI TCRA**
WATU wanne wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi nne tofauti ikiwamo tuhuma za kuchapisha...

UKURASA WA 4

**SHAHIDI AFICHUA MAZITO KESI VIGOGO CHADEMA**
SHAHIDI wa nne Konstebo wa Polisi, Fikiri Mgeta (28) katika kesi ya uchochezi, amedai...




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akionyesha silaha ya kivita aina ya AK47 kwa waandishi wa habari, jana, aliyokutwa nayo Mwalimu Solomon Letato Kipuker (aliyefungwa pingu mikononi), wa Shule ya Msingi Naan, katika Kata ya Engserosambu, wilayani Ngorongoro. **P**

## Vitambulisho machinga vyaibua makubwa

UKURASA 3

# Waziri afichua siri nzito mikopo ya nje

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAZIPELEKA YANGA, KMC CAF UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Waombaji mikopo elimu juu walegezewa masharti

Na Beatrice Moses

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetoa mwongozo na kuboresha vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi, ikiwamo kuongeza umri wa waombaji mikopo kutoka miaka 33 hadi 35.

Akizungumza jana na waaandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema kuwa wametoa mwongozo huo kwa utoaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 unaotaja sifa, vigezo na utaratibu.

Badru aliwataka waombaji wa mikopo kuusoma mwongozo huo ili waweze kuandaa nyaraka muhimu zinazotakiwa, kabla ya kufunguliwa kwa mfumo wa maombi kwa njia ya mtandao Juni 15, 2019 na utafungwa Agosti 15, 2019.

Alizungumzia pia kuhusu kuboreshwa baadhi ya vigezo vya utoaji mikopo kwa lengo la kuwafikia wanafunzi wahitaji wengi zaidi, hasa baada ya kuzingatia maoni ya wadau wa elimu.

"Tumeongeza umri wa waombaji mikopo kutoka miaka 33 hadi 35 na pia mwaka huu tutapokea maombi kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita au stashahada ndani ya miaka mitano iliyopita awali ilikuwa miaka mitatu," alisema Badru.

Alisema katika mwaka wa masomo 2019/2020, Serikali kupitia HESLB imepanga kutoa mikopo na ruzuku ya elimu ya juu yenye thamani ya Sh. bilioni 450 kwa jumla ya wanafunzi 128,285.

"Kati ya hao, wanafunzi 45,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza, mwaka huu 2018/2019, unaoelekea mwisho jumla ya Sh. bilioni 427.5 zilitolewa kwa jumla ya wanafunzi 123,000," alisema.

"Tofauti na miaka mingine, mwaka huu tunatoka kivingine tunatoa takribani wiki mbili kuanzia leo (jana) kwa waombaji kusoma mwongozo na kuandaa nyaraka muhimu, baada ya wiki mbili, tutafungua mfumo wa kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao," alisema.

Badru alibainisha kuwa mfumo huo unatarajiwa kufunguliwa kuanzia Juni 25 hadi Agosti 15, 2019,

INAENDELEA UK. 26



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kushoto), akizungumza na wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga katika Soko la Kariakoo, jijini humo jana, wakati alipokuwa akikagua mwitikio wa matumizi ya vitambulisho kwa wafanyabiashara hao. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waziri afichua siri nzito mikopo ya nje

Na Sanula Athanas, DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amelieleza Bunge kuwa amesita kutia saini baadhi ya mikopo kutoka nje kutokana na masharti magumu yaliyowekwa na wakopeshaji.

Amesema baadhi ya masharti hayo ni kuchukuliwa kwa mali za jeshi na migodi iliyopo nchini endapo serikali itashindwa kurejesha mikopo husika.

Dk. Mpango aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma juzi jioni alikuwa anapohitimisha mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha kwa kujibu hoja mbalimbali za wabunge.

Moja ya hoja zilizoibuliwa na wabunge wakati wa mjadala huo, ni kuchelewa kutiwa saini kwa mikataba mbalimbali ikiwamo inayohusisha mikopo ambayo serikali imeomba kwa wadau wa maendeleo.

Akijibu hoja hiyo, Dk. Mipango alisema kuchelewa kutiwa saini kwa mikataba hiyo kumetokana na masharti magumu ambayo wakopeshaji wameweka katika mikataba hiyo.

Alibainisha kuwa miongoni mwa mikataba hiyo inahusisha serikali kukopeshwa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege Zanzibar, Bandari ya Mpinga Nduri na mradi wa upanuzi wa Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam.

"Tunachofanya serikali ni kupitia masharti ya mikataba ili kujiridhisha kama kilichoelezwa kinawiana na fedha ambazo serikali itakopeshwa. Kama tukiona kuna uhalisia, tutatia saini, hakuna asiyetaka kutekeleza miradi hiyo muhimu.

"Lakini Mheshimiwa Spika na waheshimiwa wabunge wenzangu, baadhi ya mikataba ina masharti magumu, siko tayari kuhukumiwa kwa kutia saini mikataba inayotaka kushikiliwa mali za jeshi na migodi yetu pale ambapo serikali ikishindwa kulipa madeni," alisema.

Dk. Mpango pia alisema wameandika barua kwa wizara na taasisi kuzitaka kuzingatia Sheria ya Bajeti pale wanapotaka kutoza kodi na tozo mbalimbali.

Alisema wizara yake imekuwa ikiwataka wadau kuwasilisha kodi na tozo wanazopendekeza ili kuondoa mgongano kwa taasisi kutoza kodi zinazofanana.

Kuhusu ulipaji madeni, alisema serikali inaendelea kutenga fedha kulipa madeni yaliyohakikiwa.

"Madeni yakishahakikiwa yanawasilishwa kwa maofisa masuhuli, hivyo maofisa masuhuli wanatakiwa kuwajulisha wahusika ambao madai yao yamekataliwa ili wafahamu," alisema.

Mtaalamu huyo wa uchumi alisema uhakiki wa madeni ya kuanzia mwaka 2017/18 hadi mwaka huu, umeanza na unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

Vilevile, waziri huyo alisema serikali inaendelea kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa deni la taifa ambalo kila mwaka lazima lifanyiwe uthamini.

"Tunafanya majadiliano na nchi ambazo si mwanachama wa Paris Club kuangalia uwezekano wa kutusamehe madeni yao, lakini pia tunahakikisha mikopo ya ndani inazingatia uwezo wa soko na kukopa bila kupunguza uwezo wa taasisi mbalimbali kukopesha sekta ya ndani.

"Kokopa si dhambi, mradi mikopo ielekezewe kwenye kuzalisha mali na uwezo wa nchi katika kulipa," Dk. Mpango alisema.

Kwenye ukurasa wa 18 wa kitabu cha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Dk. Mpango anabainisha kuwa wizara mwaka huu ilipanga kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu ya kiasi cha Sh. trilioni 2.67 kutoka

INAENDELEA UK. 26

# Mwalimu mbaroni tuhuma kukutwa na bunduki AK47

Na Woinde Shizza, ARUSHA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Naan katika Kata ya Engserosambu, Tarafa ya Loliondo wilayani Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, Solomon Letato Kipuker (30), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kukutwa na bunduki aina AK47.

Jeshi la Polisi limesema kuwa bunduki hiyo pia ilikutwa ikiwa na risasi tano zikiwa kwenye magazine.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Arusha, Johnathan Shana, alisema walifanikiwa kukamata silaha hiyo juzi kutokana na ushuirikiano kati ya Jeshi la Polisi na kikosi kazi cha kupambana na ujangili na uhalifu wa silaha za moto kupitia uwezeshwaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), na kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa katika Kata ya Engserosambu.

Alisema mtuhumiwa huyo pia ni miongoni mwa wafanyabiashara haramu wa uingizaji wa silaha za moto ndani ya nchi. Pia anahusishwa na biashara ya nyara za serikali hasa hasa meno ya tembo, pembe za faru pamoja na kujihusisha na shughuli za ujangili kwa ujumla.

"Mara baada ya kumuhoji alikiri kumiliki silaha hiyo ya kivita kwa kushirikiana na watuhumiwa wengine ambao bado wanatafutwa," alisema na kuongeza:

"Aidha, baada ya kumuhoji alisema silaha hizo pia amekuwa akizikodisha katika mapigano ya kikabila kati ya jamii za wasonjo, watemi na wamasai pamoja na kuzitumia katika matukio mbalimbali ya ujambazi na utekaji wa wawatalii."

Wakati huo huo, Jeshi hilo limekamata bunduki aina ya AK47 ikiwa na risasi moja iliyotelekezwa katika ofisi ya kijiji Mbukeni Kata ya Arashi Tarafa ya Loliondo baada ya kupata taarifa za kiitelijensia.

Pia, Kamanda huyo alisema wanawashikilia majangili sugu wakiwa na nyara za serikali Juni 30 katika kitongoji cha Maji ya Chai Kata ya maji ya chai na tarafa ya Kingori wilayani Arumeru.

Alisema jumla ya watuhumiwa watatu ambao majina yanaifadhiwa, wameojiwa na wamekiri kujihusisha na biashara ya ujangili, huku wakiwa na vipande vinne vya meno ya tembo walivyokuwa wamehifahi kwenye mifuko ya sandarusi.

Kamanda Shana alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu wa madhehebu ya Answari Sunni, Mkoa wa Dodoma, wakiwa kwenye Swala ya Eid El Fitri, iliyoswaliwa viwanja vya Shule ya Central Sekondari, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vitambulisho machinga vyaibua mapya

**Na Waandishi Wetu**

PAMOJA na juhudi kubwa ya uhamasishaji inayofanywa na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa wafanyabiashara wadogo (Machinga) kutumia vitambulisho rasmi vya kuwatambulisha katika biashara zao hizo ili wasibughudhiwe, imebainika kuwa wengi hawana vitambulisho hivyo na hutumia 'feki'.

Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, alibaini hayo jana baada ya kufanya operesheni katika eneo la Kariakoo ya kutathmini utekelezaji wa agizo hilo ambalo lilitolewa na Rais John Magufuli kwa kuhakikisha kila mmachinga anapatiwa kitambulisho hicho lengo likiwa ni kuwasaidia wafanye biashara zao kwa uhuru bila bughudha.

Makonda alisema katika tathmini na operesheni hiyo wamebaini kwamba kati ya wamachinga 10, wanne hawana vitambulisho hivyo.

Jambo jingine ambalo alisema wamelibaini ni udanganyifu wanaofanya wamachinga hao kwamba badala ya kulipia Sh. 20,000 na kupatiwa vitambulisho vyao halali, wanatoa kopi na kutengeneza feki.

Jambo la pili ambalo Makonda alisema wamelibaini ni wamachinga hao kuazimana vitambulisho.

Aidha, wamegundua wamachinga hao kukodishana vitambulisho hivyo kwa Sh.1,000 wenyewe kwa wenyewe ili ukaguzi unapofanyika wanaonekane wanavyo na kuwa salama.

"Katika operesheni hii tumebaini mengi na masikitiko yangu ni kwamba wamachinga wengine wameamua kutokuwa waaminifu badala ya kulipia Sh. 20,000 apate kitambulisho chake halali wameamua kuanza kutoa kopi na kutengeneza vitambulisho feki jambo ambalo haliruhusiwi kisheria," alisema Makonda.

Makonda aliwaagiza wakuu wa wilaya zote katika mkoa huo, kufanya operesheni ya kubaini wamachinga wote ambao wanafanya biashara bila vitambulisho hivyo na kuwachukulia hatua.

"Tumeamua kufanya operesheni hii kwa lengo kuu moja tu kuangalia effectiveness (matokeo) ya vitambulisho vya Rais, ambaye kwa mapenzi yake makubwa aliamua kuwapa wamachinga vitambulisho ambavyo sisi wakuu wa mikoa tulipokea na kusambaza kwa wakuu wa wilaya," alisema Makonda na kuongeza:

"Mkoa wetu ulipewa vitambulisho zaidi ya 175,000, lakini mpaka juzi vilikuwa vimebaki vitambulisho 2,000 kwenda 3,000 na ndiyo maana nilitangaza kuanzia Jumatatu tufanye kazi ya kuangalia, je, ni kweli waliotakiwa kuwa na vitambulisho hivyo wanavyo na wanaofanya biashara wote wana vitambulisho?"

Alisema tayari ameshaelekeza wamachinga wanaofanya mchezo huo kuchukuliwa hatua kali na waliobainika kuwa na vitambulisho feki katika eneo la Kariakoo tayari wameshakamatwa na hatua zinaendelea kuchukuliwa.

"Tumebaini kwamba katika watu 10 ni wanne tu wenye vitambulisho, na hata vichache tulivyokuja navyo leo (jana) hapa Kariakoo vimeisha kabla hata kumaliza mita 200,

INAENDELEA UK. 8

# Washtakiwa kuchapisha maudhui bila kibali cha TCRA

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi nne tofauti ikiwamo tuhuma za kuchapisha maudhui katika mtandao wa Youtube bila kibali kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Washtakiwa hao ni, Charles Kombe (24) mkazi wa Mikocheni, John Chuwa (28), mkazi wa Tabata Barakuda, Amos Warema (27) na Raymond Mkoroka (30).

Katika kesi ya kwanza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando, mshtakiwa Kombe alisomewa mashtaka yake.

Wakili wa Serikali Elizabeth Mkunde alidai kuwa kati ya Agosti Mosi, 2017 mpaka Mei 21, mwaka huu mahali tofauti mshtakiwa Kombe alichapisha katika mtandao wa Youtube kwa jina Charles Kombe, maudhui bila kibali.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo, upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Mshtakiwa yupo nje kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kuwa na wadhamini wawili waliosaini bondi ya Sh. milioni tano kila mmoja.

Katika kesi ya pili, mshtakiwa Chuwa, alisomewa shtaka mbele ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Wakili wa Serikali, Elizabert Mkunde, alidai kuwa katika terehe tofauti kati ya 2018 na Aprili 2019 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alichapisha maudhui kupitia mtandao wa Youtube uitwao Charles Kombe, bila kibali kutoka TCRA.

Mshtakiwa huyo alikiri kutenda kosa hilo na alichiwa kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kujidhamini mwenyewe kwa bondi ya Sh.milioni tano pamoja na mdhamini mmoja aliyesaini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

INAENDELEA UK. 8

# PSSSF sasa kutolipa mafao wasiohakikiwa

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umesema hautalipa mafao kwa mwanachama yeyote ambaye hatahakiki taarifa zake.

Akizungumza hivi karibuni katika mahojiano na chombo kimoja cha habari, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema uhakiki wa wanachama ulianza Januari mwaka huu, ili kuwa na taarifa sahihi kwa wanachama wote.

Alisema wastaafu 124,000 wanatakiwa kuhakikiwa na hadi kufikia Aprili wanachama 113,000 wamehakikiwa na kwamba wapo ambao hawakujitokeza.

"Usipohakikiwa unaondolewa kwenye daftari la kulipwa pensheni ili ujitokeze urudishwe kwenye daftari, kuna wanachama waliokuwa wanalipwa pensheni zaidi ya 10,000 ambao walikosa pensheni, lakini kila anayejitokeza tunamrudisha kwenye mfumo," alisema na kuongeza:

"Changamoto ni kwamba wapo wanaokuja katikati ya mwezi ambako maandalizi ya malipo, hawa ndio wanaolalamika kuwa walihakikiwa, lakini hawapo kwenye daftari la kulipwa pensheni baada ya kuingia kwenye mfumo wanalipwa," alisema.

Alisema mfumo hautemi watu bali unawekewa watu wa kulipwa na kwamba hadi sasa wapo hawajarudishwa kwenye daftari hadi wajitokeze ndipo watalipwa haki zao zote.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, waliojitokeza Aprili na Mei, wataingizwa kwenye daftari na watalipwa malimbikizo na pensheni yao yote.

"Wale ambao hawatajitokeza kabisa wataondolewa kwenye daftari moja kwa moja," alisema Kashimba.

Alisema ulipaji wa mafao unafanyika kwenye mikoa mbalimbali na lengo mwishoni mwa mwezi huu mikoa yote iwe imeunganishwa na kwamba hadi sasa mikoa 11 iliyounganishwa na mfumo inalipa mafao mikoani.

Alisema yapo mambo na taratibu zilizobadilika kutokana na mifuko kuunganishwa kutoka kwenye utaratibu wa awali.

"Tumeunganisha tamaduni nne ili tuwe na zinazofanana kuwahudumia Watanzania, kuna ambao walikuwa na mafao mengi yaliyogawanywa gawanywa na wengine walikuwa na

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
**04/06/2019**

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 05/06/2019 kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCION & INVESTMENT** itapita bila mizigo kutoka KABANGA kuelekea SUMBAWANGA gari hilo lenye namba za usajili

   **T949 BNT /T646 BCJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   **Urefu – mita 20.0**
   **Upana - mita 3.0**
   **Kimo – mita 2.90**

3. Njia itakayotumika **KABANGA hadi SUMBAWANGA kupitia MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115260502

# Bandari ya Mwanza yaongeza mapato kwa 54%

**Na Mary Geofrey,** MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kupitia Bandari ya Mwanza, imeongeza mapato yake yatokanayo na shughuli za kupakia na kupakua shehena kwa wastani wa asilimia 54.6 katika kipindi cha mwaka 2018/19.

Jumla ya Sh. bilioni 1.138 zilikusanywa kuanzia Julai mwaka 2018 hadi Aprili 2019, ikilinganishwa na mwaka 2017/18 walipokusanya Sh. milioni 619.71.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, aliyaeleza hayo jana jijini Mwanza kwa waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya bandari katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais John Magufuli.

"Mapato yatokanayo na shughuli za kupakia na kupakua shehena bandarini yameongezeka kwa wastani wa asilimia 54.6 katika kipindi cha mwaka mmoja kutoka Sh. milioni 619.71 hadi Sh. bilioni 1.134.62," alisema Lwesya.

Alitaja sababu za kuongezeka kwa mapato hayo ni kufunguka kwa njia ya Mwanza hadi Bandari ya Uganda maarufu kama 'Port Bell' ambayo ilikuwa haifanyika kazi kwa zaidi ya miaka 10. Alisema sababu nyingine za kuongezeka mapato ni matumizi ya bei zinazolingana kwenye huduma 'tarrif' tangu mwaka 2018 na kurejea kwa shughuli za usafirishaji wa mizigo katika Bandari ya Musoma.

Lwesya alisema pia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), katika makusanyo ya mapato zinatumika katika bandari kubwa za Kemondo na Mwaloni, Kyamkwikwi, Mwanza Kaskazini na Kusini, Isaka, Mwigobero Bukoba na Mwalo wake na Nansio.

Alisema kurejea kwa wateja ambao walikuwa wameacha kutumia Bandari ya Mwanza Kusini na Musoma na maboresho ya shughuli za usafirishaji katika Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL).

Mbali na kuongezeka kwa mapato alisema, idadi ya meli zinazohudumiwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imekuwa ikipungua kwa wastani wa asilimia 33.4.

Alisema katika mwaka 2013/14 meli zilizohudumiwa zilikuwa 2,682 na ilipungua na kufika meli 530 kwa mwaka 2017/18, lakini mwaka 2018/19 zilianza kuongezeka.

Alitaja sababu za kupungua ni kuwapo kwa ushindani katika njia ya barabara, kuwapo kwa bandari za watu binafsi na kuongezeka kwa safari za ndege za abiria kwenda na kutoka Bukoba.

Alisema wanaendelea na mikakati ya kuendelea na wateja waliopo, kutafuta wapya, kurudisha walioondoka kwenye soko na kuzidisha wateja wakubwa.

## KESI YA KINA MBOWE:

# Shahidi: Sifahamu sababu kifo cha Akwilina Akwilini

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa nne Konstebo wa Polisi, Fikiri Mgeta (28) katika kesi ya uchochezi, amedai kwamba hafahamu kama kifo cha Akwilina Akwilini kilisababishwa na majeraha ya kupigwa risasi.

Shahidi huyo alitoa madai hayo wakati akihojiwa na upande wa utetezi katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe na wenzake nane.

Ushahidi huo unasikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Jopo la Jamhuri liliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Mawakili wa Serikali Jaqline Nyantori, Wankyo Simon na Salimu Msemo.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Prof. Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya, Hekima Mwasipu na Jeremia Mtobesya.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya Wakili Kibatala na shahidi:

**Wakili:** ni kweli Akwilina Akwilini alikuwa katika ya Barabara ya Mkwajuni?

**Shahidi:** Sifahamu.

Wakili: Je, ni sahihi kuwa Akwelina alifariki kwa majeraha ya kupigwa risasi?

**Shahidi:** Hapana, sifahamu.

**Wakili:** Shahidi umetaja majina ya dereva aliyewapeleka wewe Koplo Rahimu Hospitali?

**Shahidi:** Simfahamu.

Wakili: Shahidi kwa mujibu wa sheria ukiumia kuna maelezo kama muathirika unaandika, ninachotaka kufahamu kama uliandika maelezo ya muathirika?

**Shahidi:** Ndiyo, niliandika.

**Wakili:** Uliandika mnamo tarehe ngapi na mwezi gani?

**Shahidi:** Sikumbuki.

**Wakili:** Shahidi, ni ofisa gani wa Polisi aliyeandika maelezo yako wewe kama kuathirika uliyejeruhiwa kwa jiwe?

**Shahidi:**Sikumbuki.

**Wakili**: Maelezo hayo wewe ndiye uliyatamka uliyatoa mahakamani

**Shahidi**:Sikuyatoa

**Wakili:** Ulikumbuka kuzungumzia chochote juu ya wewe kutoa hayo maelezo

**Shahidi**:Sikuzungumzia

**Wakili:** Unafahamu Koplo Rahimu aliruhusiwa lini kama kweli ulilazwa naye

**Shahidi:**Sifahamu alilazwa lini

**Wakili:** Nani alianza kuruhusiwa, yeye au wewe?

**Shahidi:** Siwezi kuongelea

**Hakimu:** Muulize swali

**Wakili:** Ni nani kati ya wewe na Koplo Rahimu alianza kuruhusiwa

**Shahidi:**Sijui

INAENDELEA UK.26



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti wa Bodi wa Taasisi ya Kidini ya Kingdom Leadership Network Tanzania (KLNT), Ibrahim Kaduma, alipomtembelea nyumbani kwake, eneo la Kisasa jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Vipande 10 meno ya tembo vyashikiliwa

**Na George Tarimo,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa kwa kushirikiana na kikosi cha kupambana na ujangili wamekamata meno ya tembo vipande 10 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 vikiwa ndani ya mfuko wa salfeti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alisema tukio hilo lilitokea Kijiji cha Magubike Tarafa ya Kalenga Wilaya ya Iringa, na kuwa wamemkamata mtuhumiwa Habibu Mkenja (47), mkulima wa Magubike kutupa na kukimbia baada ya kuwekewa mtego, lakini baadaye alikamatwa Aprili 28, mwaka huu.

Kadhalika, Juni 1, mwaka huu, majira ya 4:00 usiku katika Kijiji cha Wenda Kata ya Tanangozi jeshi hilo kwa kushirikiana na ofisa wanyamapori wamewakamata watu wawili ambao ni Geofrey Kiswaga (35) na mwenzake Nelson Kiduru (31) ambaye ni dereva bodaboda wakiwa na meno matatu ya tembo ambayo hayajajulikana thamani yake.

Kamanda Bwire alisema meno hayo yalikuwa na uzito wa kilo nane ambayo yalikuwa yamehifadhiwa kwenye mfuko wa salfeti na kuyasafirisha kwa kutumia usafiri wa pikipiki iliyokuwa ikiendeshwa na Nelson wakitokea kijiji cha Nyamihuu-Kidamali kuelekea Wenda kwa ajili ya kufanya biashara.

Katika tukio lingine katika kijiji cha Kilolo kata na Tarafa ya Kasanga Wilaya ya Mufindi, jeshi hilo linamshikilia Jupista Mhinza (30) kwa kosa la kuchoma na kijinga cha moto mwanaye wa miaka sita sehemu za siri.

Alisema tukio hilo lilitokea Mei 27, mwaka huu majira ya usiku, na kuongeza kuwa mtoto huyo ni mwanafunzi wa awali katika Shule ya Msingi Kilolo kutokana na mtoto huyo kuchelewa kurudi nyumbani kutokana na kucheza na wenzake. Bwire alisema mtoto huyo amelazwa katika Hospitali ya Kasanga akiendelea na matibabu, na chanzo cha tukio hilo ni ulevi.

## HABARI KITAIFA



Mshtakiwa John Albert akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, na kusomewa mashtaka ya kuposti picha kwenye mtandao wa Youtube bila kuwa na kibali cha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waonywa kuvua, kulima chanzo cha maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga wameonywa kufanya shughuli za kilimo na uvuvi kwenye chanzo cha maji mbadala cha bwawa la Ning'wa lililopo mjini hapa, ambalo husambaza maji safi na salama kwenye makazi ya watu, ili kutoharibu chanzo hicho kwa kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Imeelezwa kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wananchi kwenda kufanya shughuli za kilimo na uvuvi kwenye chanzo hicho cha maji pamoja na kutupia mifuko ya plastiki, hali ambayo imekuwa ikiharibu chanzo hicho kwa kukichafua, na kusababisha uwapo wa matumizi ya maji machafu ambayo ni hatari kiafya.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Flaviana Kifizi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya siku mazingira duniani leo, na kupiga marufuku shughuli za uvuvi na kilimo kwenye chanzo hicho.

Alisema licha ya chanzo hicho cha maji kuwa mbadala kwa sasa, lakini kinapaswa kutunzwa katika hali ya usafi wa mazingira, ambapo bomba la maji ya Ziwa Victoria linapokuwa likiharibika, hulitumia bwawa hilo kusambaza maji kwenye makazi ya watu, na kuanza kutoka machafu, hivyo kuingia gharama kubwa ya kuyasafisha.

"Natoa tahadhari kwa wananchi ambao wanaendelea kufanya shughuli za kilimo na uvuvi kwenye chanzo cha maji cha bwawa la Ning'wa, waachane na tabia hiyo mara moja," alisema na kuongeza:

"Tutakayemkamata tutamchukulia hatua kali za kisheria za uharibifu wa mazingira," alisema Kifizi. "Pia natoa wito kwa wananchi waachane kabisa na matumizi ya mifuko ya plastiki bali watumie mifuko mbadala ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira vikiwamo na vyanzo vya maji."

Kwa upande wake Ofisa Mahusiano wa SHUWASA, Nsianel Gerald, aliwataka wananchi wawe wanatoa taarifa pale wanapokuwa wakiona uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji, ili wapate kuudhibiti mapema na kuendelea kuwapatia huduma ya majisafi na salama.

# Kampuni za ujenzi barabara, mifereji zategwa viwango

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema haitavumilia kampuni zitakazochelewesha na kufanya kazi chini ya viwango katika mradi wa ujenzi wa barabara na mifereji wenye gharama ya Sh.bilioni 62.4 utakaotekelezwa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika utiliaji saini wa mikataba na kampuni nne za ukandarasi za ndani na nje, Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Chaurembo, alisema miradi hiyo iliyo chini ya mpango wa uboreshaji wa jiji la Dar es Salaam (DMDP) inatakiwa kutekelezwa kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Alisema serikali ya awamu ya tano imejizatiti kuboresha maisha ya watu wa hali ya chini, na miradi hiyo itakapokamilika itarahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi pamoja na kuwaepusha na mafuriko ya mara kwa mara.

"Nataka niwaonye kwamba serikali haitavumilia kampuni ambayo itaonekana kusuasua katika kutekeleza mradi husika, tutamfukuza na ikibidi arudishe pesa zetu ambazo zinatokana na kodi za wananchi," alisema.

Miradi itakayohusika ni ujenzi wa

**INAENDELEA UK.8**

# Watoto wenye uhitaji waomba kusaidiwa

**Na Romana Mallya**

WATOTO wa Kituo cha malezi ya watoto yatima Chakuwama kilichopo Sinza, jijini Dar es Salaam, wameiomba jamii yenye uwezo kujitoa mara kwa mara kuwasaidia ili kuvipunguzia mzigo vituo vilivyojitoa kuwahifadhi.

Mtoto Mwanahamis Havivu, aliyasema hayo jana wakati wakipokea msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya Sikukuu ya Idd El Fitr kutoka kwa mmiliki wa First Super Marker, Devotha David, ambaye naye ni yatima.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya watoto wenzake wapatao 64 waliopo kituoni hapo, Mwanahamis alisema wanapopokea misaada kutoka kwa makundi mbalimbali kwenye jamii yanawafanya wajione bado wanawazazi.

Kituo cha Chakuwama kina watoto wenye umri wa kuanzia miaka mitatu hadi 19 ambao wapo wanaosoma ngazi mbalimbali za elimu.

"Endapo jamii itaendelea kuwa na mwamko kama wa dada Devotha utasaidia kupunguza mzigo vituo ambavyo vimebeba jukumu la kutuhifadhi sisi tusio na wazazi," alisema.

Devotha alisema mara kwa mara amekuwa akijumuika na watoto kwa sababu na yeye ni yatima na kwamba huwa anatoa misaada ya chakula na vifaa vya shule ili kusaidia nao wajione ni sehemu ya jamii.

"Ninaiomba jamii wawe na moyo wa huruma na kutoa siyo utajiri, ukitoa Mungu atakuzidishia, jamii tujitahidi kuwakumbuka wale ambao hawana uwezo mtu mwingine anaona ni bora akatoa kwa starehe kuliko kwa hawa wasiokuwa na kitu kabisa, tuwafikirie hawa," alisema.

Pia aliiomba jamii inapofikiria kutoa, itoe vitu wanavyovipenda na siyo ambavyo hawavipendi.

"Mpe mtu msaada wa kitu ambacho hata wewe mwenyewe unakiona kinakufaa hiyo ndiyo maana ya kutoa ni moyo, usitoe usichokihitaji kimechoka ndo upeleke kwa mwingine hapana, hawa ni binadamu kwa wengine na wanatamani kama wangekuwa na wazazi wao," alisema.

**INAENDELEA UK.8**




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maradhi na uchafu huu vimeshindikana?

**MATATIZO** ya uhaba wa mifumo na miundombinu ya kusafirisha majitaka, madampo ya kutupa taka pia tabia za wananchi kuendelea kuishi kwenye mazingira machafu kumesababisha Dar es Salaam kuwa na magonjwa ya fedheha kama kipindupindu.

Mbali na kipindupindu ambacho kinasababishwa na kula kinyesi kibichi, mji umejaa maradhi kama dengue na magonjwa ya kuharisha yanayochochewa na tabia za kula uchafu unaoweza kusambazwa na taka za vyooni.

Uchafu huo unasababishwa na kutapisha vyoo unaofanywa na wakazi wa jiji msimu wa mvua.

Taarifa za kulipuka kipindupindu Dar zilianza tangu mwezi uliopita, lakini hadi sasa mamalishe wanaendelea kupika na kuhudumia wateja kwenye maeneo yenye mitaro inayopitisha kinyesi kibichi.

Mbali na mamalishe kuchangia kueneza magonjwa Dar, mienendo iliyozoeleka wala isiyokemewa ya kufungua vyoo wakati wa mvua na kuvitapisha ni chanzo cha kusambaza kinyesi mji mzima hali inayosababisha kila mahali kujaa uchafu wa vyooni. Ni dhahiri kuwa Dar es Salaam inasifika kwa uchafu ikilinganishwa na miji kama Moshi, Arusha na Iringa, tatizo ni kwamba hakuna miundombinu wala mipango ya uzoaji taka inayoeleweka na wakazi wake wana hulka za uchafu.

Mambo hayo na mengine mengi yanachangia Dar kuwa chafu na yenye magonjwa kama dengue, malaria, kuhara na kipindupindu kama hali ilivyo leo.

Wakati hayo yanatokea kuna maofisa afya na zipo sheria ndogondogo za jiji na za manispaa ambazo hazitumiki ipasavyo ili kulinda afya za walaji kwa kuhakikisha biashara za vyakula kuanzia migahawa, hadi vile vinavyopikwa ovyo mitaani vinadhibitiwa.

Aidha kuna sharia za usafiri wa mazingira ambazo kama zingetumiwa zingedhibiti kuzibua vyoo na kuacha kinyesi kusambaa mitaani kila wakati wa msimu wa mvua.

Huu si wakati wa kulaumiana lakini ni muda wa kukumbushana kuwa ni vyema kupanga upya na kuiweka Dar kwenye mazingira safi na salama yasiyo na magonjwa kama yanavyotokea sasa. Maofisa afya na wanamgambo wa jiji watumie sheria ndogondogo na mamlaka waliyo nayo kudhibiti maradhi hasa dengue na kipindupindu. Kwa vile kuna Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ni wakati wa kuitumia kudhibiti kutapisha vyoo, mambo yanayofanywa wakati wa misimu ya mvua ambayo kiasi miaka inavyokwenda yanazidi kuzoelekea na kukubalika.

Pamoja na maofisa wa afya wa kata na wilaya , tunatarajia pia kuona maofisa wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Mamlaka ya Chakula Dawa (TFDA), wakisimamia pamoja usafi wa jiji, wa vyakula na mazingira kwani tatizo la kipindupindu linahitaji wadau mtambuka kulishughulikia.


Tunaamini kuwa NEMC inalielewa kikamilifu suala la ujenzi unaoziba mitaro na kusababisha mafuriko kuharibu mazingira nyakati za mvua ni vyema ikalivalia njuga ili kuondoa magonjwa. Tunatarajia kuona kamati za afya za jiji zikishirikiana na NEMC, TFDA na wadau wengine wa mazingira kuzungumzia na kusimamia uzibuaji wa mitaro ya maji taka na ikibidi kuondoa majengo yaliyojengwa juu ya miundombinu hiyo.

Dar es Salaam pamoja na kuwapo na mipango ya kuondoa maji taka, kuwapa wananchi maji salama na pia kuweka mikakati ya kusafisha maneno yamekuwa mengi kuliko utekelezaji.

Tunaamini kuwa wadau wakishirikiana Dar itakuwa salama tena isiyo na magonjwa kila mmoja akitimiza wajibu wake. Ikumbukwe taifa linahitaji kuwekeza kwenye maendeleo endelevu na si kutibu maradhi yanayoepukika kama kipindupindu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Serikali iendeshe operesheni usafi wa mitaro nchi nzima

Na Raphael Kibiriti

**KUNA** mengi ambayo serikali ya awamu ya tano inazidi kujijengea uhalali kwenye suala zima la utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazokabili wananchi katika suala zima la kujenga ustawi na maendeleo ya jamii ya Kitanzania.

Ninaweza kuzungumzia maeneo mengi kuanzia kwenye suala zima la kupambana dhidi ya rushwa na ufisadi, watumishi hewa, uhalifu hususani unyang'anyi, ujambazi na ujangili.

Lakini hata katika suala la kuboresha hali ya miundombinu ya barabara, vituo vya afya, ukarabati na ujenzi wa madarasa, maabara, maktaba, utoaji wa elimu bure kwa kutaja baadhi ya mambo.

Muungwana anaona haya yote ni katika ile dhima ya kutekeleza majukumu na wajibu wa serikali hii kwa wananchi wake. Na hiyo ni kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambayo rais na timu yake, waliinadi wakati wa kampeni za kutafuta ridhaa ya kuongoza taifa hili.

Kama nilivyosema hapo juu kuna mengi ambayo yametekelezwa na serikali hii, lakini kwa makusudi maalumu Muungwana amevutiwa zaidi kuzungumzia operesheni mbili ambazo kwa mtazamo wake zimeiongezea alama serikali ya awamu ya tano.

Zimeiongezea alama mbele ya macho ya wananchi na hasa wenye mapenzi mema kwa ustawi wa taifa na raia wake, lakini pia hata katika suala la usafi wa mazingira na uhai wa viumbe vinavyoyategemea mazingira hayo.

Operesheni ya kwanza anayoirejea Muungwana ni ile iliyochukuliwa na serikali mwaka 2017 inayofahamika hadi leo kama operesheni 'piga marufuku viroba' vilivyokuwa maarufu katika maeneo mbalimbali nchini.

Kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, serikali ilipiga marufuku uzalishaji, uuzaji, uingizaji na matumizi ya pombe inayofungwa kwenye pakiti za plastiki kwa jina la viroba kuanzia Machi Mosi, mwaka 2017.

Aidha, ikaweka wazi kwamba ambaye angebainika kuvitumia angewajibishwa kwa kulipa faini, kufungwa jela au vyote kwa pamoja.

Ilichukua hatua hiyo kwa nia nzuri ya kulinda afya ya Watanzania, hususani vijana ambao ndiyo nguvukazi ya taifa hili wanaotengeneza sehemu kubwa ya idadi ya Watanzania takribani milioni 55 kwa hivi sasa.

Kwa wanaokumbuka hali ilipokuwa imefikia wakati huo kiasi kwamba viroba vilienea kila kona hata kwa watoto wa shule za msingi ambao nao walianza kuvitumia kwa sababu ya urahisi wake wa kuvibeba, kwani iliwezekana hata kuviweka mfukoni na kutembea navyo.

Madhara ya viroba yalikuwa mabaya sana kwa afya na maendeleo ya Watanzania kwani mbali na ajali za barabarani zilizotokana na uendeshaji wa kizembe hasa kwa madereva wa bodaboda, pia yaliharibu mazingira kutokana na kuzagaa kwa vifungashio hivyo.

Operesheni ya pili ambayo imeendelea kuipa alama serikali hii ni iliyochukuliwa na serikali hivi karibuni ambayo imepiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usafirishaji nje ya nchi, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko aina ya plastiki maarufu kama 'Rambo' iliyokuwa ikitumika kubebea bidhaa kuanzia Juni Mosi.

Katika operesheni zote mbili, serikali ilitoa maelekezo na hatua madhubuti itakazochukua kwa wote ambao wangekaidi maelekezo yake.

Kama nilivyosema hapo juu, kufanikiwa kwa operesheni hizi kunaonyesha kwamba serikali hii inapoelekeza marufuku dhidi ya dosari fulani iliyo na madhara kwa watu wake, wananchi wanaelewa na kutekeleza.

Wanafanya hivyo kwa sababu wanajua haina simile katika kuchukua hatua.

Wakati Muungwana akipongeza umadhubuti wa serikali katika kusimamia masuala yenye tija kwa wananchi, anatoa wito operesheni kama hiyo sasa ielekezwe katika usafi wa mitaro kwenye majiji na miji, hasa jiji la Dar es Salaam, lenye hali mbaya katika eneo hilo.

Muungwana ana imani kwamba serikali ikielekeza nguvu kwenye eneo hili la mitaro katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, suala la mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu na homa ya Dengue iliyopo sasa yatakwisha.

## MJADALA/BARUA

# Wavuta sigara wafuate sheria

**Mhariri pole na majukumu ya kila siku.**

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyo nayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii kimsingi inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*


*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

*Bahati mbaya zaidi hata pale wananchi wenzetu hawa wavutaji wanapokanywa ama kunasibiwa waache kuwakera wenzao, baadhi yao huziba masikio na wengine hutoa majibu yasiyofaa.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

**Joseph Zengo,
Malampaka, Simiyu**

# Bajeti ya serikali 2020 imulike vifo vya uzazi




**Na Gaudensia Mngumi**

MWAKA wa fedha wa serikali unaanza wiki chache kuanzia sasa itakapofika Julai mosi, 2019. Wakati Watanzania wakisubiri kusomwa bajeti ya serikali ya mwaka 2019/2020, taifa linashuhudia mafanikio mengi kama kutoa elimu msingi bure kwa wote.

Mengine ni ujenzi wa miundombinu ya kisasa na maboresho makubwa yanayofanywa katika sekta ya ukusanyaji mapato ya serikali, kudhibiti ufisadi, wizi wa mali ya umma na kukosa uadilifu.

Wakati bajeti inatarajiwa kusomwa wiki moja kuanzia sasa bila shaka Tanzania inaweza kujigamba kuwa ni moja ya nchi yenye mafanikio makubwa kwenye kuwapatia wananchi wake elimu msingi, kuboresha miundombinu na kuongeza nidhamu na uwajibikaji serikalini.

Aidha, taifa limefanya jitihada nyingi kuboresha huduma za kijamii lakini moja ambalo linakera wengi ni vifo vya wanawake na watoto.

Ndiyo maana kwa namna ya kipekee serikali na wadau wengine mwaka wa fedha mpya unapoanza na bajeti ikitarajiwa kufikishwa bungeni, kuna haja ya kutupia jicho kwenye eneo la kuwaokoa wajawazito ambao wanapoteza maisha kila siku kwenye uzazi.

Takwimu za Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya Tanzania (TDHS) za 2018, zinaonyesha kuwa idadi ya vifo vya wazazi imeongezeka na kufikia wanawake 556 kwa kila vizazi hai 100,000.

Hii si habari njema hata kidogo. Pamoja na kwamba juhudi zimefanywa kwenye kuboresha elimu msingi, kupunguza pengo la wasichana na wavulana wanaoandikishwa shule za msingi na vyuoni na hata kupunguza maradhi ya VVU na Ukimwi, kuendelea kuwapo vifo hivyo kunasikitisha.

Bajeti ya serikali ni vyema ikaja na mikakati ya kusaidia kupunguza vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi. Kuna jambo ambalo Tanzania haijalizungumzia ambalo linachangia vifo hivyo, ni wakati wa kuliibua sasa.

Mathalani, taarifa za hivi karibuni kuwa mjamzito alijifungua kwa kujifanyia operesheni mwenyewe nyumbani akijikata na wembe inashangaza mno.

Mama huyo na mwanawe ambao wote ni wazima ni mkazi wa mkoa wa Rukwa anayeelezwa kuwa alijichana na wembe na kukata mfuko wa uzazi hadi alipomtoa mtoto.

Jambo hilo ni changamoto kubwa kwa Wizara ya Afya kuwa ina kazi kubwa ya kuwafikia wanawake ambao ni wazazi wa sasa na wajawazito watarajiwa wengi wao wakiishi vijijini.

Japo serikali inajitahidi kufikisha huduma bora mijini na vijijini, kitendo cha mwanamke huyo kutoroka hospitalini kinatoa picha kuwa huenda kuna walakini kwenye utendaji wa vituo vya afya, si hapo alipofikia na kupimwa bali hata maeneo mengine.

Maswali mengi yanajitokeza ilikuwaje mjamzito akaamua kutoroka hospitalini na kurudi nyumbani?

Ni vipi mama huyu aliamua kujifungulia nyumbani licha ya elimu kutolewa kila wakati kuwa wanawake wajifungulie kwenye vituo vya afya?

Japo kuna changamoto kubwa ya kupunguza vifo hivyo ni vyema kuwe na utaratibu wa kitongoji, kijiji, na mitaa kufuatilia taarifa za kinamama wajawazito ili waweze kufikiwa na kuhudumiwa ipasavyo.

Mathalani, vijiji viwe na wakunga na wauguzi ambao jukumu lao ni kushughulika na wajawazito kuhakikisha kuwa taarifa zao za kiafya zinafahamika.

Wenye matatizo waunganishwe na wataalamu hasa madaktari bingwa wa tiba za wanawake na watoto na pia wapatiwe huduma na ushauri iwapo wana maradhi yanayotishia afya zao na za watoto.

Tukio la Katavi linaonyesha kuwa kuna haja ya kuongeza huduma za afya kwa wajawazito hasa vijijini, ili kuokoa maisha yao kwa kuwa huenda vifo vingi havifahamiki na haviripotiwi kutokana na sababu mbalimbali ambazo si rahisi kufahamika.

Pamoja na kuongeza jitihada za kuwafikia wajawazito, kuna haja ya kufanya tafiti zaidi kujua chanzo cha vifo vya wanawake wajawazito na wazazi, ili serikali ijipange zaidi na iwe na mikakati ya namna ya kuwahudumia.

Pamoja na kufahamu sababu za vifo kama ukosefu wa huduma za kibingwa, upungufu wa damu, malaria, VVU na Ukimwi, utoaji mimba usio salama na kujifungulia nyumbani utafiti ni muhimu ili kuujua ukweli na undani zaidi wa tatizo hilo.

Maelezo kama upungufu wa huduma, ukosefu wa wataalamu, usafiri na hasa uhaba wa magari ya wagonjwa, umbali wa kufikia huduma za afya hayatoshi, kuna haja ya kutafiti zaidi ili kuujua ukweli na changamoto nyingi zilizojificha vijijini.

Ni vyema kuanzisha utaratibu wa kutaja mikoa inayoongoza kwa vifo vya wanawake wajawazito na wazazi kila mwezi, kwa kuweka bayana idadi ya wanawake kwani kutahamasisha mabadiliko katika jitihada za kuwalinda mama na mtoto aliye tumboni.

Ikumbukwe maendeleo endelevu hayapimwi kwa kuondoa umaskini pekee, bali kuangalia afya za mama na mtoto pamoja na kupunguza vifo vya wanawake vinavyohusiana na uzazi vilevile.

**KABWELA NA FADHIL MOHAMMED**




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Vitambulisho machinga vyaibua mapya

INATOKA UK. 3

tafsiri yake ni kwamba wamachinga wengi waliopo katika Jiji la Dar es Salaam hawana vitambulisho," alisema Makonda.

Pia Makonda alisema wiki hii atapeleka maombi kwa Rais Magufuli ili mkoa huo uongezewe vitambulisho vingine ili angalau mkoa huo umefikishe wamachinga 200,000 wenye vitambulisho hivyo.

"Wamachinga hawana sababu yoyote ya kufoji, kukodi, kununua kitambulisho kwa bei ya zaidi ya Sh. 20,000, wala kujificha, wanatakiwa kutii sheria bila shuruti, ukifanya biashara kwa kitambulisho chako utaheshimika na utafanya biashara yako kwa uhuru, lakini kwa wale ambao wanaendelea kufanya ujanja ujanja, msako utakaofanywa na wakuu wa wilaya, utahakikisha unawabaini na kuwachukulia hatua, tusitafutiane ubaya," alisema Makonda.

Alitoa wito kwa wananchi na watendaji wote wa serikali kutowaacha bali wawaripoti wamachinga ambao wanawabaini kufanya biashara bila kitambulisho hicho.

**WABUNGE WAJA JUU**

Jijini Dodoma, serikali imelazimika kwa mara nyingine kutoa ufafanuzi bungeni kuhusu utaratibu wa ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo baada ya baadhi ya wabunge kuulalamikia.

Wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Sumve, Richard Ndassa (CCM), alisimama bungeni juzi jioni na kuitaka serikali itoe kauli kuhusu utaratibu wa ugawaji wa vitambulisho.

Mbunge huyo alisema kuwa baadhi ya maofisa wa serikali wamekuwa wakinyanyasa wananchi mitaani kwa kutokuwa na vitambulisho hivyo.

Ndassa alisema amepata taarifa za fundi ujenzi kukamatwa akiwa anafanya shughuli zake za ujenzi kisa hana kitambulisho cha mjasiriamali.

Kutokana na hoja hiyo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali (Tamisemi), Mwita Waitara, alilazimika kutoa tena kauli ya serikali kuhusu suala hilo, akirejea kauli ya serikali iliyotolewa bungeni Ijumaa iliyopita.

Alisema serikali imeandaa mwongozo wa utaratibu wa ugawaji wa vitambulisho hivyo na utagawiwa kwa maofisa wa serikali wanaohusika pamoja na wabunge.

Waitara alisema watendaji wote wa serikali wanaohusika na usimamizi wa ugawaji wa vitambulisho hivyo, wanapaswa kuzingatia mwongozo uliotolewa na serikali.

Baada ya maelezo hayo ya Waitara, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao cha bunge, alihoji: "Kama mama muuza vitumbua analazimika kuwa na kitambulisho hicho, kwa nini huyu fundi ujenzi asiwe nacho? Na ni Sh. 20,000 tu, si Sh. milioni 20."

Awali, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wakati akihitimisha mjadala huo kwa kujibu hoja mbalimbali za wabunge, alisema vitambulisho hivyo vinatolewa na serikali kwa mujibu wa sheria.

"Malipo ya vitambulisho yapo kisheria na yanaratibiwa kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ambayo ilimpa mamlaka Kamishna Mkuu wa TRA (Mamlaka ya Mapato), kuwatambua wafanyabiashara wadogo na watoa huduma na wengine ambao mauzo ghafi yao hayazidi Sh. milioni nne (kwa mwaka).

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya, DAR na Sanula Athanas, DODOMA.**

# PSSSF sasa kutolipa mafao

INATOKA UK. 3

kidogo, lakini kwa sasa kila mwanachama atalipwa kwa mujibu wa utaratibu," alisema Kashimba.

Alisema katika kuunganisha mifuko minne kuna changamoto ya mazoea au tamaduni ya kazi kwa kila mfuko, na sasa wako katika mafunzo ya kubadili matakwa ya utendaji kazi yaliyozoeleka na kuwa na utaratibu mmoja.

Alisema kazi kubwa iliyofanyika toka mifuko iunganishwe Agosti mwaka jana, kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya jamii wameunganisha mifuko minne.

Alisema PSSSF iliunganisha mifumo yote ya mifuko ya GEPF, LAF, PSPF na PPF na kuhamisha taarifa zote kutoka kwenye mifumo iliyokuwapo na taarifa kuwa pamoja.

"Mifumo iliunganishwa kabla ya zoezi ya kuunganisha mifuko, tumejenga mifumo madhubuti ambayo takwimu na taarifa zote za wanachama tunazo, tutaendelea kusafisha kumbukumbu kadiri ya nafasi na tunavyopokea taarifa na kumbukumbu za wanachama," alibainisha.

Alisema ni vyema waajiri wakapeleka michango ya wanachama kwa wakati kwa kuwa lina madhara kwenye malipo ya pensheni, na kumbukumbu za wanachama kuwapo ili kurahisisha ulipaji.

"Kwenye kulipa mafao umri wa kisheria ni muhimu, muda wa kuchangia, na mishahara ya mwisho mizuri ifahamike...kisheria mstaafu analipwa baada ya miezi miwili baada ya kuwasilisha madai yake na mwezi huo huo ataanza kulipwa pensheni ya kila mwezi," alisema.

Alisema PSSSF imesimamia ulipaji wa mafao kwa waliosubiri kwa muda mrefu na kwamba zaidi ya wastaafu 10,000, na kwamba zimelipwa zaidi ya Sh. trilioni moja, na kwa sasa wanashughulikia mrundikano wa madai ya wanachama.

# Kampuni za ujenzi

INATOKA UK. 5

barabara, mifereji ya maji ya mvua na masoko ya kisasa katika kata za Mtoni, Mbagala na Charambe. Pia ununuzi wa magari 20 na makontena ya 64 kuzolea uchafu katika halmashauri tatu.

"Miradi hiyo inatakiwa kukamilika ndani ya miezi 15, ukifika muda huo hakutakuwapo na sababu zozote za kuchelewesha kwa sababu hali ya hewa ni nzuri na pesa serikali imezitoa kwa wakati," alisisitiza.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Lusibilo Mwakabibi, alisema halmashauri yake itatoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa lengo la kulifanya eneo hilo kuwa la kisasa na linalovutia.

Alisema tayari miradi mingine iliyo chini ya DMDP yenye thamani ya Sh. bilioni 147.7 imekamilika na baadhi serikali imekabidhiwa rasmi.

## Washtakiwa kuchapisha maudhui

INATOKA UK. 3

Kesi iliahirishwa hadi Juni 7, mwaka huu, mshtakiwa atakaposomwewa hoja za awali.

Kesi ya tatu, mshtakiwa Warema ilidaiwa, alitenda kosa hilo kati ya Novemba 2018 hadi Mei 17, mwaka huu katika maeneo tofauti katika jijini Dar es Salaam.

Mshtakiwa huyo alisomewa shtaka hilo mbele ya Hakimu Mtega na kusomewa shtaka na Wakili wa Serikali, Candid Nasua.

Ilidaiwa kuwa, alisambaza maudhui hayo kupitia mtandao wa Youtube uitwao Pro Media Tanzania bila kuwa na kibali kutoka TCRA.

Mshtakiwa huyo alikana shitaka hilo na aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kujidhamini mwenyewe na kuwa na mdhamini mmoja aliyesaini bondi ya Sh.milioni tatu.

Kesi iliahirishwa hadi Julai 4, mwaka huu na upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Kesi ya nne Mkoroka alisomewa shtaka na wakili wa serikali, Elia Athanas, mbele ya Hakimu Mkazi Rwezile.

Ilidaiwa alitenda kosa hilo katika tarehe tofauti jijini Dar es Salaam na alikana shitaka.

Mshtakiwa huyo yupo nje kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kuwa na mdhamini mmoja na kujidhamini mwenyewe kwa kusaini

## Watoto wenye uhitaji

INATOKA UK. 5

Katibu Mtendaji wa kituo hicho, Hassan Khamis, alisema wanapokea watoto waliogawanyika kwenye makundi matano ambayo ni wasiyo na wazazi, wenye mzazi mmoja, waliotelekezwa, wenye migogoro ya kifamilia na mashauri yapo kwenye vyombo vya sheria na kundi la mwisho ni waliofanyiwa ukatili wa kijinsia.

"Hawa watoto wapo ambao huletwa hapa na ustawi wa jamii kutokana na mashauri mbalimbali yaliyopo kwenye vyombo vya sheria na kukosa usimamizi. Tunakaa na watoto hawa na wanapomaliza kidato cha nne wapo wanaounganishwa na familia kama zipo na wengine wasio na familia tunawatafutia makazi mahali pengine," alisema.

Kuhusu changamoto, Khamis alisema kutokana na wao hupokea wenye umri tofauti wapo ambao wanahitaji uangalizi zaidi hasa wa malezi kwa sababu kila mmoja anakwenda hapo akiwa na tabia yake.




HABARI KITAIFA

# JPM apongeza Watanzania kuacha mifuko ya plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewapongeza Watanzania kwa kuitikia wito wa serikali wa kuacha kutumia mifuko ya plastiki ambayo ina madhara makubwa katika mazingira na viumbe hai wakiwamo binadamu.

Rais Magufuli alitoa pongezi hizo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko la samaki la Feri jijini Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza sokoni hapo na kujionea wafanyabiashara na wanunuzi wa samaki wakitumia mifuko mbadala.

Rais Magufuli alimpongeza Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, January Makamba, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wote ambao wamesimamia utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa tangu mwaka 2016 kuhusu kuondoa matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, Rais Magufuli aliwataka wafanyabiashara kutotumia mwanya huo kuuza mifuko na vifungashio mbadala kwa bei kubwa na badala yake amewataka pamoja na wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kutengeneza mifuko na vifungashio kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini.

Rais Magufuli ametoa wito kwa wananchi kujenga utamaduni wa kuwa na vifaa vya kubebea bidhaa wanazozinunua madukani na masokoni ili kuepuka gharama kununua vifungashio ama mifuko mbadala.

Aliziagiza mamlaka zinazohusika, kuhamasisha utengenezaji wa mifuko na vifungashio mbadala nchini ili kuongeza ajira katika viwanda vya kutengenezea bidhaa hizo badala ya kuacha wafanyabiashara wakigeuza nchi kuwa mahali pakuingiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Akiwa katika soko hilo la Feri, alinunua samaki kutoka kwa wafanyabiashara wadogo wanaotumia vitambulisho vya wajasiriamali na kuwapongeza kwa juhudi zao za kujitafutia kipato halali.

Aliiagiza Manispaa ya Kinondoni kupunguza tozo ya pango kwa wapaa samaki kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 500 kwa siku na ameitaka manispaa hiyo kutenga Sh. milioni 10 kutoka kwenye makusanyo ya soko hilo kujenga jengo jingine la wafanyabiashara wasiouza samaki kama vile mamalishe, babalishe na wauza bidhaa zingine ambao hawanufaiki na jengo la wauza samaki ambalo mwaka jana alichangia Sh. milioni 20.

Ameiagiza Manispaa ya Ilala na menejimenti ya soko la Feri kuweka utaratibu wa kuwapokea wafanyabiashara wanaoingiza samaki sokoni hapo kwa muda wote wa saa 24, kuweka umeme na maji katika jengo mojawapo la wafanyabiashara wa samaki ndani ya siku 5 na kuingiza umeme katika jengo la huduma ya Msalaba Mwekundu lililopo sokoni hapo.

Wafanyabiashara wa soko la Feri walimshukuru Rais Magufuli kwa jinsi anavyowapigania Watanzania wanyonge wakiwamo wafanyabiashara wadogo na wamemhakikishia kuwa watatekeleza maagizo yake ya kutotumia mifuko ya plastiki kama inavyoelekezwa katika sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake.



Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari St. Anne Marie Academy, ambaye ni Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo, waliokwenda kutembelea bungeni jijini Dodoma jana, baada ya kupata daraja la kwanza na la pili kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka 2018. Kulia ni Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakimbizi waishio Dar wakumbukwa

**Na Frank Monyo**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Time To Help imetoa zawadi za vitu mbalimbali ikiwamo vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya Sikukuu ya Idi El Haji kwa familia za wakimbizi 250 wanaoishi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Taasisi hiyo, Ibrahimu Ibrahimu, alisema wameamua kutoa msaada kwa wakimbizi hao ili nao waweze kushiriki katika sikukuu hiyo na wasijihisi wapweke kwa kuwa ni wakimbizi na wapo katika nchi nyingine. Alisema taasisi hiyo mara kwa mara imekuwa ikijishughulisha na kusaidia jamii zenye uhitaji kwa kutoa misaada ya kibinadamu ikiwamo afya, elimu, kuchimba visima vya maji, kujenga shule, hospitali, na mengineyo.

"Sisi kama Time To Help huu ni utaratibu wetu wa kila siku kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali kwa kutoa misaada ya kibinadamu, na leo tumewakumbuka ndugu zetu wakimbizi ambao wanaishi hapa Dar es Salaam kwa kuwaletea zawadi ya vyakula ili washiriki sikukuu kama watu wengine," alisema Ibrahim. Naye Ofisa Mipango wa taasisi isiyo ya kiserikali inayohudumia wakimbizi Dar es Salam Relief to Development Society (REDESO), Simon Ndoika, alisema wakimbizi wanaofika katika taasisi yao ni lazima wapitie Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) na kuletwa Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudumiwa.

"Kwanza ifahamike kuwa sisi sio wasemaji wa UNHCR, ila tunafanya kazi kwa karibu sana katika kuhudumia na kutoa misaada mbalimbali kwa wakimbizi na sisi hapa hatupokei wakimbizi moja kwa moja, isipokuwa kutoka kwa washirika wetu na UNHCR," alisema Ndoika. Aliongeza kuwa REDESO inafanya shughuli za kutoa misaada kwa jamii pamoja na kuhudumia wakimbizi 250 kutoka Burundi, Rwanda, Yemen na Sudan ambao kati yao wapo ambao wamekuja kwa ajili ya matibabu, wengine wakisubiri kurudi nchini kwao pamoja na wakimbizi wa kudumu.

Alifafanua kuwa wakimbizi ambao wapo chini ya REDESO wanaishi kwenye nyumba maalum." Hapa sisi hatuna kambi kama zile za Nduta au Kibondo, lakini huko kote tunafanya kazi kwa karibu na kambi hizo chini ya UNHCR," alisema na kuongeza:

"Tunawashukuru Time To Help kwa msaada huu kwa kuwa taasisi yetu inakumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo chakula, mavazi na suala la afya kwani inafahamika wakimbizi hawa hawaruhusiwi kufanya kazi," alisema Ndoika.

# Mkaa magunia 200 magendo yanaswa

**Na Robert Temaliilwa, BAGAMOYO**

WAKALA wa Huduma za Misitu (TFS) Wilaya ya Bagamoyo wamekamata mkaa magunia zaidi ya 200 yaliyokuwa yanapitishwa kwa njia za magendo.

Mkuu wa doria wa TFS Wilaya ya Bagamoyo, Yusuf Haruna, alisema jana kuwa walifanikiwa kukamata mkaa huo kufuatia taarifa za wasamaria wema.

Haruna alisema mkaa huo ulipakiwa kwenye jahazi na kufichwa kwenye mkondo wa Bahari ya Hindi unaounganishwa na Mto Ruvu wakati wakisubiri kuusafirisha kwenda Zanzibar.

Aliongeza kuwa mara baada ya kupata taarifa hizo kikosi cha doria kilifika eneo la tukio ambapo kilikuta jahazi hilo likiwa na mzigo huo, huku mmiliki wa mkaa huo akiwa amekimbia.

Haruna alisema utoroshaji wa mazao ya misitu ni makosa kwa mujibu wa sheria, hivyo mzigo unaokamatwa unataifishwa kwa mujibu wa sheria huku chombo kilichobeba hupigwa faini.

Akizungumzia utoroshaji wa mazao ya misitu katika Wilaya ya Bagamoyo, alisema bado kuna hali ya utoroshaji wa mazao ya misitu, lakini kikosi chake kimejipanga kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ikiongozwa na mwenyekiti wake mkuu wa wilaya hiyo wanadhibiti mianya yote inayotumika.

Meneja Msaidizi wa TFS Kanda Maalum ya Saadan Wilaya ya Bagamoyo, Hadija Msuya, alitoa wito kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu katika wilayani hiyo kufuata sheria za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu.

# Vikoba kidijitali fursa wanawake

Na Mwandishi Wetu

SHUGHULI za kuweka akiba na mikopo zimetajwa ni fursa kwa wanawake kupata kipato zaidi na kuingia katika mifumo rasmi ya kifedha.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na InterMedia's Financial Inclusion Insights (FII), ndani ya mwaka 2018 kuna ongezeko la asilimia 60 ya wanawake katika mfumo wa kuweka fedha kwa njia ya simu "mobile money", kutoka asilimia 50 iliyorekodiwa mwaka 2017.

Mwaka 2002, mfumo wa kuweka akiba na mikopo kwa vikundi uitwao "Vikoba" ulizinduliwa. Mfumo huo umekuwa chachu ya uanzishwaji wa vikundi vingine vya namna hiyo katika nyanja mbalimbali za jamii mpaka vijijini.

Uwapo wa vikundi hivi nchini inaelezwa kwamba vimesaidia kwa kiasi kikubwa na kuwezesha watu wengi hasa wale wa kipato cha chini na kile cha kati kujiinua kiuchumi na hivyo kumudu kuendesha maisha katika hali ya unafuu.

Inakadiriwa kuwa asilimia 16 ya Watanzania (zaidi ya watu milioni 4.4), wengi wao wakiwa wanawake, ni wanachama wa vikundi zaidi ya 50,000 vya kuweka akiba na mikopo (VIKOBA)
ambao huhifadhi akiba zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa mwaka.

FII inasema vikundi hivi vimewawezesha wanawake hao ambao ndiyo wamekuwa na mwitikio mkubwa wa kujiunga, kupata mwamko wa kushiriki katika kuinua uchumi wa familia na pia wameweza kumiliki mali tofauti na ilivyokuwa awali.

Inaongeza kuwa vikoba vimekuwa vyanzo vya mitaji kwa wanawake, ambayo mpaka sasa wanaweza kufanya biashara katika hali ya kujiamini. Wanachama wengine ambao walikuwa wakifanya biashara ndogo ndogo kama vile maandazi, vitumbua wameziboresha biashara zao kuwa migahawa ya kisasa ambayo imezidi kuwavutia wateja wao.

"Nilipoanzisha kikundi kwa ajili ya kuweka akiba watu wengi walikuwa wagumu kujiunga kwa sababu ya kuhofia usalama wa pesa zao, lakini sasa kikundi chetu kina wanachama wafikao 72, wengi wetu ni wafanyabiashara wadogo wadogo.

"Kuweka akiba huku kumekuwa fursa ya maendeleo ya uchumi wetu, kwani tumeweza kupanua biashara zetu, kukidhi mahitaji ya nyumbani, kusomesha watoto wetu shule za kisasa na hata kujenga nyumba," alisema Tunu Hassan, mwenyekiti wa kikoba cha Tuangoma.

# Wananchi washangilia kutatuliwa kero ya maji

Na Mwandishi Wetu

CHANGAMOTO ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama iliyokuwa inawakabili wananchi wa vijiji vya Nandagala 'B' na Ingawali wilayani Ruangwa imekuwa historia baada ya Ubalozi wa Uturuki kupitia taasisi yake ya Diyanet kuwachimbia visima virefu.

Visima hivyo viwili vilikabidhiwa kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa juzi na Muambata wa Ubalozi wa Uturuki anayeshughulikia masuala ya jamii nchini, Muhammed Cicek.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Mkuu alisema Tanzania na Uturuki ni nchi rafiki na kwamba Serikali ya Uturuki imekuwa ikishirikiana na Serikali ya Tanzania katika uboreshaji wa huduma za jamii zikiwamo za afya, elimu na maji.

Waziri Mkuu baada ya kuvipokea visima hivyo aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kupitia kamati zao za maji zihakikishe zinaisimamia vizuri miradi hiyo na pia wawe wanatoa taarifa za mapato na matumizi ya kila mwezi.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amemuagiza Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Wilaya ya Ruangwa, Samwel Pyuza, ahakikishe huduma ya umeme inafikishwa katika mradi huo kwa ajili ya kusukuma maji badala ya kutumia jenereta.

Kwa upande wake, Muambata wa Ubalozi wa Uturuki, Cicek, alisema Watanzania na Waturuki ni ndugu, hivyo amefurahi baada ya wananchi wa vijiji hivyo kupokea zawadi ya visima hivyo walivyowakabidhi.

Wakizungumza baada ya makabidhiano hayo, baadhi ya wakazi wa kijiji cha Nandagala 'B' waliishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma ya maji karibu na makazi yao.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akifungua maji baada ya kukabidhiwa kisima cha majisafi kilichojengwa kwa ufadhili wa Ubalozi wa Uturuki nchini katika kijiji cha Nandagala 'B', mkoani Lindi juzi. Wa pili kulia, ni Muambata wa Ubalozi wa Uturuki anayeshughulikia masuala ya jamii, Muhammed Cicek na kushoto ni Mkurugenzi Mkazi wa Turkish Maarif Foundation, Oguz Hamza Yilmaz. **PICHA: OWM**

# Tuico yaunga mkono uchumi viwanda

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), kimesema kitaunga mkono juhudi za serikali kuhusu mpango wa Tanzania ya viwanda, na kitahimiza wanachama wake waliopo viwandani, kutimiza wajibu wao ipasavyo, ili kufikia azma hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa TUICO Taifa, Paul Sangeze, katika kikao cha 25 cha Baraza Kuu la chama hicho kilichofanyika mkoani hapa, na kusema kuwa juhudi zinazofanywa na serikali zimekuwa zikisaidia kuongeza uhai wa chama hicho, hivyo ni lazima ziungwe mkono.

Mwenyekiti huyo alisema chama hicho kimeguswa na utendaji mzuri wa serikali ya awamu ya tano, hususani katika uendelezaji wa sekta ya viwanda, na kwamba kitahakikisha kinatoa mchango wake ili kufanikisha mpango huo.

Aidha, Sangeze ameelezea nia ya chama hicho, kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa viongozi, utakaofanyika mwaka 2020, na kuwataka wanachama wa TUICO, kuanza kuandaa viongozi ambao watakuwa na maono ya kukiletea maendeleo chama hicho.

Mjumbe wa chama hicho, Eliza Msechu, alitaka uongozi wa serikali kuongeza kasi zaidi ya uanzishwaji wa viwanda hivyo, ili viweze kuongeza ajira nchini na kukuza uchumi wa nchi, ili Watanzania wengi waondokane na umaskini.

Mjumbe mwingine wa chama hicho, Juma Mtoro, alisema kupitia uongozi uliopo madarakani wamenufaika na vitu vingi kupitia chama hicho ikiwamo namna ya uongozi kufuatilia haki na maslahi ya wafanyakazi na mikataba pamoja na kusaidiana na serikali katika juhudi zake ya kuleta maendeleo kupitia uchumi wa viwanda.

# TBS yatoa elimu maonyesho ya maziwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limeshiriki kutoa elimu kuhusu viwango katika Maonyesho ya Wiki ya Maziwa, yaliyofanyika katika Uwanja vya Sheikh Amri Abeid Karume, jijini Arusha, mwishoni mwa wiki.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho hayo, Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, alisema wameshiriki maonyesho hayo ili kutoa elimu kwa wajasiriamali na wadau wa sekta ya maziwa juu ya kuthibitisha ubora wa bidhaa.

Mtemvu alisema shirika hilo linatambua kwamba wajasiriamali ni kundi muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na wana mchango mkubwa katika kuunga mkono juhudi za punguza umaskini na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

"Hivyo na sisi shirika tuna programu ya kutoa elimu kwa wananchi na wajasiriamali kwa kuwafuata popote walipo ikiwamo kwenye maonyesho kama haya ili kuwaelimisha umuhimu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao," alisema.

Ofisa huyo alisema serikali inatambua mchango wa wajasiriamali ndiyo maana imebeba gharama za kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure kupitia TBS.

"Moja ya majukumu yetu ni kuwezesha biashara, hivyo mkakati wetu ni kuwafuata popote walipo ikiwa ni pamoja na maonyesho mbalimbali yakiwamo haya, ili kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa matumizi ya bidhaa zilizothibitishwa ubora," alisema Mtemvu.

Alisisitiza kuwa wajasiriamali hawana sababu ya kuogopa kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao kwa kuwa huduma hizo zinatolewa bure.

Mtemvu alifafanua kwamba mtu anapozalisha, kusambaza na kuuza bidhaa zenye ubora, anapanua soko la bidhaa zake na kuondokana na vikwazo vya kibiashara.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kutumia fursa mbalimbali wanazopewa na taifa kupitia programu mbalimbali kuthibitisha bidhaa zao, ili kuziongezea thamani kubwa zaidi kwenye soko.

Alishauri kwamba ni muhimu juhudi hizo za wajasiriamali zisiishie hapo, bali ziwe endelevu na hatimaye kufikia mafanikio ya juu zaidi.

Katika hatua nyingine, Mtemvu, alitoa wito kwa wananchi kununua bidhaa zilizothibitishwa na TBS. Maonyesho hayo yalifungwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula (kushoto), na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yefred Myenzi, wakichanganya mchanga walipokuwa wakikagua ujenzi unaoendelea wa hospitali ya wilaya hiyo, kata ya Langai, juzi. **PICHA GIFT THADEY**

# Wakulima watakiwa kuchangamkia alizeti

**Na Jaliwason Jasson,** HANGANG

SHIRIKA la Farm Africa mkoani Manyara, limewataka wakulima kuchangamkia kilimo cha alizeti, ili kujiongezea kipato na kuisaidia serikali kuepuka kutumia gharama kubwa kuagiza mafuta nje ya nchi.

Meneja Mradi wa Alizeti kwa Maendeleo Endelevu, Tumain Elibariki, alisema hayo juzi wakati akizungumza na mamia ya wakulima waliohudhuria siku ya wakulima shambani, iliyofanyika kiwilaya katika Kijiji Cha Galangal Kata ya Mulbadaw wilayani Hanang.

Alisema katika kutekeleza mradi huo, Farm Africa inashirikiana na Agricultural Markets Development Trust (AMDT).

"Toka tumeanza, tumewafikia wakulima 5,600 ila kwa Hanang tuna vikundi 80 na tuna mashamba darasa 490. Mwitikio wa wakulima ni mzuri na kufikia Septemba tutakuwa tumefikia lengo letu la wakulima 10,000," alisema Elibariki.

Alisema lengo lao si kufundisha licha ya kuwakutanisha kwenye mashamba darasa, bali ni kuwangalia mifumo ya masoko inafanyaje kazi na namna ya kupata bei nzuri ya mazao yao.

Elibariki alitumia fursa hiyo kuwataka wakulima kuzalisha kwa wingi alizeti ili kuinasua serikali kwenye kuagiza mafuta nje ya nchi kwa gharama kubwa.

"Wakulima wakijitahidi wakazalisha kwa wingi alizeti wataokoa fedha nyingi za kigeni, ambazo serikali ilikuwa inazitumia kuagiza mafuta maana nchi yetu inaagiza asilimia 60 ya mafuta kutoka nje," alisisitiza.

Aliwashauri wakulima kupanda mbegu ya kisasa aina ya Hysun 33, ili kuvuna mazao mengi kwa kuwa inavumilia ukame tofauti na mbegu za asili.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti (Masupa) mkoani Manyara, Othman Kalunde, alisema wana viwanda 234 na wanauhitaji wa tani 120,000, hivyo wakilima zao hilo watakuwa na uhakika wa soko kwa kuwa viwanda hivyo vitanunua alizeti yote.

Mgeni rasmi katika siku hiyo ya wakulima shambani, Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Manyara, Paulo Eugeni, aliwataka wakulima kujikita katika kupanda mbegu mpya ya kisasa ili wabadili maisha yao kupitia kilimo cha alizeti.

Pia aliwaomba Farm Africa na wadau wengine kuongeza wakulima walau mpaka 20,000.

Mwenyekiti wa kikundi cha Umoja, Martha Sulle, aliwaambia wakulima wenzake kuwa wamevuna magunia 153 kwa ajili ya kuzingatia ushauri na elimu waliyopata ya kutumia mbegu za kisasa.

## DC Longido akaribisha wafanyabiashara madini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amewakaribisha wafanyabiashara wakubwa wa madini katika soko la madini lililofunguliwa hivi karibuni katika mpaka wa Namanga.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari ofisini kwake, Mwaisumbe alisema soko hilo litawarahisishia biashara watu hao pamoja na wachimbaji wadogo kuuza madini yao kwa thamani halisi na kuepukana na adha ya kupunjwa na madalali.

"Tumefungua soko la madini hapa Namanga, tunawakaribisha wafanyabiashara wakubwa na wadogo kuja kuuza na kununua madini mbalimbali yanayopatikana wilayani Longido," alisema.

Alisema soko la madini litawanufaisha zaidi wachimbaji wadogo wa madini ya Rubby, yanayopatikana wilayani hapa kwa kujua thamani halisi ya madini hayo tofauti na awali walipokuwa wakiuza kwa madalali bila kufahamu bei halisi.

Mfanyabiashara wa madini wilayani hapa, Gabriel Sendeu, alisema kufunguliwa kwa soko la madini wilayani hapa kutawasaidia wafanyabiashara kupata soko la uhakika la kuuza na kununua madini.

Pia alisema soko hilo litaisaidia serikali kuongeza mapato kwa watu kulipa ushuru na kupunguza utoroshaji wa madini uliokuwa ukifanywa awali na wafanyabiashara wasio waaminifu.

"Kufunguliwa kwa soko la madini hapa Namanga kutapunguza utoroshaji wa madini na kuwarahisishia wafanyabiashara kufanya biashara bila kupitia kwa madalali ambao huwapunja na muda mwingine wanashindwa kununua madini kwa bei inayostahili," alisema Sendeu.

Alisema aina ya madini yanayopatikana kwa wingi wilayani hapa ni Rubby ambayo huchimbwa eneo la Mundarara, hivyo wafanyabiashara watajipatia madini hayo na kununua kwa bei nzuri kupitia soko la uhakika kulingana na mahitaji yao.







Meneja wa Benki ya Exim Kanda ya Kaskazini, Amos Lyimo (kushoto), pamoja na Meneja wa benki hiyo tawi la Moshi mkoani Kilimanjaro, Masood Abutwalib (kulia), wakichangia damu juzi ikiwa ni sehemu ya mpango wa benki hiyo wa uchangiaji damu kila mwaka kupitia matawi yake yote nchini kwa ushirikiano na Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS). Anayewahudumia ni mtaalamu wa afya wa NBTS, Marygoreth Laswai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinyozi jela miaka 30 kwa kubaka

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

FUNDI kinyozi Seif Abdalah, mkazi wa Kijiji cha Karansi, Siha mkoani Kilimanjaro, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya mahakama ya wilaya hiyo kumtia hatiani kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wa kidato cha pili.

Mshtakiwa huyo amekutwa na hatia baada ya mahakama hiyo kujiridhisha kuwa alimbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 15 (jina lake na shule hiyo vinahifadhiwa).

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Siha, Jasmine Abdul, alisema mahakama yake imeridhika na ushahidi uliotolewa na watu wanne ambao ni mashahidi wa jamhuri.

Alisema ushahidi uliotolewa na mashahidi hao mahakamani hapo haujaacha shaka ndani yake, hivyo mahakama hiyo imemwona mshtakiwa ana hatia na adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela. Wakati Hakimu Jasmine anasoma hukumu hiyo, alisema kosa hilo la ubakaji ni kinyume cha kifungu cha 130 (1) (2) (e) na 131 cha Kanuni ya Adhabu cha Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, David Chisimba, kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari Mosi, mwaka huu, majira ya saa 10 jioni katika Kijiji cha Karansi, huku akitambua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa mwanafunzi huyo alibakwa baada ya kwenda katika saluni anayofanya kazi kinyozi huyo, akimtaka kumnyoa nywele zake. Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa nia ya mwanafunzi huyo kutaka kunyolewa haikutumia, kutokana na kinyozi huyo kumrubuni kimapenzi na kisha kumchukua na kwenda kulala naye hadi kesho yake.

Siku iliyofuata baada ya tukio, ilidaiwa kuwa mwanafunzi huyo aliondoka asubuhi na kufunga safari ya kurudi kwa mama yake mzazi anayeishi katika mji wa Bomango'mbe, wilayani Hai, baada ya kulipwa ujira wa Sh. 2,000 kwa kufanya kitendo hicho.

Huko Karansi, mwanafunzi huyo alikwenda kumsalimia baba yake mzazi, wakati wa likizo.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, aliomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, akitaka iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hiyo.

# Walimu waonywa kuhusu hujuma

**Na Paul William,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, kimetoa angalizo kwa walimu wa shule za serikali mkoani humo kujiepusha na ushiriki wa matukio ya kihalifu kama kuhujumu miundombinu ya shule.

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alisema jana kuwa iko haja kwa serikali kutoa semina walau mara moja kwa mwaka, ili kuwasisitiza walimu kulinda na kutunza miundombinu ya shule ili kuepusha hasara na gharama kubwa kwa serikali kufanya ukarabati.

Boisafi alikuwa akizungumza hayo baada ya kuitembelea Sekondari kongwe ya Wasichana ya Ashira iliyoko Marangu, wilayani Moshi.

Mabweni mawili ya ghorofa ya sekondari hiyo yaliteketea kwa moto Mei 23, mwaka huu, na kusababisha wanafunzi 224 kupoteza baadhi ya vifaa vyao, huku wanafunzi 73 wakipoteza kila kitu.

Baada ya kutoa angalizo hilo na kukagua mabweni yaliyoteketea, Boisafi ambaye aliongozana wajumbe wa kamati ya siasa mkoa, alikabidhi misaada ya magodoro 65 kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa shule hiyo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kwa sasa CCM imetanguliza magodoro 63, lakini magodoro mengine 35 watayapeleka baadaye ili kufanya jumla kuu kufikia magodoro 100.

Boisafi alisema kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzake, ili kuhakikisha kwamba mali hizo za umma zinakuwa salama na miundombinu yake inadumu.

Alisema Ashira ni shule peke ya wasichana ya serikali ya kidato cha tano na sita inayofanya vizuri na kwamba CCM imeagiza serikali kufanya uchunguzi wa kina zaidi juu ya tukio hilo la moto na kama kuna watu wamehusika kuihujumu wachukuliwe hatua za kisheria.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Shule hiyo, Elizabeth Abdalah, aliishukuru serikali na CCM kwa kuchukua hatua za haraka katika kutoa misaada mbalimbali.

Aidha, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, akitoa ufafanuzi zaidi kwa niaba ya mkurugenzi alisema tayari timu ya wahandisi kutoka Ofisi ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wameshafika shuleni hapo na kufanya tathmini ya gharama za uharibifu na kwamba muda wowote ukarabati utaanza.

Alisema mabweni yaliyoungua ni bweni la Japan na bweni la Muungano lakini mabweni hayo hayategemeani kwa nishati ya umeme.

# Madiwani wateule wakabidhiwa hati

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU tatu baada ya vyama vinane vya upinzani nchini, kuweka wazi kwamba havitashiriki uchaguzi wa marudio katika kata 32 utakaofanyika Juni 15, mwaka huu, madiwani wawili wateule wa Chama Cha Mapinduzi katika Wilaya ya Moshi, wamekabidhiwa hati maalum za kuthibitisha kupita bila kupingwa.

Madiwani hao ni Deogratius Mushi wa Kata ya Kibosho Magharibi na Bertin Mkami wa Kata ya Uru Shimbwe.

Madiwani hao wateule walikabidhiwa hati hizo maalumu na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi, Castory Msigala.

Mushi na Mkami walijiuzulu nyadhifa zao hizo na kukihama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Aprili, mwaka huu na kujiunga CCM, wakidai kukoshwa na kazi anazozifanya Rais John Magufuli.

Vyama hivyo vinane mwishoni mwa wiki iliyopita, viliweka wazi kwamba havitashiriki uchaguzi huo endapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), haitatekeleza agizo la Mahakama Kuu ya Tanzania la kuwataka Wakurugenzi wa Halmashauri kutosimamia uchaguzi huo.

Vyama vilivyosusia ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi, Chauma, UPDP, NLD, CCK na DP.

Katika hoja yao ya kutotaka kushiriki uchaguzi huo wa marudio, viongozi hao wa vyama hivyo walisema kitendo cha NEC kuwaruhusu wakurugenzi kuendelea kusimamia uchaguzi huo ni kuidharau mahakama na kwamba hata vyama vyao haviwezi kushiriki kwa kuwa kufanya hivyo.

Ukurasa 18



**Uchaguzi mpya Israel Netanyahu akishindwa kuunda serikali**

## UCHAMBUZI:

KUELEKEA UCHAGUZI MKUU;

Dar es Salaam mbioni kupata elimu ya uraia na mpigakura



Ukurasa 19

## Kimataifa



**Trump ataka mpango mkubwa wa kibiashara na Uingereza**

Ukurasa 17


# siasa

JUMATANO JUNI 5, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




**EAC na changamoto za Rwanda 'kujiekeleza' DRC**

Ukurasa 14

# TUNAPOELEKEA katika uchaguzi tusisahau kila uhuru una mipaka yake

**Na Fransisko Mpangala**

KUMEKUWA na maoni kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa nyakati tofauti kutoka kwa watu wa kada tofauti wakiwamo wanasiasa yanayodai kuwapo kwa unyimwaji wa haki zao, hasa hii ya uhuru wa kutoa maoni.

Kwanza niweke wazi msimamo wangu kuwa nakubaliana na natambua kuwapo kwa haki ya kila mtu kutoa maoni yake. Hata katiba yetu ibara ya 18(1) imetamka wazi kuwa kila mtu ana haki ya uhuru wa mawazo kwa kutoa maoni yoyote.

Lakini msingi wa makala yangu utaangazia pale haki ya uhuru wa kutoa maoni inapovuka mipaka na inapotumika vibaya kuvunja haki za wengine.

Tuanze kutafsiri nini maana ya haki? Haki

Endelea 16



**Chama tawala Uingereza chaanza mchakato kupata waziri mkuu mpya**

Ukurasa 15

# EAC na changamoto za Rwanda 'kujiekeleza' DRC

Na Mashaka Mgeta

WAKATI mgogoro wa kidiplomasia kati ya Rwanda na mataifa mengine yaliyo kwenye ukanda wa Afrika Mashariki (EAC) ukiendelea 'kufukuta kimya kimya', taifa hilo lenye mbinu madhubuti za kukuza uchumi wake linaonekana kujielekeza kwa nje ya ukanda huo ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rwanda ambayo kama zilivyo nchi nyingine wanachama wa EAC zinategemewa kwa fursa za biashara na ukuzaji uchumi katika ukanda huo, imekuwa katika mgogoro wa kidiplomasia na Burundi na Uganda na kwa nyakati fulani, dhidi ya DRC iliyo mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Lakini katika siku za hivi karibuni, Rwanda imejitokeza kurejesha uhusiano wa kidiplomasia na baadhi ya washirika wake, ikiwa ni baada ya kuondoka kwa watawala waliokuwa na uhusiano usiokuwa mzuri na utawala wa Rais Paul Kagame.

Miongoni mwa mataifa ambayo utawala wa Rais Kagame unajielekeza katika kukuza ushirikiano ukiwamo wa kibiashara ni DRC, iliyo pia miongoni mwa nchi majirani zake.

Hatua ya Kagame ya kuibuka ghafla kwenye hafla ya kutoa heshima kwa aliyekuwa Kiongozi wa upinzani nchini DRC Ijumaa iliyopita, marehemu Etienne Tshisekedi hivi karibuni, iliibua hisia za kuwapo nia ya kuimarisha ushirikiano zaidi kati ya nchi mbili hizo.

Akiwa nchini humo, Rais Kagame alikaribishwa na Rais Tshisekedi wa DRC ambaye pia ni mtoto wa marehemu Etienne.

Rais Kagame anayetokea Afrika Mashariki na Joao Lourenco, Rais wa Angola katika ukanda wa Afrika ya Kati, wamekuwa na 'harakati' za kuwa karibu na utawala wa Rais Tshisekedi tangu alipomrithi mtangulizi wake, Joseph Kabila.

Pia Rais Denis Sassou Nguesso wa Congo Brazzaville, taifa lililo jirani na DRC alikuwa miongoni mwa waliohudhuria hafla hiyo ya kumuaga marehemu Etienne.

Wakati wa utawala wake, Kabila aliushutumu utawala wa Rais Kagame kwa kuhusika na uchochezi unaosababisha machafuko nchini humo mara kwa mara.

Hali hiyo ilitokea pia wakati wa utawala wa awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, iliporipotiwa kudorora kwa ushirikiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo, lakini akarejea kuwa na ushirikiano wa karibu na utawala wa Rais John Magufuli.

Vyombo mbalimbali vya habari vimeripoti kuwa marais hao walishiriki kikao kifupi na moja ya mambo yaliyojiri ni kushirikiana ili kufanikisha kuviondosha vikundi vya ndani na majeshi ya nje ya Angola yanayohusika na vitendo vya uasi nchini humo.

Azma hiyo inafikiwa katika 'utatu' huo huku wakuu hao wa nchi wakikumbushana hali inavyokuwa tete kiusalama katika mpaka wa DRC na Rwanda.

Machi mwaka huu, Rais Tshisekedi, alishiriki mkutano wa saba wa kimataifa wa wafanyabiashara uliofanyika Kigali, Rwanda na kuwashirikisha viongozi wa kisiasa na wafanyabiashara wa kimataifa, lengo likiwa ni kuchagiza kasi ya uwekezaji wa sekta binafsi na ushirikiano wa kikanda.

Katika mkutano huo, Rais Kagame mwenye nia ya kuwapo soko la pamoja barani Afrika na kuondolewa kwa migawanyiko ya kisiasa anaelezewa anaweza kuishawishi DRC katika suala hilo, ikiwa ni baada ya kudumu kwa 'urafiki wa mashaka' katika uhusiano wa kidiplomasia wa mataifa hayo.

Mkutano huo wa siku mbili ulihudhuriwa na viongozi wa ngazi ya Taifa nchini humo na watendaji wakuu wa kampuni za kimataifa kutoka Togo, Ethiopia na DRC.

Rais Kagame anaamini kuwa pamoja na mataifa zaidi ya 40 kusaini Mkataba wa Makubaliano wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kuruhusu usafirishaji huru wa bidhaa na huduma, utekelezaji wake upo katika kiwango cha chini.

Rais Kagame ambaye nchi yake imejikuta mara kadhaa ikiwa katika migogoro ya kisiasa na majirani zake, anaeleza kuwa miongoni mwa vyanzo vinavyoathiri utekelezaji huo ni uhusiano mbovu wa kisiasa na kusema, "kama siasa zinakuwa mbaya, kila kitu kinakuwa kibaya."

Wakati akiyasema hayo, Rwanda ilikuwa kwenye mgogoro mkubwa wa kidiplomasia dhidi ya Uganda, hali iliyosababisha utawala wa Rais Kagame kuufunga mpaka wa Gatundu na kuutuhumu utawala wa Rais Yoweri Museveni kuwaweka ndani Wanyarwanda, kuvuruga biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na kuyasaidia makundi ya waasi wanaoupinga utawala wake.

Hali kama hiyo ilitokea pia kwa Rwanda dhidi ya DRC kutokana na mataifa hayo kutokuwa na uhusiano mzuri kwa kipindi kirefu kabla ya kuingia madarakani kwa utawala wa Rais Tshisekedi.

Ni kwa mtazamo huo, ushiriki wa mapema wa Rais Tshisekedi katika mkutano mkubwa wa kimataifa wa wafanyabiashara nchini Rwanda, ukatafsiriwa kuwa moja ya viashiria vya kuwapo ushirikiano mkubwa wa baadaye.

Mchambuzi wa masuala ya ushirikiano wa kimataifa, Abdulkadir Mohammed, anasema hatua inayofikiwa na Rwanda ni muhimu kwa taifa lolote kwa vile mafungamano ya kikanda na kimataifa hayaondoi maana kwa nchi husika kutafuta fursa zinazolenga kukuza uchumi na kustawisha maisha ya wananchi wake.

"Ni kweli kwa sasa, Rwanda inajielekeza zaidi katika kurejesha uhusiano wake na mataifa ambayo awali haukuwa mzuri isipokuwa Uganda na Burundi, lakini inaonekana kutanua wigo wake ili kunufaika kwa fursa zilizo nje ya ukanda wa Afrika Mashariki," anasema.

Mwanataaluma ya uhusiano wa kimataifa, Oscar Joseph, anasema pamoja na kuwapo manufaa kwa Rwanda, lakini ipo haja kwa viongozi wa EAC kushughulikia kadhia zinazojitokeza kwa nchi wanachama ili kupunguza hatari ya kufifia kwa ushirikiano kati yao.

Anasema kama kasi ya nchi wanachama kujielekeza katika ushirikiano nje ya ukanda huo itaongezeka, sababu ikiwa ni uhusiano mbovu unaojitokeza kati yao, kuna hatari ya kufifisha ukuaji wa uchumi na soko la pamoja kwa mataifa hayo.

Ingawa ni hivyo, Joseph anasema haiwezekani kuzuia nchi yoyote kutafuta fursa zenye maslahi yanayokidhi maendeleo yake, lakini suala hilo halipaswi kufanyika kwa mtazamo, dhana na nia ya kulikwepa soko ama fursa zilizo kwenye ukanda husika.

*Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.*



Rais Paul Kagame wa Rwanda (kushoto) akiwa na Rais Felix Tshisekedi wa DRC. **PICHA: MTANDAO**

> Rais Kagame anaamini kuwa pamoja na mataifa zaidi ya 40 kusaini Mkataba wa Makubaliano wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kuruhusu usafirishaji huru wa bidhaa na huduma, utekelezaji wake upo katika kiwango cha chini.

UCHAMBUZI

Na Ani Jozeni

# Chama tawala Uingereza chaanza mchakato kupata waziri mkuu mpya

CHAMA tawala nchini Uingereza, Conservative, kiko katika mchakato wa kutafuta waziri mkuu mpya ambaye kimsingi ni kiongozi wa chama hicho bungeni, baada ya Waziri Mkuu Theresa May kutangaza kuondoka madarakani hapo Juni 7.

Viongozi wa Conservative wanatazamia kuwa hadi kufikia mwisho wa mwezi Julai atakayechaguliwa atakuwa tayari kuingia ofisini, mkusanyiko wa ofisi zenye mlango wa kuingia ambao ni namba 10, mtaa wa Downing jijini London, kana kwamba ni nyumba ya kawaida tu.

Hakuna utabiri wowote wa anayetazamiwa, ila aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje akajiuzulu kwa mtafaruku wa Brexit, Boris Johnson, anaonekana kutangulia, licha ya mchuano mkali ngazi za chama.

Taarifa ya kinachotazamiwa katika siku za usoni ziliainishwa katika taarifa ya mwenyekiti wa chama hicho ambaye anateuliwa na kiongozi wa chama bungeni, kusimamia shughuli za utawala.

Pia kuna Kamati ya 1922 ya wabunge wa kawaida (iliyoanza kuwepo mwaka 1922) ambayo itakuwa inapokea majina na fomu za wagombea kuteuliwa kuongoza chama, na kwa maana hiyo kupitishwa kwa nafasi ya waziri mkuu.

Ilisema kuwa hadi kufikia Juni 10, siku tatu baada ya May kuondoka rasmi madarakani, kamati hiyo inatazamia kuwa itakuwa imepokea majina yote ya wanaotaka kuwania uwaziri mkuu.

Ni katika ngazi ya wabunge ambako majina hayo yatachujwa kwa kuhesabu nani anaungwa mkono, huku wa mwisho akiondolewa na mchakato huo kuanza tena hadi wabaki wawili.

Katika hatua hiyo matawi na viongozi wa chama hicho nje ya Bunge, wanaokisiwa kuwa jumla ya wanachama 124,000 au zaidi kidogo ndipo wanapopiga kura kuchagua kiongozi wa chama bungeni, na anayeshinda anakuwa waziri mkuu moja kwa moja bila kuhitaji uchaguzi mkuu.

Katika taarifa hiyo, chama hicho kilimsifu May hasa kwa kujitolea kwake, ujasiri na kufanya kila aliloweza kufikia lengo la Brexit – la kujitoa EU kwa mkataba.

May ataendelea kuwa waziri mkuu wakati mchakato huo unaendelea, hali inayomaanisha kuwa anafuatilia tu kazi za ofisi za kawaida bila jambo jipya kuwekwa mezani ambalo linahitaji mchakato wa kisera bungeni.

Vinara wa Kamati ya 1922 walisema katika taarifa hiyo kuwa wataelekeza juhudi zao kuhakikisha ushindani kamilifu, wa haki na wenye mjadala wa kina ili kumpata waziri mkuu mpya.

Wakikwepa kuzungumzia masuala ya msingi yaliyofikia kujiuzulu kwa May, walisema kuwa wana hisia ya kina kuwa chama hicho siyo tu kinachagua mtu anayefaa zaidi kuwa kiongozi wa chama hicho lakini pia atakuwa waziri mkuu ajaye wa Uingereza. Hawakugusia chochote kuhusu mada hiyo kuu ya Brexit.

Mojawapo ya juhudi za kuhakikisha mjadala mpana na wa kina kuweza kupata kiongozi mpya wa chama hicho ni pamoja na kuwezesha watu ambao si wanachama wa Conservative au hawakipigii kura chama hicho kukutana na wagombea na kutoa maswali ili yajibiwe.

Nje ya Johnson, mwenye nafasi ya uwaziri wa mambo ya nje hivi sasa, Jeremy Hunt naye anagombea, na baadhi wanadhani kuwa ana nafasi kubwa zaidi. Yuko mwanamama mmoja, aliyekuwa Waziri wa Kazi na Mafao ya Kustaafu, Esther McVey na Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa, Rory Stewart.

Mwenyekiti wa Kamati ya 1922 Sir Graham Brady naye ameondoka katika nafasi hiyo baada ya wabunge wenzake kumtaka aingie kwenye kiyang'anyiro.

Kiongozi wa chama cha Labour, Jeremy Corbyin aliendelea kusisitiza kuwa yeyote ambaye atachaguliwa kuwa kiongozi wa Conservative atahitaji kuitisha uchaguzi mkuu haraka ili wananchi watatue hali ya baadaye ya nchi hiyo.

Siyo jambo ambalo hivi sasa linajadiliwa katika chama tawala, kwani May aliitisha uchaguzi kama huo baada ya kuingia madarakani 2016. Hivi sasa kuna mpukutiko kutokana na uchaguzi Bunge la Ulaya; Conservative hawatafanya haraka.

Wakati macho yote nchini Uingereza yanaangalia nani atakayeshinda kinyang'anyiro cha uwaziri mkuu, hatari kubwa zaidi ipo katika uwezekano wa kuunda serikali na kufikia tamati ya Brexit.

Umoja wa Ulaya (EU) uliiongezea Uingereza miezi sita kujipanga kufikia tamati ya suala hilo, baada ya May kuomba muda kutoka Aprili 12 hadi Juni 30, akapewa miezi sita baadaye, kutokana na EU kuhisi kuwa tofauti nchini Uingereza kuhusu namna ya kujitoa ni za kina na huenda zitahitaji muda zaidi, si ajabu uchaguzi mkuu maalum kuhusiana na suala hilo.

Kuna mvutano wa kitaifa wa aina mbili ambao unaichanganya Uingereza pamoja na EU kuhusu jinsi ya kujitoa, kwani wakitoka itabidi mpaka wa Ireland ya Kaskazini, ambayo ni sehemu ya Uingereza, kuwa ni 'mpaka mgumu' na Jamhuri ya Ireland, ambayo iko katika EU.

Kuwepo kwa mpaka 'laini' ni moja ya misingi ya makubaliano ya kumaliza vita vya kigaidi vya IRA (Jeshi la Jamhuri ya Ireland) na hali hiyo ikibadilika, chokochoko zitaanza.

Kwa upande mwingine,. Scotland ambayo ina serikali ya ndani ni muumini wa dhati kabisa wa Umoja wa Ulaya, na endapo Uingereza itajitoa, na ikijitoa bila mkataba, uti wa Scotland utaingia dosari.

Bado wabunge hawajapata njia ya kutokea katika kuchagua kati ya kuondoka EU na mkataba aliofikia May mwezi Februari.

Yaani kubakia katika umoja wa forodha na EU na si uanachama kamili, uwepo wa soko la pamoja, kuondoka bila mkataba wowote na kufanyika kura ya maoni nyingine kutatua suala hilo.

Chama cha upinzani, Labour kinapigania suala hilo lirudishwe kwa wapigakura lakini Conservative wanasisitiza ni suala la kukamilisha utekelezaji wa matokeo ya kura ya maoni ya mwaka 2016.

Kimsingi wabunge wa Conservative wanategea ifikiwe tarehe ya mwisho ya kujitoa EU halafu wapeleke miswada bungeni ya nini cha kufanya kisera, kujazia mapungufu kwa mfano kupunguza kodi kwa bidhaa za nchi za EU, kulegeza visa.

Wakati mjadala unaendelea ndani ya chama tawala na Bunge, kuna mabadiliko yasiyoweza kupuuzwa katika hisia za kisiasa nchini huko kutokana na mkasa wa Brexit, ambako chama kipya cha siasa, Brexit party (kinachotokana na iliyokuwa National Front) kimeibuka.

Katika uchaguzi wa wajumbe wa Bunge la Ulaya nchini Uingereza, chama hicho kilipata asimilia 31, kikashinda majimbo 10 kati ya 11 na kupata viti 28.

Taarifa zinasema chama hicho kiliongoza kikifuatiwa na Liberal Democrats (Lib-Dem) ambao ni wahafidhina kiasi halafu ndiyo Labor wakafuata, huku Conservatives wakitupwa nafasi ya tano. Hata chama cha Mazingira kiliwazidi.

Kwa vile hayo siyo matokeo ya uchaguzi mkuu kimsingi hayabadilishi lolote katika mazingira ya kisiasa lakini yamewasha taa nini wapigakura wanafikiri na wanataka nini.

Mshindi halisi wa kura hiyo ni wanaotaka Uingereza ikitoe bila mkataba kwani hakuna mkataba unaokubalika EU unaoendana na kile wahafidhina wanachotaka, na pia kikubaliwe EU na Labour nchini Uingereza.

Kura ya kuchagua wajumbe wa Bunge la Ulaya imeonyesha kuwa wapigakura wa kihafidhina wana wasiwasi na chama cha Conservative, lakini hawaiungi mkono Labour badala yake, na kwa jumla siasa nchini humo, kama barani Ulaya, zinachukua sura ya kizalendo zaidi.

Ni mwelekeo ambao unawafurahisha walioko madarakani nchini Marekani hivi sasa, kwani Rais Donald Trump aliwasifu Nigel Farage na Boris Johnson kama 'watu makini' katika ukurasa wake wa twitter.

Wengi kati ya wahafidhina nchini Marekani wanaona EU kama una mfumo wa kijamaa uliopitwa na wakati, nchi za Umoja wa Ulaya pia zikiwa na ukiritimba kiasi fulani wa sekta ya umma unaozuia kampuni za Marekani kujitanua ipasavyo.

Marekani iko katika vita ya aina hiyo na China, na si ajabu baadaye vita hiyo iilenge Russia zaidi na pia EU.



Waandamanaji wakionyesha hisia zao juu ya Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya.**PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI



Baadhi ya wafuasi wa vyama vya siasa wakiwa kwenye mkutano wa hadhara.

# Tunapoelekea katika uchaguzi tusisahau kila uhuru una mipaka yake

**Inatoka Uk. 13**

inatafsiriwa kuwa ni jambo ambalo mtu anastahiki au kitu anachostahili kuwa nacho.

Kimahakama neno haki huwa lina maana ya stahiki ambayo mtu anastahili kuipata kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa katika upatikanaji wa kitu au jambo hilo.

Hivyo basi sina tatizo na hatua za wanaharakati wanaopigania haki za binadamu. Kwa kweli ni jambo ambalo halikubaliki hata kidogo kuona mtu anabaguliwa au kunyimwa haki zake eti kwasababu ya jinsia, rangi, kabila, umri au hadhi ya mtu huyo katika jamii.

Ni lazima kila mtu awe sawa na afurahie haki zake za msingi zilizopo kwa mujibu wa sheria.

Ikumbukwe kuwa haki inapaswa kudaiwa na haitolewi kama fadhila. Kwa sababu hii mtu yoyote anayeona amevunjiwa haki zake za kikatiba anaweza kwenda kufungua shauri kwenye Mahakama Kuu kwa mujibu wa ibara ya 30 (3) ya Katiba yetu.

**WAJIBU**

Lakini haki yoyote ile inakwenda sambamba na wajibu. Wajibu maana yake ni ile hali ya kuwa na jukumu la kushughulikia jambo fulani au udhibiti wa jambo au mtu fulani kisheria.

Ni muhimu kufahamu kuwa wajibu hutokea katika kila haki inapohusishwa au kutajwa. Yaani haki haipati maana iliyokamilika bila kutaja au kuihusisha na wajibu.

Kwa mfano kila mtu ana haki ya kuishi kwa mujibu wa Katiba yetu ibara ya 14. Lakini haitoshi tu kuwa na haki ya kuishi bali una wajibu wa kulinda uhai wa mtu mwingine.

Kwahiyo ikithibitika kuwa umekatisha uhai wa mtu mwingine (kuua) kwa kukusudia, basi utahukumiwa kifungo kwa mujibu wa sheria.

Suala la msingi hapa ni kuwa muuaji alipaswa kutimiza wajibu wake wa kulinda uhai wa mtu mwingine hivyo kitendo chake cha kukatisha uhai wa mtu mwingine kwa kukusudia kutamfanya kuwajibika kwa mujibu wa sheria kwa kuwa kitendo cha kuondoa uhai wa mtu mwingine kunasababisha kuondoa haki ya mtu huyo kuishi

Isitoshe Katiba yetu katika Sura ya 3 Ibara ya 12-29 inazungumzia haki na wajibu muhimu kwa raia wa Tanzania. Pia kuna sheria ya utekelezaji wa wajibu na haki za msingi (The Basic Rights and Duties Enforcement Act) Sura ya 3 ya mwaka 1995 ambayo nayo imerejewa mara kwa mara katika kifungu cha 3 cha sheria hiyo, ikisisitiza kuwa sheria hiyo itatumika katika kutekeleza matakwa ya katiba kuanzia ibara ya 12-29 ya Katiba yetu.

Hivyo basi, mtu anayelalamika kuvunjiwa haki zake, anapojaribu kuiomba mamlaka husika kumtekelezea



Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa nchini, kutoka kushoto James Mbatia wa NCCR-MAGEUZI, Prof. Ibrahim Lipumba wa CUF, Freeman Mbowe wa Chadema na Maalim Seif Sharif Hamad. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

matakwa yake, mamlaka hiyo nayo itarejea katika kumuulizia wajibu wake kama ameutimiza.

Sasa tuirudie hali yetu ya kisiasa na kijamii hapa nchini. Siku hizi kulisikia neno 'haki' ni jambo la kawaida sana.

Kila unapopita unasikia watu wakidai haki, si wanasiasa, si watoto, si wafanyakazi, si madereva, si wafanyabiashara, yaani kila mtu ni haki haki haki.

Kwa upande mwingine ni jambo zuri kwa kuwa linatoa picha kuwa watu wanazifahamu haki zao.

Lakini pamoja na hayo madai, binafsi ninaona kuwa wajibu na mipaka ya haki bado havijapewa uzito stahiki.

Yawezekana ni kwa bahati mbaya au makusudi lakini si jambo rahisi sana kuona hao wanaodai sana hizo haki wanazingatia mipaka au hata kutambua wajibu wa haki zao.

Nakumbuka nikiwa Sekondari kulikuwa na kikundi cha kiimani ambacho kilikuwa kinafanya ibada hadi nyakati za usiku sana (kwa baadhi ya siku kwenye wiki).

Kikundi hicho kilikuwa na aina ya kuabudu sisi vijana tunaiita 'kukemea' (waweza kupata picha kidogo hali ilivyokuwa).

Hali ile iliwafanya baadhi ya wanafunzi kwenda kulalamika kwa mwalimu wa malezi kuwa wanapata tabu sana kulala kwa kuwa kuna kikundi cha wanafunzi wanaofanya maombi kwa sauti kubwa nyakati za usiku darasani (madarasa yalikuwa karibu na mabweni).

Hivyo, basi kikundi hicho kikaitwa na mwalimu wa malezi na baada ya kupewa mashtaka yao viongozi wa kikundi hicho cha kiimani walijitetea kuwa wanayo haki ya kuabudu na hapakuwa na mtu mwenye mamlaka ya kuwapangia ni namna gani wanatakiwa kufanya ibada zao.

Hoja yao ilipingwa vikali sana na mwalimu kwa kuwa hata wanafunzi wenzao walikuwa na haki ya kupumzika na kulala sehemu tulivu nyakati za usiku. Hivyo basi akawapa maagizo kuwa watumie muda uliotengwa na shule tu kwa shughuli zao za maombi akiwasisitiza kuwa uhuru wao wa kuabudu lazima uwe na mipaka na wasiutumie vibaya kuleta usumbufu kwa wengine.

Mfano huu naweza kuulinganisha na baadhi ya mambo yanayoendelea hapa nchini.

Ni lazima tutambue kuwa kuna mipaka kwenye hizi haki zetu. Hivyo basi ninasisitiza kuwa tusijisahau sana na ikiwezekana tuzifurahie haki zetu huku tukizingatia mipaka yake.

Mathalan hii haki ya uhuru wa kutoa maoni ambayo ndio inayopigiwa sana kelele. Yawapasa watu wakumbuke kuitumia haki hiyo kwa kuzingatia kuwa kauli zao hazitakuwa za kuudhi, kutukana, kujenga chuki au kuchochea watu wengine kufanya fujo.

Wakumbuke msemo unaosema "Uhuru bila mipaka ni ukichaa".

**Fransisko Mpangala ni mchambuzi wa masuala ya Siasa na Sheria. Kwa maoni zaidi anapatikana kwa barua pepe fransiscompangala08@gmail.com**




Jengo la Mahakama ya Rufani nchini, katika jiji la Dar es Salaam.

## Trump ataka mpango mkubwa wa kibiashara na Uingereza

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amegeukia siasa na biashara wakati alipokuwa akitarajiwa kukutana na Waziri Mkuu, Theresa May, jana, kwenye siku ya pili ya ziara yake ya kiserikali nchini Uingereza.

Akizungumza wakati wa mkutano na viongozi wa kibiashara, Trump alimwambia May kuwa Marekani inaweza kufikia makubaliano muhimu na ya haki na Uingereza baada ya kukamilika mchakato wa Brexit.

Rais huyo wa Marekani amemshukuru May kwa kufanya kazi nzuri zaidi na hata akamuomba aendelee kuwepo ili wakamilishe muafaka huo kabla ya kuachia wadhifa wa uwaziri mkuu.

Ziara ya Trump ya siku tatu kimsingi inaingiliana na kumbukumbu inayofanyika leo Jumatano ya miaka 75 ya operesheni kutokea kumalizika kwa vita kuu ya pili ya dunia, maarufu kama D-Day.

Hata hivyo, inakuja katika kipindi ambacho ni kigumu kwa Uingereza kwa sababu Waziri Mkuu May anajiuzulu kama kiongozi wa chama cha Conservative.

Hiyo ni baada ya kushindwa kufanikisha mpango wa nchi hiyo kujiondoa katika Umoja wa Ulaya (EU), maarufu kama Brexit.

Ataendelea kuwa waziri mkuu hadi mrithi wake atakapopatikana miongoni mwa wagombea 13 ambao lazima wachukue maamuzi magumu kabla ya muda wa mwisho uliocheleweshwa mara mbili wa Brexit, yaani Oktoba 31.

Tayari Trump amelizungumzia suala la Brexit kwa kuiomba Uingereza kujiondoa katika EU bila ya makubaliano na akadokeza kuwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Kigeni Boris Johnson ambaye anaunga mkono Brexit, anaweza kuwa chaguo bora zaidi la kuiongoza serikali ili kukamilisha suala hilo.

Mazungumzo hayo yalihudhuriwa na Waziri wa Fedha wa Uingereza Philip Hammond na Waziri wa Biashara za Kimataifa Liam Fox.

Ujumbe wa Marekani unajumuisha Waziri wa Mambo ya Nchi za Kigeni Mike Pompeo na Waziri wa Fedha Steven Mnuchin.

MAANDAMANO

Wakati wa mazungumzo hayo, kulikuwa na maandamano yenye kelele mitaani yaliyofanywa na maelfu ya watu wanaompinga Trump.

Waandamanaji walibeba sanamu kubwa la mpira lenye sura ya Trump na rangi ya chungwa.

Miongoni mwa wanaoshiriki ni wanaharakati wa mazingira, wanaopinga ubaguzi na waandamanaji wanaounga mkono haki za wanawake.

Kiongozi wa chama cha upinzani cha Labour Jeremy Corbyn anatarajiwa kuzungumza katika maandamano hayo.

Corbyn alisusia hafla ya chakula cha jioni katika Kasri la Buckingham iliyoandaliwa na Malkia Elizabeth II, kama hatua ya kulalamikia sera za Trump.

Anasema maandamano ni fursa ya kuonyesha mshikamano na wale ambao Trump amewashambulia nchini Marekani, kote duniani na pia nchini Uingereza.

May na Trump watakamilisha ziara hiyo watakapoungana na viongozi wengine duniani leo katika bandari ya Uingereza ya Portsmouth kwenye kumbukumbu ya miaka 75 tangu wanajeshi wa Uingereza, Marekani na washirika wengine walipoanza operesheni ya kuikomboa Ulaya mnamo Juni 6, 1944 kutoka mikononi mwa Manazi.

**DW**




Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May (wa pili kushoto), akiwa na Rais Donald Trump wa Marekani (wa pili kulia).Trump yuko ziarani kwa sasa nchini Uingereza. **PICHA: MTANDAO**

# Uchaguzi mpya Israel Netanyahu akishindwa

**Na Anil Kija**

WAPIGAkura wa Israel, wanatazamia kurudi kwenye vibanda vya kutumbukiza kura mwanzo wa Septemba kuchagua Bunge (Knesset) kwa mara nyingine baada ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kukosa ushirikiano wa kutosha kuunda serikali.

Bunge hilo lenye wajumbe 120 linahitaji wabunge wa vyama vya siasa wanaofikia 61 kuunga mkono serikali ili iundwe, na Netanyahu alikuwa anahitaji kiti kimoja kingine kufikia wabunge 61 na siyo 60 hadi alipofikia uamuzi wa kuvunja Bunge.

Kuna kundi moja la mrengo wa kihafidhina linaloongozwa na Avigdor Lieberman, aliyekuwa waziri wa Ulinzi serikali iliyopita, aliyekataa wabunge wake watano wasiiunge mkono serikali, hivyo kulazimisha Bunge livunjwe ili ikiwezekana waongeze vita na kuunda serikali.

Endapo asingevunja Bunge, Netanyahu angehitaji kuacha juhudi za kuunda serikali na kumwachia mpinzani wake, Benny Gantz ambaye alistaafu si kitambo kama mkuu wa majeshi ya Israel, kujaribu kuunda serikali.

Kundi la Jenerali Gantz kimsingi linaelekea chama cha Labour cha zamani na vikundi vingine vyenye mrengo wa kushoto, na si ajabu angehitaji kufikia muafaka na Lieberman kutokana na kushindwa kwa Netanyahu kupata saini yake, licha ya kuwa ni mhafidhina mwenzake.

Tatizo la kufikia muafaka na Lieberman lilikuwa ni yeye kutaka madai ya chama xxx chake yafikiwe kiasi cha kutosha, licha ya kupata viti vitano tu katika uchaguzi mkuu. Ni kutawala kwa kupitia kuhitajiwa kushiriki madarakani.

Netanyahu na washirika wake wanatazamia kuwa watapata ushindi mzuri zaidi katika uchaguzi wa marudio wa wabunge, ili kuondoa haja ya kuhitaji ushiriki wa kundi la Lieberman lenye viti vitano bungeni.

Wapinzani wa Netanyahu miongoni mwa makundi yanayomuunga mkono Jenerali Gantz walimlaumu Netanyahu kwa hatua hiyo, wakisema kufanyika uchaguzi wa Bunge mara mbili ndani ya mwaka mmoja ni matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Walitaka kuwa Netanyahu angemsikiliza Lieberman ili serikali iundwe, na siyo kukataa madai ya chama hicho halafu nchi ianze tena kampeni.

Suala jingine linaloweza kuhatarisha kampeni ya Netanyahu kuelekea uchaguzi mkuu mwingine ni kwamba jua liwake au kuwe na mvua, ifikapo mwanzo wa Oktoba ataanza kufuatilia kesi yake mahakamani ambako anatuhumiwa kwa rushwa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifikia tamati kuwa Netanyahu ana kesi ya kujibu, lakini kundi la vyama vya mrengo wa kulia likiongozwa na kund la Netanyahu bado likapata wingi zaidi wa kura na kufikia viti 60, idadi ambayo haiwezi kufikiwa na kundi la vyama vya upinzani vikiongozwa na Lieberman.

Ni kichekesho au 'kibonzo' kwa wapiga kura wa Israel ambao hawakupiga kura za kutosha kwa Netanyahu kuunda serikali bila kutegemea wapinzani wa kihafidhina, kuhitajiwa kupiga kura tena ili Netanyahu aweze kuunda serikali bila kutegemewa na Lieberman, n.k.

Mpinzani wa mrengo wa kushoto-kati, Yair Lapid alidai katika mahojiano kuwa kufanyika kwa uchaguzi mpya wa Bunge kuna dhamira moja tu, ya kuzuia Netanyahu asifikishwe gerezani, kwa maana kuwa akiunda serikali atakuwa na uwezo wa kupeperusha kesi hiyo.

Moja ya sababu za kushindwa kuunda serikali ilikuwa ni dai la Netanyahu kuwa Bunge lipitishe sheria haraka kuwa yeye na wabunge wenzake wasiwe katika hatari ya kushtakiwa kwa tuhuma zozote mradi bado wanatumika bungeni au serikalini, dai ambalo wapinzani wake hata wa kihafidhina wanalikataa.

Mpinzani wake muhimu zaidi, Gantz alidaka madai hayo kuwa kufanyika kwa uchaguzi ni juhudi ya kujinasua kutoka hatari ya kufungwa jela, punde.

Rais Reuven Rivlin wa Israel alikuwa ametoa ahadi ya kutoruhusu uchaguzi mwingine ufanyike ndani ya mwaka mmoja lakini mwelekeo uliochukuliwa bungeni na kundi la Netanyahu (vyama vya mrengo wa kulia) havikumpa nafasi kufanya maamuzi.

Bado siyo rahisi kujua kama kuna uwezekano wa mabadiliko halisi miongoni mwa wapigakura kumpa ushindi mzuri zaidi Netanyahu, kwa kuondoa uungwaji mkono kwa vikundi vya sera za mrengo wa kati au uhafidhina dhaifu kama Lapid, Lieberman na wengine.

Ina maana pia kuwa uhafidhina kwa jumla unahitaji kuthibitishwa kwa kura nyingine kuchagua wabunge.

Moja ya maeneo yaliyoleta utata katika majadiliano yaliyochukua siku 42 kujaribu kupata muafaka na kundi la Lieberman ni dhamira ya chama chake kulazimisha wafuasi wa dhehebu la kihafidhina (ultra-Orthodox) la dini ya Kiyahudi kushiriki mafunzo ya kijeshi ya lazima kwa vijana.

Wadadisi wanasema kuna zuio dhidi ya uandikishwaji huo jeshini ulioanza mwaka 1948 kwa barua ya utawala wa kwanza wa Kiyahudi ( au Kizayuni) nchini humo, wakati kundi hilo linashikilia viti 16 na ni muhimu kwa juhudi yoyote ya kuundwa kwa serikali ya vyama vya mrengo wa kulia.

Wana matumaini kuwa wafuasi wa Lieberman wataacha kuunga mkono uongozi wake na hivyo kutoa nafasi kwa vyama kuunda serikali.

Kuna mgogoro mwingine kati ya Lieberman na uongozi wa kihafidhina wa makuhani wa dini hiyo kuwa wanataka miiko ya Sabato ifuatwe kwa ukali zaidi, lakini Lieberman anapinga, akisema haungi mkono utawala wa kikuhani, ila wa kizalendo tu.

Kundi la kihafidhina katika dini lina wafuasi wanaoishi katika maeneo hao wenyewe kwa kujitenga na sehemu iliyobaki ya jamii ili kusimamia sheria za Torati kwa ukaribu zaidi, na wanapinga mambo kadhaa yanayotambulisha jamii huru na ya kisasa, kwa mfano matumizi ya 'simu janja' pamoja na kushirikiana bila vizuizi wanaume na wanawake katika jamii.

Kuna kabila la wa-Haredi ambalo ni la wafuasi wa tafsiri kali ya Torati ambayo haiendani na utandawazi, na licha ya kuwa wanaokana kuwa uzalendo wao ni hafifu na hivyo ni tishio la aina fulani kwa usalama wa nchi hiyo, sera zake zina wafuasi wengi nchi za nje ambako Wayahudi wengi wanakaa, kwa mfano Ulaya na Marekani.

Suala ni kuwa misimamo yake inaleta mazingira ya kuaminiwa kwa nchi ya Israel kuwa ina mwelekeo chanya wa kutaka amani, hasa kutokana na upinzani wa wazi wa ultra-Orthodox kwa utamaduni wa kuenzi jeshi na ushindi katika medani ya vita.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifikia tamati kuwa Netanyahu ana kesi ya kujibu, lakini kundi la vyama vya mrengo wa kulia likiongozwa na kund la Netanyahu bado likapata wingi zaidi wa kura na kufikia viti 60, idadi ambayo haiwezi kufikiwa na kundi la vyama vya upinzani vikiongozwa na Lieberman.

Ni hisia rahisi kujenga hasa kwa kuwa Israel imezungukwa na maadui ambao hawatasikitika Israel ikiparaganyika kisiasa, hivyo kuwa na hatari ya fungamano la kisiasa la uzalendo usiokuwa na hisia za dhati za kufikia muafaka na Wanapestina, n.k.

Cha kufurahisha kwa kiasi fulani ni kuwa mkwamo wa kuunda serikali nchini Israel na kujiandaa kwa kampeni mpya na kupiga kura Septemba kuchagua Bunge jipya kutawezesha Marekani kuendelea kukalia mpango wake wa amani katika eneo la Mashariki ya Kati ambao kimsingi umeshindwa kabla ya kutangazwa rasmi.

Mpango huo umevuja kila eneo na unalenga zaidi kusaidia Mamlaka ya Palestina kiuchumi bila kutaja uwezekano wa kuunda dola halisi ya Wapalestina, jambo ambalo linaleta raha kwa baadhi ya washirika wa Marekani eneo la Ghuba kwa mfano Saudia, lakini halikubaliki kwa utawala wa ndani wa PLO (chama cha ukombozi wa Palestina) kinachoongozwa na Rais Mahmud Abbas wa Mamlaka ya Palestina.

Pia kuna kundi la Hamas ambalo linataka Wapalestina waliokimbia eneo ambalo sasa ni Israel wawe na haki ya kurudi, jambo ambalo hakuna chama cha kisiasa nchini Israel kina uwezo wa kulijadili.

Hivyo uchaguzi mpya wa Bunge hauwezi kuendeleza mazungumzo ya amani na utawala wa Abbas au viongozi wa Hamas, ila utaongeza ari ya utawala wa Rais Donald Trump wa Marekani kusaidia utawala wa Netanyahu kuendelea kumega eneo la Ukingo wa Magharibi na kuzima juhudi za Syria na Iran kuandaa mzingiro wa kijeshi, kuongeza mitaro ya kupenya kuingia Israel bila kutumia mipaka, n.k.

Mkwamo wa amani unadumu wakati wapigakura wanajadili taswira ya Netanyahu kama mla rushwa...



Waziri Mkuu Benjamini Netanyahu (kulia), akiwa na aliyekuwa mpinzani wake kwenye uchaguzi uliopita Jenerali Avigdor Lieberman. **PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI

Na Sabato Kasika

# KUELEKEA UCHAGUZI MKUU;
# Dar es Salaam mbioni kupata elimu ya uraia na mpigakura

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam wanatarajia kuanza kupata elimu ya uraia na ya mpigakura mwezi huu, ili kujiandaa kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwaka 2020.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hutoa elimu hiyo kwa kuzingatia kwamba kila mwaka wapigakura wapya wamekuwa wakiongezeka, ambao nao wanahitaji kutambua haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Wakati huu ambao nchi ikielekea katika uchaguzi, baadhi ya wadau wanaoshirikiana na tume hiyo wameanza kujipanga ili kutoa elimu hiyo kwa Watanzania kwa ajili ya kujiandaa kwa uchaguzi huo.

Shirika lisilo la kiserikali linalotoa elimu ya demokrasia, utawala bora, uraia na upigajikura kwa vijana na wanawake la Tanzania Feminist and Youth Change Organization (Tafeyoco) ni miongoni mwa wadau hao.

Mkurugenzi Mtendaji wake Elvice Makumbo anasema shirika hilo linatarajia kuanza kutoa elimu hiyo jijini Dar es Salaam Juni 17, mwaka huu, ili kuhakikisha watu wanajiandikisha kwa wingi.

Makumbo anasema siyo tu watu kujiandikisha kwa wingi, bali pia waweze kushiriki kikamilifu katika katika uchaguzi mkuu unaokuja wa mwaka 2020.

**UTOAJI ELIMU DAR**

Anasema elimu itaanza kutolewa Dar es Salaam Juni 17, hadi Septemba 30, mwaka huu, kisha utoaji wa elimu hiyo utasimama kupisha uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa shirika hilo litasimamia uchaguzi huo kwenye baadhi ya mitaa kama waangalizi huru kwa kushirikiana na halmashauri husika.

Mkurugenzi huyo anafafanua kwamba baadaye elimu itaendelea kutolewa hadi Nec itakapoanza kazi ya kuboresha Daftari la Kudumu la Mpigakura na kuzipa ratiba rasmi asasi zote 24 zilizochaguliwa kutoa elimu.

"Kwa maana hiyo, kuendelea na utoaji wa elimu wakati huo itategemea taarifa ya Nec kwa kuwa ndio wenye mamlaka kisheria ya kutoa tarehe rasmi ya kuanza au kuendelea na zoezi hilo," anasema.

Anasema kwa sasa shirika lake lina nguvukazi ya vijana wazalendo, wasomi 200 wa kujitolea katika utoaji wa elimu ya uraia na ya mpigakura, lakini pia linatoa nafasi kwa vijana wengine wenye umri wa miaka 21 hadi 34.

Anasema hadi sasa wameshapokea maombi ya vijana 500 wasomi na wazalendo wanaotaka kuelimisha umma wa Watanzania na kwamba wanaendelea kufanya uchambuzi na kuangalia vigezo muhimu.

"Tunataka vijana wenye elimu ya diploma, digrii na masters (Shahada ya Umahiri) kwani lengo letu ni kuwa na timu ya watu 500 watakaopewa semina ya siku mbili hadi nne na wataalam wa masuala ya elimu ya uraia na mpigakura," anasema.

Makumbo anasema njia hiyo pia itawaandaa vizuri vijana na kuwaondoa katika uanaharakati pale wanapoanza kutoa elimu kwa wananchi, kwa vile Tafeyoco inataka kuondoa mambo ya siasa katika kazi zake.

"Kimsingi shirika letu halina mahusiano na chama chochote cha siasa wala dini wala kabila, isipokuwa tunafanya kazi na Watanzania wote nchi nzima bila kujali itikadi zao za kisiasa," anasema na kuongeza:

"Tunawaomba wadau wa demokrasia na utawala bora waje tushirikiane kuhakikisha tunaisaidia serikali yetu katika kuboresha na kuongeza ufahamu wa demokrasia ili chaguzi zijazo watu wengi wajitokeze kupigakura na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi."



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage. **PICHA: MTANDAO**

**MAANA YA ELIMU HII**

Mkurugenzi huyo anasema elimu watakayoitoa ni mafunzo kwa wananchi ili kuwapa stadi na ufahamu, maadili, maarifa na mwelekeo wa kuwawezesha kushiriki katika masuala ya umma na kuwatayarisha kwa majukumu ya kijamii.

"Elimu hii pia inawapa wapigakura maarifa na ufahamu kuhusu masuala ya demokrasia, utawala bora na mchakato wa uchaguzi, hasa katika demokrasia ya vyama vingi, ambapo kuna ushindani mkubwa wa kisiasa," anasema.

Anabainisha kwamba elimu ya uraia huwapa wananchi stadi na kuwahamasisha kushiriki katika uchaguzi na kuhakiki raslimali za umma, kwa vile kupata elimu ya uraia na kupigakura ni haki ya mwananchi kikatiba.

Makumbo anasema elimu ya uraia inalenga kuhakikisha kwamba wapigakura wako tayari, wanakubali, na wana uwezo wa kushiriki katika siasa na uchaguzi.

Anaongeza kuwa elimu hiyo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wapigakura wanaweza kutumia haki yao ya kupiga kura na kudhihirisha matamanio yao ya kisiasa kupitia mchakato wa uchaguzi.

"Kwa ujumla haki hii inalindwa na katiba na sheria za uchaguzi, ambazo zinatengenezwa kama njia ya utekelezaji wa katiba ya nchi... tunaamini wananchi wakipata elimu hii watabadilika," anasema.

**MSINGI WAKE NI UPI?**

Makumbo anasema msingi wa elimu hiyo ni kutayarisha hali ya ufahamu ili kuwawezesha wapigakura watarajiwa kushiriki katika uchaguzi ujao na pia kuwawezesha kupiga kura zao kwa matumaini.

"Ikumbukwe kuwa kura ya mtu ni muhimu kwani ndio inayoweza kumweka mtu madarakani au kumwondoa, ila kumekuwapo na dhana potofu, kwamba mtu haendi kupiga kura kwasababu hampendi mgombea fulani," anasema.

Anabainisha, mpigakura hawezi kukaa nyumbani bila kupiga kura kwa kuamini kwamba hiyo ndio njia ya kumkataa mgombea asiyempenda, na kufafanua kuwa hiyo ni dhana potofu, kwa vile kinyume chake ni kumweka madarakani.

> "Ikumbukwe kuwa kura ya mtu ni muhimu kwani ndio inayoweza kumweka mtu madarakani au kumwondoa, ila kumekuwapo na dhana potofu, kwamba mtu haendi kupiga kura kwasababu hampendi mgombea fulani," anasema.

"Elimu hii ni msingi muhimu, ambayo mwananchi wa taifa lolote lile linaloendeshwa kidemokrasia anastahili kupewa, kwani kupiga kura ni haki ya kikatiba... ndio maana sisi tunajiandaa kutoa elimu hiyo," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema elimu hiyo ipo miaka yote kwa vile wapigakura wapya wamekuwa wakiongezeka kila mwaka, hivyo nao hawana budi kuipata na kuitumia katika uchaguzi.

"Elimu kwa mpigakura inafaa kutiliwa nguvu na juhudi endelevu za elimu kwa raia ili kufanikisha utamaduni wa kidemokrasia unaotokana na chaguzi za mara kwa mara, kwani inahusisha wananchi si wapigakura tu," anasema.

Makumbo anasema, kwa kawaida wananchi wanatakiwa kuhusika katika mchakato wa kisiasa mara kwa mara, siyo wakati wa uchaguzi tu, na kwamba ndio maana Tafeyoco, imekuwa ikitoa elimu ya demokrasia, utawala bora, uraia na elimu kwa vijana na wanawake, ambao ndio wapigakura.

**UCHAGUZI 2010, 2015**

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), Jaji mstaafu Lewis Makame, alitaja idadi ya Watanzania waliokuwa wamejiandikisha kwa ajili ya uchaguzi huo.

Mwenyekiti huyo ambaye kwa sasa ametangulia mbele za haki, alisema katika uchaguzi huo walikuwa wamejiandikisha Watanzania 20,137, 303, lakini waliojitokeza kupiga kura walikuwa ni 8,626,283 tu.

Hapa inaonyesha kuwa watu ambao hawakupiga kura walikuwa ni 11,511, 020, ambao ni wengi zaidi kuliko ya wale waliojitokeza kushiriki kwenye uchaguzi huo mkuu.

Jaji Makame aliweka wazi idadi hiyo ndogo ya wapigakura wakati akimtangaza mshindi wa urais katika uchaguzi huo, Jakaya Kikwete, ambaye kwa sasa ni rais mstaafu.

Mwaka wa uchaguzi uliofuata wa 2015, aliyekuwa mwenyekiti wa Nec wakati huo, Jaji Damian Lubuva naye alitangaza idadi ya Watanzania waliojiandikisha na wale waliopiga kura kuwa walikuwa ni 23,161,440.

Kwa mujibu wa Jaji Lubuva, waliojitokeza kupiga kura walikuwa ni 15,589,639, ambapo kwa hesabu hiyo inaonekana kuwa Watanzania 7,571,801, hawakujitokeza kupigakura ingawa walijiandikisha.

Mwaka 2015 unaonekana ulikuwa na unafuu kidogo, kwani zaidi ya nusu ya waliojiandikisha walijitokeza kupiga kura katika uchaguzi huo uliompa ushindi Rais wa sasa John Magufuli.

Hata hivyo, ipo haja ya kuendelea kutolewa kwa elimu ya uraia na mpigakura ili Watanzania wengi wazidi wajiandikisha na kupiga kura kuliko ilivyo sasa, ambapo wengine wamekuwa wakijiandikisha, lakini hawajitokezi kupiga kura.

# Serikali Austria yaanguka chama cha kifashisti kikiumbuliwa kwa rushwa

**Na Anil Kija**



Chansela wa Austria, Sebastian Kurz. **PICHA: MTANDAO**

SERIKALI ya Austria imeanguka na hivi karibuni uchaguzi mkuu mwingine itabidi ufanyike, baada ya kutolewa kwa mkanda wa video unaomwonyesha kiongozi wa chama cha mrengo wa kulia Freedom Party akiwaahidi mawakala wa Russia kandarasi nchini humo wakisaidia chama hicho fedha za kampeni.

Chancellor Sebastian Kurz alisema mwishoni mwa wiki kuwa inabidi umoja huo tawala ufungashe virago baada ya miezi 17 ya madaraka kutokana na kashfa hiyo ya rushwa, iliyomgusa moja kwa moja Heinz-Christian Strache, kiongozi wa chama hicho serikalini. Ilichukua chini ya saa 24 tangu kutolewa kwa video hiyo na serikali kuanguka.

Video hiyo inamwonyesha akiomba fedha kwa mwanamke aliyedhani ni mpwa wa tajiri mmoja wa Russia, wanaoitwa oligarchs (kwa lugha ya hapa si tajiri tu bali inalenga pia kuwa ni fisadi) na ambao wana urafiki wa mashaka na mtawala wa Russia, Vladimir Putin.

Chancellor Kurz alitoa tamko linalosema 'yatosha' akigusia pia changamoto lukuki alizopata akishirikiana na chama hicho cha utaifa siasa kali, ambako chama chake, People's Party kimekuwa kikipata tabu kujibu au kusahihisha matamshi ya kibaguzi ya viongozi wa Freedom Party wanaoshirikiana madaraka.

Chancellor Kurz ni mshirika wa vyama vipya vya mrengo wa kulia, rafiki wa familia ya Rais Donald Trump wa Marekani, akaitwa hafla ya kikazi na mkwewe Trump, Jared Kushner.

Kurz alisema Freedom Party imechafua taswira ya taifa hilo, akisema pia kuwa kilichoko katika mkanda huo hakihitaji mjadala, Chancellor Kurz alisititiza kuwa uamuzi wake haukuwa na uhusiano na taarifa kuwa Strache alikuwa akijihusisha na tafrija za kimapenzi za watu kadhaa kwa pamoja, ila alieleza kuwa haielekei kuwa chama cha Freedom kina mpango wa kubadili mwelekeo wake.

Ni mabadiliko makubwa katika mazingira ya kisiasa nchini Austria muda mfupi kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa wajumbe wa Bunge la Ulaya.

Siasa za Ulaya kwa jumla zimepata pigo kwa kuibuka kwa kashfa hiyo na kuanguka kwa serikali ya Austria kwani Bunge la Ulaya limeongezeka nguvu kadri ushirikiano wa nchi wanachama unavyoimarika, na changamoto nyingi kuzuka.

Kwa mfano Austria imekuwa mwanga wa kukua kwa vyama vya aina mpya vya utaifa mkali mrengo wa kulia ambavyo kimsingi havina imani na Umoja wa Ulaya (EU) kama mfumo wa siasa unaofaa Ulaya yote, na mwelekeo huo unachochewa na Russia ambayo inaona umoja huo unasaidia Marekani kuwa kinara kwa siasa za Ulaya na dunia kwa jumla.

> Ni kama wakinzani wa serikali hiyo ya pamoja ya mrengo wa kulia walikuwa wanangoja litokee jambo ili kilichotokea kisirudiwe tena, na huku nchi nyingine kama Ujerumani ambazo zina vyama vya mrengo wa kulia wa kawaida zikimtaka Kurz kuachana na Freedom Party kwani heshima yake binafsi inakuwa mashakani.

Russia ambayo pia ina serikali ya utaifa mkali inachochea uzalendo huo eneo la lugha ya Kirusi ambalo zamani lilikuwa katika ukanda wa iliyokuwa Soviet Union, ikasambaratika 1991.

Tayari Strache alishajiuzulu baada ya mkanda huo kutolewa, katika mazingira ambayo inaelekea yalipangwa na watu fulani, wakitumia ushawishi wa Russia katika ukanda huo, na lugha ya kawaida ya kisiasa inayotumika kuwasiliana na vyama vyenye mwelekeo wa kifashisti barani humo.

Bado hakuna ufafanuzi wa nini kilimtuma mtu kumtegea kiongozi huyo wa chama cha kifashisti kuingia katika majadiliano hayo, wakati ambapo umoja wa People's Party na Freedom Party ulishaanza kuwa taa ya kukua kwa mrengo huo wa kisiasa barani Ulaya, kwani ndicho kinachohofiwa maeneo mengi barani Ulaya, kuwa vyama vya utaifa ni vya kihuni zaidi.

Kwa mfano Italia ina mshikamano kama huo uliopo madarakani, na nchini Ufaransa 'National Front' inatisha, na sasa inapata msaada mkubwa wa waandamanaji wanaojitokeza karibu kila wiki kutaka serikali ijiuzulu, na wanashabihiana na viongozi wa mrengo wa kulia wa Italia.

Hawajitambulishi na 'National Front' inayoongozwa na mwanamama Marine Le Pen aliyemrithi baba yake Jean-Marie Le Pen (ambaye wakati mmoja alisema hadithi ya kuuawa kwa Wayahudi milioni sita na Ujerumani ya kifashisti haifahamu vizuri, ni tukio la ziada tu wakati wa vita).

Ni tamshi lililoweka bayana ubaguzi unaoendekezwa na vyama hivyo, kushabikia utumiaji nguvu.

Katika mkanda huo Starche aliahidi kutoa kandarasi nono za serikali endapo anapatiwa michango ya kampeni kutoka kwa bilionea huyo mzaliwa wa Russia na mbaya zaidi alijadili jinsi ya kuficha malipo hayo kutoka kwa mamlaka ya serikali, yaani kinyume cha sheria za Austria.

Wachambuzi wa habari wanasema uamuzi wa kusitisha ushirikiano huo serikalini ni njia ya Chancellor Kurz ya kulinda chama chake kisiathirike kwa kuchanganywa na mshirika wake katika kashfa hiyo.

Isitoshe, maelfu ya waandamanaji walikusanyika nje ya ofisi kuu za serikali baada ya mkanda huo kutolewa katika mitandao ya kijamii, hivyo ilibidi afanye uamuzi haraka.

Baadhi ya waandamanaji walieleza matumaini yao kuwa ushirika huo wa vyama viwili vya mrengo mkali wa kitaifa utaanguka na hivyo Austria kurudi katika 'demokrasia,' akimaanisha serikali yenye mwelekeo wa kawaida unaoendana na Umoja wa Ulaya, siyo utaifa na ubaguzi.

Ni kama wakinzani wa serikali hiyo ya pamoja ya mrengo wa kulia walikuwa wanangoja litokee jambo ili kilichotokea kisirudiwe tena, na huku nchi nyingine kama Ujerumani ambazo zina vyama vya mrengo wa kulia wa kawaida zikimtaka Kurz kuachana na Freedom Party kwani heshima yake binafsi inakuwa mashakani.

Baadhi ya wachambuzi nchini Austria wanadhani Chancellor Kurz anaweza kufaidika na janga lililoikumba Freedom Party, wapigakura wake wahamie People's Party kwani nacho kina mrengo wa kulia ingawa si wa kupitiliza, kifashisti.

Bado wachambuzi hawajaridhika kuwa katika uchaguzi mkuu mwingine Chancellor Kurz anaweza kufaulu kuunda serikali ya mrengo wa kulia kivyake bila Freedom Party, hata kama atasomba sehemu isiyo ndogo ya wapiga kura wa Strache.

Hata hivyo, vyama vya kijadi vya Austria vinatazamia kupata afueni kwa kumkosoa Kurz kuwa hakutumia busara au weledi katika kuchagua chama au kiongozi wa kushirikiana katika madaraka, vikiashiria zilikuwapo dalili za kutosha kuwa chama hicho hakiwezi kuaminika. Bado akajitosa kuungana nao kuunda serikali.

Migawanyiko ya kisiasa nchini Austria inaendana na jadi ya migawanyiko na kuundwa kwa serikali za kushirikisha vyama tofauti, kwani People's Party inaungwa mkono na takriban theluthi moja ya wapigakura.

Kwa njia hiyo Freedom Party inapovuka asilimia 15 au 20 ya kura zote inakuwa na uwezo wa kuwa mshirika serikalini, kwani ni ya mrengo wa kulia na inaweza kuendana na sera za kitaifa kama za Rais Trump nchini Marekani, Rais Putin wa Russia na kwa maana hiyo hata Rais Xi Jinping wa China, n.k.

Rais Van der Bellen wa Austria alishtushwa na mkanda huo akisema unaumiza kuangalia, na hauonyeshi sura ya Austria ilivyo, akimlaani Strache.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wa siasa wanaona tukio hili ni kielelezo kuwa Russia inaingia tena katika anga za taifa kubwa shawishi, baada ya kuigawa Marekani kuhusu uchaguzi wa 2016.



# Wazururaji kupelekwa gerezani kulima

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

MKUU wa Wilaya ya Songwe, Samwel Opurukwa, amewataka vijana wote wilayani humo kushiriki shughuli za kilimo na kuonya watakaokutwa hawana kazi ya kufanya watakamatwa kama wazururaji na kupelekwa gerezani ili wakafundishwe kufanya kazi.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa anazindua soko la ufuta lililopo katika Kijiji cha Maleza.

Alisema ni lazima vijana wote washiriki shughuli za kilimo badala ya kuwaachia wazee na wanawake kufanya shughuli hizo.

Alisema watakaokamatwa watapelekwa katika Gereza la Gwala lililopo wilayani humo na kwenda kufundishwa kulima kwa lazima kama Rais Dk. John Magufuli alivyoagiza.

Opurukwa alisema kila mwananchi aishiye wilayani humo lazima ashiriki shughuli za uzalishaji mali na kwamba wanaozurura bila kazi wanaweza wakawa vibaka.

"Katika Gereza la Ngwala kuna zaidi ya ekari 3,000 ambazo zinatakiwa kulimwa na hazijalimwa kwa sababu ya uhaba wa rasilimali watu, sasa kijana tukikukamata kwenye uzururaji lazima tukupeleke ukatusaidie kulima," alisema Opurukwa.

Katika hatua nyingine aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya kilimo cha ufuta ambacho kina soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Aliitaka kila familia kulima ekari zisizopungua tano za ufuta na kuuza katika soko ambalo limeanzishwa wilayani humo ama katika soko lolote ambalo wao wenyewe wataona linawalipa.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi ambao wanajishughulisha na kilimo cha ufuta, waliwaomba wataalamu wa kilimo kuzihakiki mbegu wanazowauzia ili kuepuka kuuziwa mbegu ambazo hazioti.

Mmoja wa wakulima hao, Richard Mihayo, alisema msimu uliopita wakulima wengi waliingia hasara baada ya kuuziwa mbegu ambazo zilikuwa hazioti mashambani.

Alisema kutokana na hali hiyo baadhi ya wakulima waliamua kulima upya na kupanda mazao tofauti huku baadhi wakirudia mbegu zingine tofauti na zile walizonunua madukani.

"Nililima ekari tatu na nikapanda mbegu ambazo mawakala wanauza, lakini mbegu hizo hazikuota nikaamua kuwapigia wataalamu na walipofika shambani kwangu kweli waliona na wakaniambia nilime upya, ili kuepuka hasara wataalamu watusaidie," alisema Mihayo.

Kwa upande wao mawakala wanaouza mbegu hizo walidai kuwa chanzo cha mbegu kutoota ni wakulima kununua mbegu mapema na kuzihifadhi ndani kwa muda mrefu kabla ya msimu kuanza.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Songwe, Abdulkadr Mfilinge, alisema wakati mwingine mbegu huwa hazioti kwa sababu wakulima hufukia kupita kiasi.

Aliwataka kuacha kufukia mbegu za ufuta kwa kutumia ng'ombe na badala yake watumie jembe la mkono kwa kuparua na kumwaga mbegu kisha kufukia kidogo.

# Wawili washikiliwa kwa tuhuma za mauaji

**NA Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wawili wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Ifumbo, wilayani Chunya wakidaiwa kumuua mfanyabiashara wa ufuta kwa kutumia kitu kinachodhaniwa kuwa ni sumu na kumpora Sh. milioni 55. Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu akiwa safarini kuelekea Moshi mkoani Kilimanjaro, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei alisema watuhumiwa hao ni Raphael Walolile na Goliat Walolile.

Kamanda Matei alimtaja marehemu kuwa ni Osward Malambo, mfanyabiashara wa zao la ufuta ambaye alikuwa ananunua katika wilaya za Songwe na Chunya na kuuza Mbalizi, mkoani Mbeya.

Alisema tukio hilo lilitokea Juni 2, mwaka huu na kwamba marehemu ndiye aliyetoa taarifa za kwamba alinyweshwa sumu na watuhumiwa, lakini haijathibitishwa.

"Hawa watuhumiwa walishirikiana na mtu mwingine anajulikana kwa jina la Peter Mpamba, ambaye alikimbia baada ya Osward kufariki, lakini tunaendelea kumsaka na tutahakikisha anapatikana na kutiwa nguvuni," alisema Matei na kuongeza:

"Kwa sasa bado tunasubiri taarifa za daktari ili tujuwe kama kweli alinyweshwa sumu na ikibainika kuwa ni kweli tutawashtaki kwa kosa la mauaji," aliongeza.

Wakizungumza na waandishi wa habari wakati walipokuwa wanachukua mwili wa marehemu katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, waliliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kwa madai kuwa wanapata vitisho kutoka kwa marafiki wa watuhumiwa.

Mwenyekiti wa wanafamilia hao, Mhandisi Selemani Malambo, ambaye ni kaka wa marehemu, alisema ndugu yao aliondoka nyumbani kwao kwenda Mbalizi kuuza ufuta akiwa mzima, lakini baada ya kuuza ufuta wakati akijiandaa kurudi aliombwa na watuhumiwa wakafanye mazungumzo.

Alisema watuhumiwa wawili waliokamatwa ni shemeji zao na mmoja ambaye ametoroka ni mjomba yao na kwamba awali walikuwa na kesi mahakamani ambayo inaendelea mpaka sasa na walimuita ili wakazungumze namna ya kuiondoa kesi hiyo mahakamani.

Mhandisi Malambo alisema watuhumiwa walimtaka ndugu yao huyo wakazungumze naye kwenye moja ya baa zilizopo katika eneo la Kabwe, jijini Mbeya na alipofika akiwa na wadogo zake walimtaka awaache nje ili wasisikie kinachozungumzwa.

Alisema baada ya kuingia kwenye baa hiyo waliendelea na mazungumzo na walimuweka chini ya ulinzi kwa kumuonyeshea bastola na kumuamuru kuchagua kunywa juisi yenye sumu ama kupigwa risasi ndipo akachagua kunywa juisi.

"Alitupigia simu kuwa anaumwa anaomba tumpeleke hospitali na tulipofika alitueleza kila kitu walichofanya, lakini pia alitueleza kuwa walimwambia aweke fedha zote mezani na wakamwambia watawaua wote atakaowaambia," alisema Mhandisi Malambo.

Kwa upande wake mdogo wa marehemu, Erenest Malambo, alisema familia yao inapata vitisho kutoka kwa marafiki wa watuhumiwa akiwamo mmoja anayejitambulisha kwa jina la Hitla kuwa watawaua wote.

Alisema wanawatuma ujumbe kwenye simu wakiwaeleza kuwa wamemuua mmoja na wataendelea kuwaua wengine na kwamba wanamtandao mkubwa na watawaua wote.

Aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia ulinzi wa familia ili wasije wakadhuriwa na watu hao wanaotoa vitisho.



Kazi ya ujenzi wa majengo ya hospitali yenye hadhi ya wilaya ikiendelea katika kijiji cha Suguti, Musoma Vijijini mkoani Mara jana. Serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, huku wananchi nao wakijitolea kwa hali na mali ili kuufanikisha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Aanza ujenzi wa vyoo vya wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MDAU wa maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela, ameanza kutekeleza ahadi ya kukamilisha ujenzi wa vyoo vya wanafunzi wa Shule za Msingi Nero na Mapambano katika Kata ya Iyela, jijini Mbeya, ambavyo ujenzi wake umekuwa ukisuasua huku kukiwa na mkanganyiko wa matumizi ya Sh. milioni 10 za Mfuko wa Jimbo.

Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za St. Patrick Mission za jijini Dar es Salaam, alianza utekelezaji wa ahadi hiyo juzi baada ya kuwasilisha vifaa vya ujenzi kwenye shule hizo vyenye thamani ya Sh. milioni 2.3.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa kwa Kamati za Wazazi wa shule hizo na kaka yake, Mwalimu Anthon Mwaselela, ambaye alisema lengo la kusaidia kukamilisha mradi huo ni kuhakikisha wanafunzi wa shule hizo mbili wanaondokana na adha wanayoipata kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Vifaa alivyowasilisha ni mbao, mabati, misumali, tofali, saruji na vifaa vingine ambavyo vilikuwa vinahitajika kwa ajili ya kukamilisha vyoo hivyo vyenye matundu 16. "Naomba kwa niaba ya Ndele Mwaselela niwakabidhi vifaa hivi kwa ajili ya kukamilisha mradi huu ambao aliwaahidi kuwa atakamilisha, na ameniambia kuwa lengo lake ni kuhakikisha mradi huu unakamilika kabla ya mwezi Julai," alisema Mwalimu Mwaselela.

Wakipokea vifaa hivyo kwa niaba ya wazazi wa wanafunzi wa shule hizo, wenyeviti wa kamati za shule hizo za Nero na Mapambano, walimshukuru mdau huyo wa maendeleo kwa kuamua kuwasaidia watoto wao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Mapambano, George Mwangonele, alisema kukamilika kwa ujenzi wa vyoo hivyo kutasaidia kuwanusuru watoto na magonjwa ambayo yanaweza kulipuka kutokana na vyoo wanavyotumia kuwa na hali mbaya.


Alisema tatizo la vyoo hivyo lilianza kushughulikiwa tangu mwaka 2009, lakini mpaka sasa tatizo halijaisha kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao.

"Kwa niaba ya wazazi wenzangu wa Shule ya Msingi Mapambano, namshukuru ndugu yetu Mwaselela, tulianza naye na akatuahidi kumalizia palipobakia na sasa tunaona ameanza kutekeleza na tutampa ushirikiano ili vikamilike haraka," alisema Mwangonele.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Nero, Amos Mwakalinga, alisema vyoo vya shule hiyo vinavyotumika kwa sasa vinatia kinyaa kutokana na kuharibika kwa kiasi kikubwa na hivyo kuhatarisha maisha ya watoto.

Alisema kutokana na hali ilivyo, watoto wanaogopa kuingia ndani na badala yake wanajisaidia nje hali ambayo inahatarisha afya zao.

Hivi karibuni iliibuka sintofahamu ya mradi huo baada ya wenyeviti wa Kamati za Shule kumlalamikia Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyela kwa madai ya kutafuna Sh. milioni 10 za Mfuko wa Jimbo ambazo zilipelekwa katika kata hiyo kwa ajili ya kukamilisha mradi huo, lakini baadaye Mkurugenzi wa Jiji la





# Shekhe Mustapha awapa neno waislamu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Shaaban, amewataka waislamu kuishi kwa amani na upendo na kujitoa kuwasaidia watu wasio na uwezo wakati wa kusherehekea Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Wito huo aliutoa juzi katika hafla ya kufuturisha watoto yatima zaidi ya 200 iliyoandaliwa na Kampuni ya QNet.

Mbali na futari hiyo pia kampuni hiyo ilitoa zawadi mbuzi, kilo 100 za mchele, kilo 50 za unga, kilo 25 za maharage, kilo 25 za sukari na lita 20 za mafuta ya kula kwa kila vituo kumi vya watoto yatima mkoani humo.

Aliitaka jamiii kuiga mfano uliofanywa na QNET katika kusherehekea Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

"Niipongeze kampuni ya QNET kwa kutayarisha futari kwa vituo vya watoto yatima jijini Dodoma, kwa moyo wa msaada na ushirikiano hasa katika mwezi huu wa Ramadhani," alisema.

Naye, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda, alipongeza kampuni hiyo kwa kuwajali yatima.

Kampuni ya Qnet inafanya biashara ya mtandao duniani, sambamba na tamaduni zake na jitihada za kusaidia jamii, kusambaza upendo, huruma na ukaribu kwa kutoa msaada na kuleta faraja kwa jamii nyingi zisizo na uwezo barani Afrika.

Katika nchi zote ambako kampuni hiyo inaendesha shughuli zake barani Afrika, imeandaa futari kwa ajili ya watoto yatima na wasiyojiweza.

# Magari zaidi ya 150 yaunganishwa matumizi ya gesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam(DIT), imeanza kuunganisha magari kwenye mfumo wa matumizi ya gesi asilia badala ya petroli, ambapo hadi sasa magari zaidi ya 150 yameunganishwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mratibu wa Mradi wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari kutoka DIT, Dk. Esebi Nyari, alipokuwa akizungumza na wabunge waliokuwa wakiangalia gari lililounganishwa na mfumo huo katika viwanja vya Bunge jijini hapa.

Dk. Nyari alisema gesi hiyo inayowekwa kwenye magari inapatikana Mtwara na kwamba mfumo huo unawezesha magari yaweze kutumia gesi na petroli.

"Mfumo huu unakuwa na faida nyingi ambapo gesi hiyo kwa ujazo wa kilo moja ni Sh.1,450, wakati petroli lita moja ni zaidi ya Sh. 2,200, ukiweka gesi asilia unaweza kwenda umbali mrefu zaidi, ambapo kilo moja ya gesi asilia inaenda zaidi ya kilometa 20 wakati petroli lita moja inaenda kilometa 12," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa wamebadilisha mfumo kwa magari zaidi ya 150 na miongoni mwa wanufaika ni Taxify na Uber kwa Jiji la Dar es salaam.

"Mfumo huu bei yake ni Sh.1,800,000 lakini inategemea ukubwa wa gari kwa hiyo cylinder nne ni bei hiyo, lakini ikiwa zaidi ya hiyo inapanda kidogo," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto iliyopo ni upatikanaji wa vituo vya kujaza gesi kwa sababu kwa sasa kipo kimoja eneo la Ubungo Maziwa.

"Lakini DIT tumeshajipanga kutafuta mbia ili aweze kuweka kituo kingine pale DIT na kadri wateja watakavyopatikana tutaweka sehemu mbalimbali, kuelekea barabara za Nyerere, Kilwa, na Tegeta," alisema.

Mratibu huyo alisema wanashirikana na kampuni ya wazawa iitwayo Energo Tanzania Limited ambayo ni kwa ajili ya teknolojia, huku DIT ikitoa mafunzo kwa wataalamu wa kuunganisha mfumo huo.

"Hatuondoi mfumo wa gari uliopo bali tunaongeza mfumo, hivyo kutakuwa na mfumo wa petroli na gesi, unaweza kutumia petroli ukiishiwa unarudi kwenye gesi," alisema.

Kadhalika, alisema mtungi wa gesi wa kilo 15 unaweza kutumika kutembea kilometa 200 tofauti na petroli.

"Gesi yetu hii ni safi haichafui mazingira, ni wakati wa kuachana na matumizi ya petroli na kutumia gesi asilia ambayo ni yetu, tunaomba serikali ipanue wigo wa mtandao wa gesi," alisema.

Aidha, alisema wanatarajia kufanya majaribio kwa magari yanayotumia mafuta ya dizeli ambapo kwa sasa wako kwenye mazungumzo na UDART na BRT, ili wafanye majaribio kwenye magari mawili ya mwendokasi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Felister Bura, alipongeza jitihada za taasisi hiyo na kudai kuwa hatua hiyo itasaidia kujenga uchumi wa nchi.

Naye Mbunge wa Mbulu Vijijini(CCM), Flatei Massay, alionyesha kufurahishwa na mfumo huo na kusema kuwa utasaidia wananchi kuondokana na gharama za mafuta ya petroli kwenye magari.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. James Kiologwe (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa kliniki ya mguu kifundo ndani ya Hospitali ya Rufani ya Dodoma juzi, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mguu Kifundo yaliyofanyika hospitalini hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai awapongeza wanafunzi St. Anne Marie

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ZAIDI ya wanafunzi 120 wa Shule ya St. Anne Marie Academy na Brilliant ambao wamefanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka 2018, wametinga bungeni, huku Spika wa Bunge Job Ndugai akiwapongeza kwa kufaulu kwenye masomo yao.

Akitangaza wageni waliotembelea Bunge juzi, Ndugai alisema wanafunzi hao wamefaulu kwa kupata daraja la kwanza na la pili kwenye matokeo hayo.

Alimpongeza Mbunge wa Bukoba Vijijini(CCM), Jasson Rweikiza ambaye ndiye mmiliki wa shule hizo, kwa malezi mazuri kwa watoto hao ambao wameweza kufaulu kwa kiwango kikubwa na kuwataka wengine kuiga mfano huo.


Akizungumzia ziara hiyo ya kimasomo ya wanafunzi hao, Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabura alisema kuwa wanafunzi hao wamepewa ziara hiyo kama motisha kutokana na kufanya vizuri sana kwenye mitihani yao.

Alisema wanafunzi waliopata fursa hiyo ni wanafunzi 29 wa St.Anne Marie waliopata daraja la kwanza na 59 waliopata daraja la pili na sita wa shule ya Briliant waliopata daraja la kwanza na 20 waliopata daraja la pili.

Ndyetabura alisema imekuwa kawaida kwa shule hiyo kuwapa motisha wanafunzi wa shule hizo na ndiyo sababu shule imekuwa ikipata matokeo mazuri kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa.

Alisema wanatarajia kuanza kuwapeleka nchini Dubai, Uingereza hadi Marekani wanafunzi watakaokuwa wanafanya vizuri kwenye mitihani yao ili iwe chachu kwa wengine kufanya vyema kwenye mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.

"Shule imejiwekea utaratibu wa kuwapa motisha wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi na huwa tunakawaida ya kuwapeleka mbuga za wanyama kama Serengeti, Mikumi, Ngorongoro, hivyo tutaanza kuwapeleka Ulaya," alisema.





Wananchi wakitafuta mahitaji kwa ajili ya sikukuu ya Eid el Fitr, katika eneo la Darajani, mjini Unguja jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Walia bidhaa kuzuiwa Tanzania Bara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuzipatia ufumbuzi kero za biashara ambazo zimekuwa kikwazo kwa wafanyabiashara, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao vizuri kwa kulitumia soko la Tanzania Bara.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda, Waziri asiye na Wizara Maalumu, Said Soud, alisema yapo malalamiko makubwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kushindwa kuingiza bidhaa zao katika soko la Tanzania Bara.

Alisema wakati bidhaa za Zanzibar zikizuiwa kuingia katika soko la Tanzania Bara, bidhaa mbalimbali kutoka Tanzania Bara zinaingizwa Zanzibar bila vikwazo vya kibiashara.

Soud ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima (AFP), alisema ni matarajio yake makubwa kwamba kero hizo zitapatiwa ufumbuzi kwa sababu serikali zote mbili zinaongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tunawaomba mawaziri wetu wa pande mbili kukaa na kulipatia ufumbuzi tatizo hili kwani linarudisha nyuma juhudi za wafanyabiashara wetu katika kupiga hatua ya maendeleo na kulitumia soko lenye idadi kubwa ya watu la Tanzania Bara," alisema.

Naye Mwakilishi wa Magomeni, Rashid Makame Shamsi, aliitaka Wizara kutayarisha sera ya viwanda ambayo itakuwa mwongozo katika kuanzisha viwanda vya aina mbalimbali nchini.

Alisema juhudi kubwa zimeanzishwa za kuwahamasisha wananchi na wafanyabiashara kuanzisha viwanda lakini uzalishaji wa viwanda hivyo pamoja na bidhaa zake, zimekuwa zikiwekewa vikwazo kuingia Tanzania Bara.

"Mheshimiwa Spika, hatuwezi kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika uchumi kama hatuna sera madhubuti ya kuanzisha na kuendeleza viwanda nchini," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mpendae, Mohamed Said Dimwa, aliitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kuvipatia ufumbuzi vikwazo viliopo sasa vya kibiashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ambavyo vinadumaza sekta hiyo.

Alisema takribani bidhaa zote za viwandani zinazozalishwa Zanzibar zimewekewa vikwazo kuingia katika soko la Tanzania Bara na kuwaweka katika mazingira magumu wafanyabiashara kuitikia wito wa kuifanya Zanzibar kuwa nchi ya uchumi wa kati.

"Ni vigumu kutekeleza malengo ya serikali ya kuifanya Zanzibar kuwa nchi ya viwanda kwa sababu bidhaa zinazozalishwa zimewekewa vikwazo kuingia upande wa pili wa soko la Tanzania Bara lenye idadi kubwa ya watu," alisema.

# China kukarabati kiwanda cha makonyo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) limetiliana saini mkataba wa ushirikiano na kampuni ya Kunshan Asia Aroma kutoka China kwa ajili ya kufanyia ukarabati mkubwa kiwanda cha makonyo kilichoko Wawi, Pemba.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema hayo juzi alipokuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Balozi Amina alisema katika makubaliano hayo, kampuni hiyo itanunua tani 1,000 za mafuta ya makonyo na kwamba katika ukarabati huo, kiwanda hicho kitakuwa na njia mbili ikiwamo ya kuzalisha mafuta ya mikaratusi.

Kutokana na mkataba huo, aliwataka wakulima wa karafuu kutumia nafasi hiyo kuzalisha zaidi karafuu na kupata makonyo kwa ajili ya kuyauza ZSTC.

Aidha, Balozi Salum alisema wakulima wana fursa kubwa ya kuzalisha mafuta ya mikaratusi baada ya Zanzibar kupata soko la bidhaa hiyo nchini China.

Alisema kampuni ya Kunshun imeahidi kununua tani 2,000 za mafuta ya mkaratusi kutoka kwa wakulima Unguja na Pemba.

"Hiyo ni fursa nyingine kwa wakulima wa Zanzibar kujikita katika kilimo cha mafuta ya mkaratusi ili kukidhi soko la China," alisema. Alisema hicho, kutokana na mkataba huo, kinatarajia kuongeza uzalishaji baada ya kufunga mashine ya kuchemsha maji na kuzalisha mvuke.

Waziri alisema mashine hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha mvuke wa maji tani nane kwa saa na ufungaji wa vyungu vipya vitano vya kuzalisha mafuta ya mkaratusi, huku akiongeza kuwa kazi za kuimarisha uzalishaji katika kiwanda hicho unatarajiwa kukamilika katika mwaka huu na kazi zote zitagharimu Sh. bilioni 1.3.

Balozi Amina aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh. bilioni 15.597 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

# Hospitali ya meno kujengwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameushukuru uongozi wa kampuni za Okan zenye makao makuu nchini Uturuki, inayokusudia kujenga hospitali ya matibabu ya meno Zanzibar.

Akizungumza jana na Mwenyekiti wa Okan ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo Kikuu cha Okan kilichoko Istanbul, Uturuki, Dk. Shein alisema Zanzibar na Uturuki zina historia kubwa hali ambayo imesababisha lugha ya Kiswahili kutohoa baadhi ya maneno kutoka katika lugha ya Kituruki.

Dk. Shein alisema Zanzibar na Uturuki zina uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu kutokana na uongozi thabiti wa pande zote mbili.

Akieleza kuhusu azma hiyo ya Okan kujenga hospitali ya meno na upanuzi na utoaji wa vifaa kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Shein alisema hilo ni jambo la busara na litasaidia kuimarisha sekta ya afya Zanzibar.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaiunga mkono miradi hiyo na iko tayari katika kushirikiana na kampuni hiyo kubwa katika kuianzisha miradi hiyo baada ya kukamilika kwa taratibu na majadiliano baina ya pande mbili hizo.

Serikali ya Zanzibar, alisema kwa upande wake itaunda timu maalumu na kukaa na timu ya Okan kwa lengo la kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa na linakwenda kwa kasi na kufikia azma iliyokusudiwa.

Alisema Zanzibar kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ina mpango wa kuanzisha masomo yanayohusiana na kada ya utibabu wa meno, hivyo itakuwa jambo la busara kwa Chuo Kikuu cha Okan kushirikiana na SMZ kuanzisha hospitali hiyo.

Naye Okan alimweleza Dk. Shein azma ya kampuni hiyo kupitia Chuo Kikuu cha Okan kuanzisha miradi hiyo mikubwa miwili.

Alisema Okan iko tayari kuanza kwa miradi hiyo mikubwa baada ya kukamilika kwa taratibu zote za serikali zikiwamo mazungumzo ya pamoja kati ya timu za wataalamu wa Uturuki na Zanzibar na kuahidi kuanza ujenzi mara tu baada ya mazungumzo.

# Wataalamu uendeshaji reli ya kisasa kuandaliwa

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimesaini makubaliano na Chuo cha Zhengzhou Railway Vocational and Technical cha China, ili kuwaandaa wataalamu wengi watakaoiendesha reli ya kisasa (SGR).

Pia wataweza kuzalisha watunga sera za reli, maofisa usafirishaji wa reli, pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wengine katika sekta ya usafirishaji nchini.

Akizungumza baada ya makubaliano hayo, Mkuu wa Chuo cha NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema utekelezaji wa mkataba huo utaanza miezi sita ijayo.

"Bado tunahitaji wataalamu wa masuala ya reli nchini, kwa hiyo kuingia kwa makubalinao haya kutawezesha kuwajengea uwezo wataalamu wetu ambapo walimu wa NIT watakwenda china na wale wa China watakuja NIT, hivyo hivyo kwa wanafunzi wa vyuo hivi viwili," alisema Prof. Mganilwa.

Aliongeza kuwa walimu kutoka China watakuja nchini kuwafundisha wanafunzi pamoja na wafanyakazi walioko katika mashirika ya Tazara na TRL kuhusu masuala ya uendeshaji wa reli, ambapo wataweza kuihudumia SGR yetu kwa ufasaha zaidi.

Prof. Mganilwa alisema China wamekuwa wabobezi wazuri katika masuala ya reli, hivyo ushirikiano huo utainufaisha Tanzania ambayo kwa sasa inakwenda katika uchumi wa viwanda, pamoja na kujenga SGR.

"Unapojenga uchumi wa viwanda ni lazima uwe na reli madhubuti, na ndiyo maana Rais John Magufuli ameamua kujenga reli ya kisasa, sasa tutapata walimu wa kutufundisha kuhusu masuala ya reli na namna gani ya kuiendesha reli yetu tunayoijenga," alisema Prof. Mganilwa.

Aliongeza kuwa Tanzania kuna wataalamu wa reli ambao wamebobea katika operesheni, hivyo kupitia makubaliano hayo kutaongeza wataalamu wa sera za reli pamoja na maofisa usafirishaji wa reli.

Naye Rais wa Chuo cha Zhengzhou Railway Vocational and Technical cha nchini China, Kong Fanshi alisema wamekuja NIT kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na wanaamini mahusiano



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akilikokota guta lililosheheni mzigo mkubwa katika Barabara ya Uhuru, jana, hivyo kushindwa kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Wenye ualbino walalamikia kudhalilishwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BAADHI ya makabila nchini yamelalamikiwa na watu wenye ualbino kutokana na kudhalilisha utu na thamani ya watu hao kwa kutumia majina yasiyostahili, hivyo kushawishi hali ya unyanyapaa na kuwapo kwa matukio ya mauaji ama ukatili kwa watu hao.

Malalamiko hayo yalitolewa na Ofisa Mlaghibishi kutoka Shirika la Kimataifa lisilokuwa la kiserikali la kutetea Usalama, Ustawi na haki za watu wenye Ualbino la 'Under the Same Sun', Kondo Sefu, kwenye mafunzo ya siku mbili ya wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu matumizi sahihi ya lugha katika kuandika ama kutangaza habari zinazowahusu watu wenye ualbino.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto za matumizi ya majina sahihi ya makundi ya watu wenye ulemavu na kutolea mfano majina wanayoitwa watu wenye ualbino kuwa ni pamoja na 'walemavu wa ngozi, zeruzeru na albino, hivyo majina hayo kudhalilisha utu na heshima yao.

Alilipongeza Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) kwa kueleza kuwa jina sahihi ni watu wenye albino, hivyo alivitaka vyombo vya habari kutumia jina hilo katika habari mbalimbali za watu wenye ualbino zitakazoandikwa ama kutangazwa ili kulinda utu na heshima ya watu hao.

Awali akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Under the Same Sun, Berthasia Ladislaus, alisema shirika hilo kwa kushirikina na serikali limeweza kusaidia kupunguza matukio ya mauaji na vitendo vingine vya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino. Alisema kuwa katika kipindi cha Januari hadi Mei kumekuwa na matukio mawili tu ya matishio ya utekaji wa watu wenye ualbino katika maeneo ya Ngorongoro na Kwimba, ambapo watu wasiojulikana walitaka kuwadhulu watoto wawili wenye ualbino hata hivyo majaribio hayo hayakufanikiwa.

Hata hivyo, aliipongeza serikali kwa kuchua hatua za dharura ikiwamo kuwahamishia watoto wenye ualbino kwenye baadhi ya shule maalumu kama shule ya Buhangija iliyopo mkoani Shinyanga na Mitindo iliyopo Mwanza kwa sababu za kiusalama.

Akizungumzia mafanikio ya shirika hilo tangu lilipoanzishwa mwaka 2009, Berthasia alisema wameweza kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wenye ualbino kuanzia elimu ya awali hadi chuo kikuu.

Naye Ofisa Sheria wa shirika hilo, Maduhu Wilium, alisema kutokana na elimu inayotolewa kwa watu wa kada tofauti, watu wenye ualbino wameweza kupata haki zao ikiwamo ya kuoa ama kuolewa na tu asiyekuwa na ualbino. Pia haki ya kusoma na kupata ajira mahali popote.

## Wadau miwa wahakikishiwa

**Na Sabato Kasika,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, Assumpta Mshama, amesema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa kilimo cha miwa, ili kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya Siku ya Wakulima wa Miwa wa Kibaha, yaliyoshirikisha wadau kutoka Kilombero, Kagera, Morogoro na Manyara.

Aidha, liipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)– Kibaha kwa kuandaa Siku ya Wakulima wa Miwa-Kibaha ambayo iliwakutanisha wadau wa sekta hiyo na kufanya tathmini ya changamoto zinazoikabili.

"Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa kilimo cha miwa, ili kufanikisha dhamira ya kufika uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Mshama.

Mshama alisema, serikali ilianzisha TARI chini ya sheria ya TARI ya mwaka 2016, huku Wilaya ya Kibaha ikiwa ni miongoni mwa wilaya yenye kituo cha taasisi hiyo kati ya vituo 17 nchini, na kwamba kituo cha TARI -Kibaha, moja ya majukumu yake ni kufanya utafiti wa kilimo cha miwa nchini kwa ngazi ya kitaifa.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSC), Hans Veenstra, alisema kampuni hiyo inaunga mkono utafiti wa kilimo cha miwa.

Alisema KSC imekuwa mmoja wa wadau wanaotumia na kufaidika na utafiti wa taasisi hiyo kuhusiana na kilimo cha zao la miwa, ambao umewanufaisha wakulima wa zao hilo katika bonde la Kilombero.

Alifafanua kuwa katika kufanikisha mkakati wa kuendeleza wakulima wa miwa ambao kampuni hiyo inashirikiana nao, imeajiri maofisa ugani 24 wanaotoa ushauri na mbinu bora za kufanikisha kilimo cha zao hilo.

Ofisa Mwandamizi wa Maendeleo na Mipango kutoka Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Grace Kabate, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, alisema Siku ya Wakulima wa Miwa ni muhimu kwa ajili ya kukuza uzalishaji endelevu wa zao hilo nchini.

## HABARI KIMATAIFA

### Trump ataka mpango mkubwa wa kibiashara na Uingereza

**LONDON, Uingereza**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemweleza Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May kuwa nchi yake inaweza kufikia makubaliano muhimu na ya haki na Uingereza baada ya kukamilika mchakato wa Brexit.

Rais Trump yupo nchini Uingereza katika siku ya pili ya ziara yake ya kiserikali inayotarajiwa kushuhudiwa na maandamano ya umma.

Rais Trump amemshukuru May kwa kufanya kazi nzuri zaidi na hata akamuomba aendelee kuwapo ili wakamilishe muafaka huo kabla ya kuachia wadhifa wa waziri mkuu.

Ziara ya Trump ya siku tatu inaingiliana na kumbukumbu ya miaka 75 ya operesheni ya kumalizika kwa vita kuu ya pili ya dunia. Maarufu kama D-Day. Lakini inakuja katika wakati mgumu kwa Uingereza.

May atajiuzulu kama kiongozi wa chama cha Conservative baada ya kushindwa kufanikisha mpango wa nchi hiyo kujiondoa katika Umoja wa Ulaya – Brexit.

May ataendelea kuwa waziri mkuu hadi mrithi wake atakapopatikana miongoni mwa wagombea 13 ambao lazima wachukue maamuzi magumu kabla ya muda wa mwisho uliocheleweshwa mara mbili wa Brexit, ambao ni Oktoba 31.

Rais Trump tayari amelizungumzia suala la Brexit kwa kuiomba Uingereza kujiondoa katika Umoja wa Ulaya bila ya makubaliano na akadokeza kuwa aliyekuwa waziri wa mambo ya kigeni Boris Johnson ambaye anaunga mkono Brexit, anaweza kuwa chaguo bora zaidi la kuiongoza serikali na kukamilisha suala hilo.

Mazungumzo baina ya viongozi hao wawili yalihudhuriwa na Waziri wa Fedha wa Uingereza, Philip Hammond na Waziri wa Biashara za kimataifa Liam Fox.

Ujumbe wa Marekani unajumuisha Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo na Waziri wa Fedha, Steven Mnuchin.

Wakati wa mazungumzo hayo, kulikuwa na maandamano yenye kelele mitaani yaliyofanywa na maelfu ya watu wanaompinga RaisTrump.

Waandamanaji walibeba sanamu kubwa la mpira lenye sura ya Trump na rangi ya chungwa.

Miongoni mwa walioshiriki ni wanaharakati wa mazingira, wanaopinga ubaguzi na waandamanaji wanaounga mkono haki za wanawake. Kiongozi wa chama cha upinzani cha Labour, Jeremy Corbyn anatarajiwa kuzungumza katika maandamano hayo. Corbyn alisusia hafla ya chakula cha jioni katika Kasri la Buckingham iliyoandaliwa na Malkia Elizabeth II, kama hatua ya kulalamikia sera za Rais Trump.

**DW**

# Jeshi lafuta makubaliano, latangaza uchaguzi mkuu

**KHARTOUM, Sudan**

KIONGOZI wa Baraza la Kijeshi nchini Sudan, Jenerali Abdel Fatta al Burhan, amesema baraza lake limeamua kufuta makubaliano yote ya awali waliyoafikiana na wakuu wa waandamanaji kuhusu kuundwa kwa serikali ya mpito, na badala yake sasa Uchaguzi Mkuu utafanyika baada ya miezi tisa.

Awali, wanajeshi ambao ndio waliomuondoa madarakani Rais wa zamani Omar Al-Bashir Aprili, mwaka huu walikuwa wamekubaliana na waandamanaji kuunda baraza la uongozi ambalo lingeongoza serikali kwa miaka mitatu kabla ya kukabidhi rasmi madaraka kwa utawala wa kiraia.

Tangazo la Jeshi limetolewa wakati huu zaidi ya watu 30 wakiripotiwa kupoteza maisha kutokana na makabiliano kati ya waandamanaji na maafisa wa usalama yaliyotokea siku ya Jumatatu, wakati wa operesheni ya kuwaondoa raia katika kambi yao nje ya makao makuu ya jeshi jijini Khartoum.

Jenerali al-Burhan alisema makubaliano yote ya awali yamefutwa na sasa uchaguzi mkuu utafanyika chini ya uangalizi wa Jumuiya za Kikanda.

Ulinzi mkali umewekwa kuzingira makao makuu ya Jeshi baada ya kushuhudia wanausalama waliokuwa na silaha wakiwavamia na kuwalazimisha kuondoa waandamanaji ambapo mamia walijeruhiwa.

Marekani na mataifa kadhaa ya barani Ulaya, yamekashifu kile yalichosema ni ukatili dhidi ya waandamanaji, wakati huu mataifa hayo yakiendelea kuweka shinikizo kwa jeshi kukabidhi madaraka.

Baraza la usalama la Umoja wa Mataifa litakutana kujadili hali inayoendelea kushuhudiwa nchini Sudan.

Wakati huo huo, Jeshi nchini Sudani limelaumiwa kutokana na mashambulizi yake dhidi ya waandamanaji mjini Khartoum, hatua iliyosababisha watu 30 kupoteza maisha.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres ametaka uchunguzi ufanyike kuhusu kitendo hicho huku akisema kuwa amesikitishwa na taarifa kuwa maafisa wa jeshi walifyatua risasi hospitalini.

Wakati UN ikikemea kitendo hicho, Marekani na Uingereza zimesema ni tukio la kikatili.

Viongozi walioongoza vuguvugu la kutaka utawala wa kiraia kuongoza nchi hiyo, wamesema wamesitisha mawasiliano na serikali ya mpito ya kijeshi na kufanya mgomo.

Vikosi vya usalama vilifika maeneo ambayo watu walikua wakiandamana, juzi na sauti za risasi zilisikika kwenye picha za video.

Katika taarifa iliyosomwa kwa njia ya televisheni ya taifa, Jeshi lilieleza masikitiko yake kwa namna hali inavyozidi kuwa mbaya na kusema kuwa operesheni ilikua imewalenga wanaotia dosari hali ya usalama na wahalifu. Pia limesema kuwa limekuwepo kwa ajili ya kulinda raia.

Awali, wanaharakati walieleza kuwa vikosi vya usalama waliizunguka hospitali moja mjini Khartoum na kufyatulia risasi hospitali nyingine.

Taarifa iliyotolewa na Kamati kuu ya madaktari wa Sudan, walio karibu na waandamanaji walisema watu 30 akiwamo mtoto wa miaka minane wameuawa, na idadi ya waliopoteza maisha inatarajiwa kuongezeka.

Baadhi ya wakazi wamekilaumu kikosi cha Rapid Support Forces, kilichokuwa kikipambana kumsaidia Bashur kubaki madarakani na kushiriki kwake kwenye mzozo wa Darfur magharibi mwa Sudan ulioanza mwaka 2003.

Katibu Mkuu wa UN amezitaka mamlaka za Sudan kufanya uchunguzi kisha kuchukua hatua dhidi ya wale wote waliohusika.

Taarifa yake imelaani matumizi ya nguvu kuwatawanya waandamanaji, na kushtushwa na ripoti kuwa vikosi vya usalama kufyatua risasi kwenye hospitali.

Shirika la habari la Sudan limesema mwendesha mashtaka ameunda kamati kufanyia uchunguzi matukio hayo.

Waandamanaji wamekua wakiweka kambi nje ya jengo la makao makuu ya jeshi tangu Aprili 6, siku tano kabla ya kuangushwa kwa utawala wa Bashir.

Mwezi uliopita, waandaaji na majenerali watawala walikubaliana kuhusu muundo wa serikali mpya na muda wa mpito wa miaka mitatu kuelekea kwenye utawala wa kiraia.

Hata hivyo, hawajaamua kuhusu ni upande upi hasa kati ya raia au jeshi kuchukua nafasi nyingi zaidi.

**BBC**



Rais wa Marekani, Donald Trump (Kushoto) akiwa na Malkia wa Uingereza, Elizaberth, alipokaribishwa jana. **PICHA: REUTERS**

## Mexico yaijibu Marekani juu ya ushuru mpya

**TOLUCA, Mexico**

MEXICO imesema kwamba kitisho cha Rais wa Marekani, Donald Trump, kuiwekea ushuru mpya wa bidhaa zake zinazosafirishwa kwenda Marekani utaumiza uchumi wa nchi zote mbili.

Imesema itasababisha wahamiaji zaidi wa Amerika ya kati kusafiri kupitia Mexico ili kufika Marekani.

Maafisa wa Mexico walieleza hatua iliyochukuliwa na Marekani itasababisha nchi zote kuumia kiuchumi na itawalazimu wanaotafuta uhamiaji Marekani wanaopitia Mexico kwanza kuomba hifadhi nchini humo.

Kwenye mazungumzo yaliyoanza Washington, maafisa wa Mexico walisema wataweza kufikia kiwango fulani cha kutekeleza matakwa ya Rais Trump ya kuzuia idadi kubwa ya wahamiaji wanaopitia Mexico ili kuepuka ushuru wa asilimia tano unaotarajiwa kuanza Juni 10.

Maofisa hao walipinga uwezekano wowote wa makubaliano ya nchi ya tatu itakayowalazimu wanaotafuta uhamiaji Marekani kuanza kuomba hifadhi Mexico.

Balozi wa Mexico nchini Marekani, Martha Barcena alieleza kwamba kuna kiwango kikubwa watakachoweza kufikia katika majadiliano na kiwango hicho ni hadhi ya Mexico.

Alisema ushuru huo wa Marekani unaweza kusababisha msukosuko wa kifedha na kiuchumi na hivyo kupunguza uwezo wa Marekani kukabiliana na kuingiliwa na wahamiaji.

**VOA**

## Waombaji mikopo elimu juu walegezewa masharti

INATOKA UK. 2

hivyo wanaamini muda uliotolewa unatosha kumwezesha mwanafunzi kuandaa nyaraka muhimu pamoja na kuelezwa mwongozo huo.

Alisema wamelazimika kuwa tofauti na miaka mingine baada ya kubaini kuwa waombaji wengi hukimbilia kwenye mtandao na kujaza fomu za maombi wakati mwingine bila kusoma mwongozo.

"Mwaka 2018/2019, waombaji zaidi ya 9,000 kati ya 57,000 waliopata udahili katika vyuo mbalimbali walikosea kujaza fomu za maombi.

Ndiyo sababu mwaka huu tumetembelea shule za sekondari na kukutana na wanafunzi kwa lengo la kuwaelimisha," alisema.

Alisema serikali imefanikiwa kuongeza bajeti ya mikopo hiyo ya elimu ya juu kutokana na ulejeshwaji mzuri wa mikopo unaofanywa na wanufaika.

Badru alisema hatua hiyo inaonyesha Serikali inavyoweka kipaumbele kutoka mikopo katika kuhakikisha inafanikiwa kuongeza idadi ya wasomi nchini, na kuwa hiyo inatokana na fedha ambayo serikali imewekeza kipindi cha miaka 20 tangu mikopo ianze.

"Ni katika kipindi hiki cha awamu ya tano ndicho kipindi pekee fedha iliyokopeshwa imeweza kurudi kiasi kikubwa zaidi na kwa kwa kasi ya haraka zaidi kuliko ilivyowahi kuwa zamani," alisema. "Mwaka 2015 zilirejeshwa bilioni 90, lakini katika kipindi cha miaka minne tunaelekea kurejesha Sh. bilioni 500, hivyo tunapata uhakika wa kukopesha wanafunzi wengi zaidi," alisema Badru.

Mkurugenzi wa Uchambuzi, Upangaji na Utoaji wa Mikopo, Dk. Veronika Nyahenda, alieleza dirisha la maombi limefunguliwa kwa wote wenye vigezo, hata wale wanaoendelea na masomo ambao waliomba mwaka jana hawakufanikiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya kukosea kujaza fomu.

# Waziri afichua siri nzito mikopo ya nje

INATOKA UK. 2

kwa washirika wa maendeleo, ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Anabainisha kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, misaada na mikopo ilifikia Sh. trilioni 1.7, sawa na asilimia 86 ya lengo la kipindi hicho.

Dk. Mpango pia anabainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha, wizara pia ilipanga kuratibu upatikanaji wa mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara ya jumla ya Sh. trilioni 8.9.

Kati yake, Sh. trilioni 3.11 ni mikopo ya nje, Sh. trilioni 1.19 ni mikopo ya ndani na Sh. trilioni 4.6 ni mikopo ya ndani ya kulipia hatifungani zilizoiva. Anabainisha kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, Sh. bilioni 692.3 zilikopwa kutoka nje, Sh. trilioni 3.3 zilikopwa kutoka soko la ndani zikijumuisha malipo ya dhamana za serikali zilizoiva.

**HOJA YA ZITTO**

Akijibu hoja ya Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), kwamba kumbukumbu za Deni la Taifa zinatunzwa kwenye madaftari (counter books), Dk. Mpango alisema mbunge mwenzake huyo amelenga kupotosha.

"Naomba niseme tuhuma alizozitoa Zitto ni 'very serious', haiwezekani tukatunza takwimu za deni la serikali kwa 'counter books', si kweli na ni udhalilishaji kwa serikali, alipaswa kufuta kabisa kauli hiyo," Dk. Mpango alisema.

Alibainisha katika kutunza kumbukumbu za madeni, serikali inatumia mfumo wa utunzaji madeni unaotumika kwa nchi za Jumuiya ya Madola tangu mwaka 1996.

"(Zitto) usipoteshe umma hata kidogo, takwimu za deni ni sahihi. CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) hazuiliwi kufanya ukaguzi wa Deni la Taifa na hata akitaka kuhakiki atafanya hivyo.

"Tofauti (za takwimu za Deni la Taifa na Deni la Serikali) zinaweza zikaja kwa tofauti ya 'exchage rate' (viwango vya kubadilishia fedha) au 'human era' (kosa la kibinadamu). Hata kukiwapo makosa hayo, majadiliano yanafanyika," alisema.

Waziri huyo pia alijibu hoja ya Zitto kuhusu kushuka kwa ukusanyaji wa mapato, akidai kuwa mbunge huyo hafahamu vyema suala hilo kutokana na kile alichoeleza kuwa huenda masuala ya kisiasa yanamchanganya.

"Nadhani siasa inakuchanganya. Kidogo wakati ule ukiwa darasani kwangu unaweza kuona. Uwiano wa Pato la Taifa ni kweli unachukua makusanyo ya kodi unagawanya na Pato la Taifa. GDP imeongezeka kwa kasi kuliko makusanyo ya kodi.

"Ni muhimu Pato la Taifa liendane na ukuaji uchumi. Wakati ule tulikuwa tukitumia kizio cha mwaka 2007, kuna mabadiliko makubwa tangu wakati ule hadi sasa.

"Muhimu kuzingatia baadhi ya nchi za Afrika Mashariki bado hazijabadilisha vigezo vya ulinganifu kama tulivyokubaliana," Dk. Mpango alisema huku akilikumbusha Bunge kuwa Zitto ni mwanafunzi wake katika somo la uchumi Chuo Kikuu.

Awali, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema alijibu hoja hiyo ya Zitto akieleza kuwa si kweli kwamba makusanyo ya kodi yameshuka.

"Watanzania wanaona yanayotendeka kupitia makusanyo ya kodi. Kama makusanyo yameshuka, tungeweza wapi fedha za kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR)?

"Kama makusanyo yangekuwa ya chini, tusingeweza kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme kwenye Mto Rufiji," Dk. Kijaji alisema.

Aliongeza kuwa kabla serikali awamu ya tano haijaingia madarakani, mwaka 2014/15 makadirio ya makusanyo yalikuwa Sh. trilioni 11.9 na kilichokusanywa ni Sh. trilioni 10.66.

"Mwaka 2017/18, makadirio yalikuwa kukusanya Sh. trilioni 17.3, lakini tulikusanya Sh. trilioni 15.25. Ukilinganisha mambo hayo mawili unaweza ukabaini kama mapato yamepungua au la. Takwimu za kodi hazijawahi kudanganya," alisema.




Kiongozi Mkuu wa Waislamu dhehebu la Shia Ithnasheriya Tanzania, Maulana Sheikh Hemed Jalala, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam wikiendi, baada ya kufanya matembezi ya amani ya Siku ya Kimataifa ya Quds yaliyoanzia katika eneo la Ilala Boma hadi viwanja vya Pipo Kigogo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shahidi: Sifahamu sababu kifo cha Akwilina

INATOKA UK. 4

**Wakili:** Ukiwa Hospitali kitanda chako na Koplo Rahimu vilikuwa karibu au mbali

**Shahidi:** Vilikuwa mbali

**Wakili:** Ulikuwa baada ya vitanda mia kumi

**Shahidi:** Siwezi kukadiria

**Wakili:** Mlikuwa wewe na Rahimu au mlikuwa wengi?

**Shahidi:** Tulikuwa wengi

**Wakili:** Unamkubuka uliyekuwa naye jirani

**Shahidi:** Sikumbuki

**Wakili:** Ukiacha tukio la wewe kuwa muathirika, uliwahi kuchukuluwa maelezo juu ya maandamano?

**Shahidi:** Niliwahi

**Wakili:** Nani Ofisa wa Polisi alirekodi mazungumzo yako?

**Shahidi:** Simkumbuki.

Naye, Profesa Safari alimhoji shahidi kama ifuatavyo:

**Wakili:** Ulisema ulikuwa na SMG

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Ilikuwa na risasi ngapi?

**Shahidi:** 30

**Wakili:** Uliwahi kutumia

**Shahidi:** Sikuitumia

**Wakili:** Ulibeba tu hukuitumia?

**Shahidi:** Sikuitumia

**Wakili:** Askari wenzako waliitumia au hawakuitumia

**Shahidi:** Sikumbuki

**Wakili:** Unafahamu kwenye tukio hilo alikufa Akwilina

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Unajua kilichomua

**Shahidi:** Sijui

**Wakili:** Unatumia pombe

**Shahidi:** Situmii

**Wakili:** Sigara unavuta

**Shahidi:** Sivuti

**Wakili:** Sigara kali unavuta

**Shahidi:** Sivuti.

Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri mfululizo Julai Mosi mpaka 4, mwaka huu.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime, Mjini Esther Matiko; Katibu Mkuu Taifa,Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu- Zanzibar, Salu mMwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDAO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACEBOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33

## MCHANGANYIKO

**MONKALI INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu ya muda mrefu,inarejesha kongosho katika utoaji ute mchunguna kuwa normal balance 4.5.6 ipo ktk mfumo wa maji na vidonge husaidia mmengenyo wa chakula , tiba lishe, gaut, vidonda vya tumbo,bawasili, 0713293988/0758078280.

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 39/2019

Ombi la IBRAHIM E. SUMBE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **MCH. JUDITH W. SUMBE**
**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 13/06//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 3/6/2019

215261102

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.29 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late JAMES ANYINGISYE MWANGIDE**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by PRISCA ADAM MWAKALUKWA**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 26th /06/2019.

Dated at Dodoma this ….29TH /05/2019

215261002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA
Usimamizi wa Mirathi NAMBA 17/2019
Ombi la **ABUBAKARI ISSA MBELA** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu MWASITI ABDALLAH MIZE

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 28/06/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 31/5/2019

215260902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**THEONEST KAJUMA RUHILABAKE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NADIA rangi SILVER yenye namba za usajili **T 781 BDR.** Chassis namba **SXN10056822,** Engine namba **3S8014613.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM /TR/RB/819/2019.**

115262002

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**MUSSA MBOYI GULAKA** anatangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja yenye **Plot No. 741 Block KK (HD).** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SHY/RB/2019.**

115262302

## GOROFA INAUZWA



**BOKI KAMWANGA STR**
**LOW DENSITY AREA**
**BLOC "C",**
**PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311***

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# JUVE, POGBA WATETA

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus inataka kumsajili Paul Pogba kutoka Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto na tayari imeshafanya mazungumzo na wawakilishi wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akihusishwa na mpango wa kundoka pale Old Trafford na Juventus ambayo ni klabu yake ya zamani inapewa nafasi kubwa ya kumnasa.

Ingawa amekuwa na nafasi kikosi cha kwanza chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer, ambaye alitua hapo Desemba mwaka jana baada ya kutimuliwa kwa Jose Mourinho, lakini Pogba anaonekana kuwa hana mpango wa kuendelea kubakia hapo.

Pia amekuwa akiwaniwa na Klabu ya Real Madrid, lakini Juventus ambayo ilimuuza Pogba kwa United kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89, mwaka 2016 - sasa wanataka kumrudisha tena Turin.

Imedaiwa kwamba mawasiliano tayari yameshafanywa na wakala wa Pogba, Mino Raiola juu ya uwezekano wa kutua pale kwenye dimba la Allianz, huku United ikiwa inajua kuhusu mawasiliano hayo.

Pogba alitumia miaka minne pale kwa 'Kibibi Kizee' cha Turin baada ya kuondoka Old Trafford mwaka 2012 kwa uhamisho huru.

Alicheza pamoja na Andrea Pirlo na Claudio Marchisio, na haraka akawa mchezaji muhimu wa Juventus na wakalitwaa taji la Serie A.

Alirudi Old Trafford miaka mitatu iliyopita na amefunga mabao 31 katika mechi 135 tangu arudi katika klabu hiyo.






# CHELSEA
## YAMGEUKIA GRACIA AMRITHI SARRI

**LONDON, England**

KOCHA wa Watford, Javi Gracia, anafikiriwa kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri pale Chelsea kama Muitaliano huyo ataondoka Stamford Bridge kwenda Juventus, ESPN FC imebainisha.

Licha ya kuiongoza klabu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi ya Europa kwa kuifunga Arsenal kwenye fainali mjini Baku wiki iliyopita, majaliwa ya Sarri hapo Chelsea yamebaki kuwa shakani.

Sarri amekuwa hana uhusiano mzuri na kikosi cha Chelsea na tayari yeye mwenyewe amebainisha kwamba anataka kuondoka.

Massimiliano Allegri, ambaye aliondoka Juventus baada ya kushinda taji la Serie A katika misimu yake yote mitano hapo Turin sasa nafasi yake inatajwa kuchukuliwa na Sarri.

Lakini vyanzo kadhaa vimeitonya ESPN FC kwamba Chelsea wanataka kufanya mazungumzo na Gracia ili kchukua nafasi ya Sarri ambaye alitua hapo baada ya kutimuliwa kwa Antonio Conte.

Gracia mwenye umri wa miaka 49, anaonekana kuwa mtu sahihi wa kuchukua mikoba ya Sarri kipindi hiki cha majira ya joto.

# Lichtsteiner atangaza kuondoka Arsenal

**LONDON, England**

BEKI wa Arsenal, Stephan Lichtsteiner, ametangaza kwamba ataondoka klabuni hapo wakati mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto baada ya kukaa na 'Washika Bunduki' hao kwa msimu mmoja.

Lichtsteiner, ambaye alitimiza umri wa miaka 35 Januari mwaka huu alijiunga na Arsenal kwa uhamisho huru akitokea Juventus kipindi cha majira ya joto kilichopita baada ya kushinda taji la Ligi Kuu ya Italia mara saba mfululizo.

Beki huyo mkongwe raia wa Uswisi hakuwa na wakati mzuri zaidi pale Arsenal akicheza mechi 23 katika mashindano yote huku akianza katika mechi 10 tu za Ligi Kuu.

Alikuwa benchi wakati Arsenal ikifungwa kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa dhidi ya Chelsea.

Lichtsteiner aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Istagram, "Ndugu zangu 'Washika Bunduki', tunakabiria kuweka ukurasa mpya katika historia ya klabu. Lakini kwa bahati mbaya nalazimika kuwaaga.

"Ulikuwa wakati mzuri nilipotua Arsenal na kwa hakika nilikuwa na muda mzuri wa kucheza kwenye Klabu kubwa kama Arsenal.

"Nawatakiwa wachezaji wezangu wote kila la heri, na naamini tutakutana wakati mwingine."






ruiz

Joshua

# JOSHUA SASA ASHAURIWA KUMTEMA KOCHA WAKE

**NEW YORK, Marekani**

BAADA ya kupokea kipigo kikali, bondia Anthony Joshua ameshauriwa kumtimua kocha wake, Rob McCracken kwani ni mtu wa daraja la tatu.

Ushauri huo umetolewa na bondia wa zamani wa uzito wa juu na bingwa wa dunia, Lennox Lewis ambaye amemwambia Joshua kuwa aachane na mwalimu wake ambaye anamfundisha, baada ya kupokea kichapo kutoka kwa Andy Ruiz.

McCracken amekuwa kocha wa Joshua kwa muda mrefu sasa huku akimpatia mafanikio ya kutwaa ubingwa wa IBF, WBA na WBO, lakini Lewis anaamini anapaswa kuachana na mwalimu huyo hasa kutokana na matokeo hayo ya aibu aliyopata kwenye ukumbi wa Madison Square Garden Jumamosi.

"Ninasema huwezi kwenda duniani huku ukiwa na mwalimu wa daraja la tatu, huwezi kuwa na jibu la maswali yako kwa daraja analolitaka, anahitaji kuwa na profesa.

"McCracken ni mwalimu, lakini kwa sasa Joshua hawezi kuendelea kuwa chini yake kwa sababu daraja lake ni la chini.

"Sidhani kama kuna umuhimu wa kuendelea kuwa na mwalimu ambaye kiwango chake kipo chini," alisema Lewis.

# Liver kucheza Klabu Bingwa Dunia Qatar

**LONDON, Englad**




LIVERPOOL itasafiri kwenda Qatar Desemba mwaka huu kwa ajili ya kushiriki michuano ya Klabu Bingwa Dunia ya Fifa baada ya nchi hiyo kutangazwa kuwa itakuwa mwenyeji.

Michuano hiyo ambayo hushirikisha klabu bingwa kutoka mabara sita, itafanyika Qatar na Liverpool ambayo ni bingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, itaanza kushiriki mashindano hayo hatua ya nusu fainali.

Qatar itakuwa mwenyeji wa mashindano hayo mara mbili, mwaka huu na mwakani na pia itandaa mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2022.

Awali, iliripotiwa kwamba michuano hiyo ya Klabu Bingwa Dunia, haitafanyika mwaka huu baada ya Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa, kufanya mabadiliko.

Moja ya mabadiliko hayo ni kwamba timu zitakuwa 24 na mashindano hayo yatafanyika kila baada ya miaka minne badala ya mashindano ya Kombe la Mabara.

Liverpool kwa mara ya mwisho ikishiriki mashindano ya Klabu Bingwa ya Dunia nchini Japan mwaka 2005, ilifungwa bao 1-0 kwenye fainali na waliokuwa mabingwa wa Amerika Kusini, Sao Paulo.

Real Madrid ilishinda michuano iliyopita ya Klabu Bingwa Dunia kwa kuwafunga Al Ain ya Falme za Kiarabu kwa mabao 4-1 kwenye fainali ya Desemba mwaka jana na kulitwaa taji hilo kwa mara ya tatu.

# SEMENYA
## ENDELEA NA RIADHA - MAHAKAMA

**GENEVA, Uswisi**

MWANARIADHA wa kike, Caster Semenya, hatahitajika kutumia dawa za kupunguza kiasi cha homoni za kiume ili kushiriki mashindano baada ya Mahakama ya Uswisi kusitisha kwa muda hukumu iliyotolewa na Shirika la Riadha duniani, IAAF.

Bingwa huyo wa Olimpiki wa mbio za mita 800 mwenye umri wa miaka 28, mwezi uliopita alishindwa kesi katika Mahakama ya Usuluhishi wa Migogoro Michezoni (Cas) alipokua akipinga hatua ya kupunguza kiasi cha homoni za kiume ili kukithi vigezo kwa wakimbiaji wa kike.

Hukumu hiyo ingewaathiri wanawake wanaoshiriki mbio za mita 400 ambao wanaonekana kuwa na homoni nyingi za kiume.

"Nina matumaini kuwa baada ya rufaa kwa mara nyingine nitaweza kukimbia nikiwa huru," alisema Semenya mara baada ya hukumu hiyo akiwaambia waandishi wa habari

"Ninashukuru majaji wa Uswisi kwa uamuzi wao."

Baada ya uamuzi wa mahakama ya usuluhishi wa migogoro michezoni, Semenya alikata rufaa kwenye Mahakama ya Uswisi, akieleza nia yake ya kutetea haki za binadamu.

Wakili wake daktari Dorothee Schramm, alisema: "Mahakama imemuwekea ulinzi wa muda Caster Semenya."

"Hii ni kesi muhimu kwa kuwa italeta matokeo mazuri katika kuzingatia haki za binadamu linapokuja suala la wakimbiaji wanawake," alisema daktari huyo.

Katika hukumu yake, awali Cas ilibainisha kuwa sheria mpya zilizotolewa na IAAF kwa wakimbiaji wa kike wenye homoni kwa kiwango kisicho cha kawaida ni za kibaguzi, lakini ikahitimisha kuwa hatua hiyo ilikua "lazima, na yenye muhimu, wa kueleweka na wa uwiano kwa ajili ya kulinda maadili ya wanariadha wanawake."

IAAF imesema bado haijapokea nakala yoyote kuhusu uamuzi mpya wa Mahakama ya Uswisi.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO AWATOA MESSI, RONALDO BALLON D'OR 2019

Mchezaji bora duniani anapaswa kuwa mshindi, kama Juve ama Barca ingetwaa Ligi ya Mabingwa...

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, amefunguka sababu ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi hawataweza kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia mwaka huu ['Ballon d'Or'].

Kwa mujibu wa kocha huyo ambaye pia aliwahi kuinoa Real Madrid, mchezaji bora wa dunia anapaswa kuwa "mshindi" na kwa kutaja neno mshindi, akimaanisha utukufu wa Ligi ya Mabingwa.

Licha ya kuwa na msimu mzuri kwa upande wa mafanikio binafsi, Lionel Messi wa Barcelona amemaliza msimu kwa landha chungu mwezi uliopita. Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alishindwa kuiwezesha Barcelona kutwaa mataji mengine matatu kwa msimu.

Messi na washirika wenzake, walishuhudiwa wakiwa na usiku mbaya zaidi katika soka la Ulaya, kufuatia Liverpool kupindua matokeo katika Uwanja wa Anfield baada ya kushinda 3-0 katika mechi ya mkondo wa kwanza Camp Nou walijikuta wakipigwa 4-0 ugenini.

Miamba hao wa Catalunya pia walishindwa kutwaa mataji mawili ya ndani, wakiwa tayari wametwaa ubingwa wa La Liga Aprili mwaka huu walijikuta wakipigwa na Valencia katika mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'].

Hali kadhalika, Juventus na Cristiano Ronaldo waliweza kutwaa taji la Serie A kirahisi, lakini wakishindwa kufurukuta kote kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Copa Italia, baadhi ya mambo yaliyowaharibia msimu wao.

Licha ya kufunga mabao 28 katika msimu wake wa kwanza Italia, Ronaldo alijikuta akiishia robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kufuatia Juventus kushtukizwa kipigo na Ajax.

Akizungumza na Eleven Sports Portugal, kocha huyo raia wa Ureno, Mourinho alijadili sifa za kushinda Ballon d'Or.

"Mchezaji bora duniani anapaswa kuwa mshindi," alisema kama alivyonukuliwa na Marca.

"Kama Juventus ingetwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya tungeweza kusema kwamba Ronaldo atashinda Ballon d'Or."

"Endapo Barcelona ingetwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, tayari ikiwa imeshinda ubingwa wa La Liga, na kama itashinda Copa America tuzo itakuwa kwa Lionel Messi," aliongeza.

**KIFUATACHO**

Ronaldo ataiongoza Ureno kuivaa Uswisi leo kwenye mechi ya nusu fainali ya michuano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya ['UEFA Nations League']. Vile vile, Messi anajiandaa kuichezea Argentina kwenye michuano ijayo ya Copa America nchini Brazil.

## KWA UFUPI

### MADRID MCHECHETO KWA SALAH
Real Madrid inahofu Manchester United na Bayern Munich zitatoa ushindani kwao katika kuwania saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Misri, Mohamed Salah, 26, kutoka Liverpool majira haya ya joto. ***(AS - in Spanish)***

### GRACIA ANUKIA KUINOA CHELSEA
KOCHA wa Watford, Javi Gracia, anapewa nafasi ya kurithi mikoba ya Maurizio Sarri Chelsea, kama Mtaliano huyo ataondoka Stamford Bridge kwenda kuinoa Juventus.***(ESPN)***

### AUBAMEYANG AGOMBEWA CHINA
KLABU za China, Guangzhou Evergrande na Shanghai SIPG zinavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang na zimempa ofa ya kumlipa pauni 300,000 kwa wiki. (Times)

### SARRI KUPEWA MITATU JUVE
Juventus inajiandaa kumpa mkataba wa miaka mitatu Maurizio Sarri utakaogharimu pauni milioni 6.22 kwa msimu. ***(Corriere della Sera - in Italian)***

### TAJIRI PSG KUINUNUA LEEDS
Nasser Al Khelaifi, ambaye ni kiongozi mkuu wa Qatar Sport Investment - wamiliki wa Klabu ya Paris St-Germain - atakutana na wawakilishi wa Leeds United mjini Doha kwa lengo la kuinunua klabu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza England, Championship. ***(L'Equipe - in French)***

### HAZARD KIMEELEWEKA MADRID
Eden Hazard anatumai kukamilisha uhamisho wake kutoka Chelsea kwenda Real Madrid na mchakato huo alitarajia kuukamilisha mapema jana. ***(Evening Standard)***

### FELIX KUZIGONGANISHA CITY, UTD
Manchester City na Manchester United zinajiandaa kukutana uso kwa uso katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Benfica, Mreno Joao Felix kwa pauni milioni 120. ***(Mirror)***

### JUVE KUMREJESHA POGBA
Juventus inataka kumsajili kwa mara nyingine kiungo wa Manchester United, Mfaransa Paul Pogba. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, aliwatumikia mabingwa hao wa Serie A kwa kipindi cha miaka minne kati ya mwaka 2012-2016. ***(Sky Italy)***

### JORGINHO APINGA SARRI JUVE
KIUNGO wa Chelsea, Mtaliano Jorginho, 27, amesema itakuwa ni "usaliti" kwa kocha wa zamani wa Napoli, Maurizio Sarri kujiunga na Juventus. ***(Standard)***

### NEYMAR AGOMEWA PSG
MMILIKI wa PSG, Nasser Al Khelaifi, hayupo tayari kuona mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27, akiondoka klabuni hapo majira haya ya joto. ***(Marca)***

### MADDISON LULU MAN UNITED
Manchester United inapewa nafasi zaidi ya kumsajili kiungo wa Leicester City, Muingereza James Maddison, 22, majira haya ya joto. ***(Independent)***

### CHILWELL AMTAJA GUARDIOLA
BEKI wa kushoto wa Leicester, Ben Chilwell, 22, amesema kocha wa Manchester City, Pep Guardiola amemwambia alivutiwa sana naye msimu huu. ***(Mirror)***

### BAYERN YAISHUKIA CITY KWA SANE
RAIS wa Bayern Munich, Uli Hoeness amesema Manchester City ni "wendawazimu" katika kumthaminisha winga Mjerumani Leroy Sane, 23, ambaye anatakiwa na mabingwa hao wa Bundesliga majira haya ya joto. ***(Star)***



# PAMBA YAMPASUA KICHWA MAXIME

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza wa mchujo ['Play Off'] dhidi ya Pamba ya jijini Mwanza, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema mambo bado ni magumu kwa upande wake katika kuhakikisha anainusuru timu hiyo isishuke daraja.

Kagera Sugar inatarajia kurudiana na Pamba Jumamosi Juni 8, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba na mshindi atakata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime, alisema mechi ya juzi ilikuwa ngumu na yenye ushindani kuanzia dakika ya kwanza hadi ya mwisho ya mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana.

Maxime alisema timu yake ilitengeneza nafasi nyingi, lakini washambuliaji wake walishindwa kuzitendea haki na kuufanya mchezo kumalizika kwa sare ya bila kufungana.

Beki na nahodha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar alisema wanachotakiwa kukifanya katika mchezo wa marudiano ni kuongeza umakini na kutoruhusu wapinzani wao kutangulia kupata bao.

"Mechi ilikuwa ngumu sana, nasikitika tumetengeneza nafasi nzuri, lakini hatukuzitumia, ndio mchezo wa mpira ulivyo, nafasi bado tunayo, tunatakiwa kujiandaa kupambana," Maxime alisema.

Naye Mkurugenzi wa Ufundi wa Pamba, Muhibu Kanu, alisema mabadiliko ya siku ya mchezo yalichangia kuharibu mipango ya kikosi chake, lakini akakiri pia baadhi ya wachezaji walionao hawana uzoefu ukilinganisha na wapinzani wao.

Kanu alisema wataenda Bukoba kwa lengo moja la kupambana ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kutimiza ndoto yao ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo wameikosa kwa muda mrefu sasa.

Mechi nyingine ya mchujo itakayochezwa Jumamosi itakuwa ni kati ya Mwadui FC dhidi ya Geita Gold FC ambazo pia zilitoka sare tasa kwenye mechi ya mkondo wa kwanza.




Mkuu wa Bidhaa na Huduma wa Tigo, David Umoh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa Promosheni ya Soka la Afrika, ambapo wateja 10, watajishindia tiketi za kwenda Misri kushuhudia Kombe la Mataifa ya Afrika pamoja na mamilioni ya fedha. Kulia ni Mtaalamu wa Huduma za Ziada wa Kampuni hiyo, Ikunda Ngowi. **PICHA: JOHN BADI**

# Tigo kugawa mamilioni, kupeleka 10 Afcon Misri

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI zikiwa zimebaki siku 18 kabla ya timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Star' kushuka dimbani kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri kuivaa Senegal, wateja wa Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo wamepewa nafasi ya kujishindia safari ya kwenda kushuhudia michuano hiyo pamoja na kushinda fedha taslimu kupitia promosheni mpya inayojulikana kama "Soka la Afrika".

Kupitia promosheni hiyo, wateja 10 wa Tigo wataweza kujishindia tiketi ya safari ya kwenda na kuingia uwanjani kushuhudia mashindano hayo makubwa barani Afrika, yanayotarajiwa kuanza Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu, ambapo Taifa Stars mbali na Senegal pia itavaana na Algeria na majirani zao Harambee Stars ya Kenya katika Kundi lao la C.

Mbali na kujishindia tiketi hizo 10 ambapo washindi watalipiwa kila kitu, pia Tigo imetoa fursa kwa wateja wake kujishindia fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni 50 kupitia promosheni hiyo ya Soka la Afrika iliyozinduliwa jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa promosheni hiyo, Mkuu wa Bidhaa na Huduma wa kampuni hiyo, David Umoh, alisema Soka la Afrika ipo mahsusi kwa ajili ya kuwazawadia wateja waaminifu wa Tigo ambao siku zote wamekuwa mstari wa mbele kutumia bidhaa na huduma za kampuni hiyo.

Alisema ili wateja waweze kushiriki katika promosheni hiyo na kujipatia nafasi ya kuwa mamilionea pamoja na kushinda tiketi, watatakiwa kutuma neno SOKA kwenda 15670 au kutembelea tovuti ya www.tigosports.co.tz ili kuweza kujibu maswali yanayohusu mashindano hayo yanayofanyika nchini Misri na Taifa Stars ikishiriki kwa mara ya kwanza baada ya miaka 39.

"Tunaamini kwa kutumia mashindano haya, tunaweza kupata fursa nzuri kutoa habari, elimu na burudani kwa kutumia jukwaa la mawasiliano na michezo," alisema Umoh.

Fainali za Mataifa ya Afrika, ni mashindano makubwa kuliko yote barani Afrika ambayo yanawaleta pamoja wachezaji wa Kiafrika wanaoshiriki ligi kubwa na zenye ushindani ndani na nje ya bara hili.

"Tunaamini itakuwa ni jambo zuri kwa wateja wetu kupata nafasi ya kwenda kushuhudia mashindano haya makubwa ikiwa ni pamoja na kushangilia timu yetu ya Taifa Stars itakayotuwakilisha. Tunawatakia kila kheri," aliongeza Umoh.

Kwa upande wa zawadi za fedha, Umoh alisema: "Zaidi ya wateja 100 watashinda fedha kila siku, kila wiki na kila mwezi kwa muda wa miezi mitatu."

Umoh aliwahimiza wateja wa Tigo kushiriki katika promosheni hiyo na kusema kuwa kadiri mteja anapojibu maswali, ndivyo anavyozidi kujiongezea pointi na nafasi kubwa zaidi ya kushinda tiketi ya kwenda Misri au mamilioni ya pesa.

## Namungo yamng'oa Bigirimana Alliance

**Na Mwandishi Wetu**

KAZI imeanza! Ili kuanza kukisuka upya kikosi chake, uongozi wa Namungo FC ya Ruangwa mkoani Lindi imetangaza kumsajili rasmi mshambuliaji, Blaise Bigirimana kutoka Alliance FC ya jijini Mwanza, imefahamika.

Namungo FC pamoja na Polisi Tanzania tayari zimeshapanda daraja na msimu ujao zitashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, huku zikisubiri timu nyingine mbili ambazo zitajulikana Juni 8, mwaka huu baada ya kumalizika kwa mechi mbili za mchujo ['Play Off'] kati ya Kagera Sugar dhidi ya Pamba na Mwadui FC dhidi ya Geita FC, ambapo mechi zote za mkondo wa kwanza zilimalizika kwa sare tasa.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zilieleza kuwa Bigirimana ambaye ni raia wa Burundi amesaini mkataba wa mwaka mmoja na hiyo inatokana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya mshambuliaji huyo na klabu hiyo.

Alisema kuwa klabu yake itahakikisha inafanya usajili kwa kuzingatia ripoti ya ufundi iliyotolewa na makocha wao, kwa sababu wanataka kutoa ushindani katika mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao watakazocheza.

## Shaali: Uongozi ZFF sasa basi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**


Aliyekuwa mgombea wa Umakamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Khamis Shaali ameachana rasmi na uongozi katika vyama vya soka baada ya kushindwa katika uchaguzi huo uliofanyika Juni 2, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Uwanja wa Amaan jana, alisema amechukua maamuzi hayo baada ya kupata matokeo mabaya ya kura tatu sawa na asilimia 10.7 kati ya wajumbe 28 waliopiga kura hizo. Alisema amejitathmini kuhusiana na matokea hayo mabaya aliyoyapata hivyo kujiona kwamba hakubaliki katika soka la Zanzibar.

"Kura tatu nilizozipata kama ni mtihani wa shuleni, basi hapo mimi nimepata sifuri, imeniuma sana na nilishindwa hata kulala vizuri nikiyafikiria matokeo yale, hii imemaanisha kwamba sikubaliki katika soka hata katika mkoa wangu ambao mimi ni mjumbe wa mkoa pia naona sikubaliki hata kidogo kuwa kiongozi hii imeniuma sana," alisema.

Aidha, alisema ana mpango wa kujiuzulu nafasi ya ujumbe wa Chama cha Soka Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo anatarajia kuandika rasmi barua kuhusu mpango wake huo na kusema kuwa kuanzia sasa hatogombea tena nafasi yoyote ya uongozi katika vyama vya soka iwe mikoa, wilaya na hata Taifa.

Michezo
Jumatano Juni 5, 2019
Nipashe



Mourinho awatoa Messi, Ronaldo Ballon d'Or 2019

HABARI UK 30

UZI WA 2019/20...




Wachezaji wa Barcelona, mshambuliaji Lionel Messi na beki wa kati, Gerard Pique (kulia), wakiwa ndani ya uzi mpya utakaotumiwa na klabu hiyo kwenye mechi za nyumbani kwa msimu mpya wa 2019/2020. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAZIPELEKA YANGA SC, KMC CAF

Ni msimu wa 2019/2020, Rais TFF afunguka, Shirikisho la Soka Afrika latoa sababu Tanzania kuingiza timu nne kuwa ni...

**Na Mwandishi Wetu**

JITIHADA na kujituma kwa Klabu ya Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na hatimaye kuiwezesha Tanzania kufikisha pointi 18, hivyo kushika nafasi ya 12 bora kwenye viwango vya ubora vya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), zimezaa matunda baada ya shirikisho hilo kutangaza sasa Tanzania itaingiza jumla ya timu nne katika mashindano yake kwa msimu mpya wa 2019/2020.

Katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyomalizika wiki iliyopita kwa Esperance ya Tunisia kutetea ubingwa huo, Simba iliishia hatua ya robo fainali baada ya kutolewa na TP Mazembe kwa jumla ya mabao 4-1.

Hata hivyo, kabla ya Simba kushiriki michuano hiyo, Tanzania ilikuwa na pointi tatu tu zilizopatikana kutokana na Yanga kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa misimu mitatu mfululizo ikiambulia kuvuna pointi moja kila msimu.

Lakini juhudi za Simba ambayo ilivuka hatua ya makundi na kucheza robo fainali, ziliiwezesha Tanzania kuvuna pointi 15, hivyo kufikisha jumla ya alama 18, zilizoiwezesha kushika nafasi ya 12 ya ubora ya viwango vya Caf, nafasi ambayo inatoa fursa kwa nchi kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa; mbili Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyopokelewa jana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), Caf imethibitisha kuwa Tanzania itakuwa na timu nne katika mashindano ya kimataifa kwa msimu wa 2019/2020, ambapo sasa timu mbili zitashiriki kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na mbili Kombe la Shirikisho.

Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu zilizofanyiwa marekebisho na Kamati ya Utendaji baada ya kupatikana nafasi nne, timu za Tanzania zitakazoiwakilisha kwenye mashindano hayo ni Simba na Yanga ambazo zitapeperusha bendera hiyo Ligi ya Mabingwa (Caf CL), huku Azam FC na KMC zikiiwakilisha nchi Kombe la Shirikisho (Caf CC).

KMC imepata nafasi hiyo ya kucheza Kombe la Shirikisho kwa mujibu wa kanuni hiyo ambayo inatamka kuwa kama timu iliyomaliza nafasi ya tatu itakuwa ndiyo bingwa wa Kombe la FA, basi mshindi wa nne atapata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho kwa sababu bingwa wa FA anaiwakilisha nchi kwenye mashindano hayo.

Wakati huo huo, tayari taarifa ya Caf imefungua dirisha kwa mashirikisho kusajili timu kupitia mtandao wa CMS na mwisho wa usajili ni Juni 30, mwaka huu, ambapo TFF inatakiwa iwe imesajili timu zitakazoshiriki kwenye mashindano ya kimataifa msimu wa 2019/2020.

Rais wa TFF, Wallace Karia, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, amezitaka timu zilizopata nafasi hiyo, kusajili kwa umakini na kujiandaa kwa mashindano ya Caf ili kutopoteza nafasi hiyo ya kuendelea kuingiza timu nne katika mashindano hayo ya Caf.

## Kinara wa mabao Uganda atua Simba

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI mabosi wa Yanga wamefanikiwa kumpa mkataba mpya beki wao, Gadiel Michael ambaye msimu uliopita aliisaidia klabu hiyo kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wenyewe wamemnasa mshambuliaji bora wa Ligi Kuu ya Uganda, Juma Bulinya kutoka Polisi Uganda.

Bulinya ambaye yuko katika kikosi cha Uganda kinachokwenda Afcon, ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu Uganda baada ya kufunga mabao 19, ametua katika rada za Simba ambayo msimu ujao itashiriki tena mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kiongozi mmoja wa Simba aliliambia gazeti hili kuwa mazungumzo na mshambuliaji huyo ambaye ni askari yako katika hatua za mwisho.

Kwa upande wa Gadiel aliyejiunga na Yanga akitokea kwa mabingwa wa Kombe la Kagame na Kombe la FA msimu huu, Azam FC, taarifa kutoka kwa viongozi wa klabu yake hiyo ya sasa, zinasema beki huyo ambaye pia ameitwa kikosi kitakachokwenda fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), amesaini mkataba wa miaka mitatu.

"Kama ingekuwa ni kwa Wazungu wangesema "Deal Done", tayari kwa Gadiel, tunaendelea na mazungumzo na wachezaji wengine," kilisema chanzo chetu.

Nyota huyo ambaye aliitikisa safu ya ulinzi ya Azam FC baada ya kubainika amejiunga na Yanga, pia alitajwa kutakiwa na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, lakini mambo yameendelea kuwa mazuri kwa upande wa Yanga.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alipoulizwa kuhusu kumaliza mchakato wa kumpa mkataba mpya beki huyo, alisema ni mapema kueleza hatua ambayo klabu yake imefikia katika kuzungumza na wachezaji inaowahitaji.

"Bado hatujaanza kusajili wachezaji wa ndani, kwa sasa tunahakikisha tunawapata wachezaji wa nje ambao mwalimu amewahitaji, baada ya kumaliza ndio tutawageukia wazawa, wengi wao tulishakubaliana vitu vya msingi, imebakia kuwapa mikataba," alisema Mwakalebela.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042